# SHERIA YA (UTAFUTAJI NA UCHIMBAJI) MAFUTA NA GESI ASILIA, 2016

---

## MPANGILIO WA VIFUNGU

**VIFUNGU** **MAELEZO**

### SEHEMU YA KWANZA
### VIFUNGU VYA AWALI


1. Jina fupi na kuanza kutumika.
2. Matumizi.
3. Ufafanuzi.


### SEHEMU YA PILI
### HAKI ZA MAFUTA NA GESI ASILIA KUSIMAMIWA NA SERIKALI


4. Dhamana ya haki ya mafuta na gesi asilia.
5. Makubaliano na Serikali.
6. Kazi na wajibu wa Waziri.


### SEHEMU YA TATU
### MAMLAKA YA UDHIBITI (UTAFUTAJI NA UCHIMBAJI) WA MAFUTA NA GESI ASILIA NA KAMPUNI YA MAENDELEO YA MAFUTA NA GESI ASILIA


7. Mamlaka ya Udhibiti (Utafutaji na Uendelezaji) wa Mafuta na Gesi Asilia.
8. Kazi na Wajibu wa Mamlaka.
9. Miongozo ya Waziri.
10. Miongozo ya Mamlaka kwa Kampuni na Mkandarasi.
11. Utii wa Miongozo.
12. Bodi ya Wakurugenzi.
13. Kazi za Bodi.
14. Uwezo wa Bodi.
15. Sifa ya Mwenyekiti na Wajumbe wa Bodi.
16. Mienendo ya Bodi.
17. Uteuzi wa Mkurugenzi Mwendeshaji.
18. Kazi za Mkurugenzi Mwendeshaji.
19. Idara na Vitengo vya Mamlaka.
20. Wafanyakazi wa Mamlaka.
21. Kinga dhidi ya Wajumbe wa Bodi na Maafisa wa Mamlaka.
22. Wajibu wa kutokutoa taarifa.

23. Fedha za Mamlaka.
24. Wajibu wa utendaji wa kusimamia misingi ya kifedha.
25. Uwezo wa kufungua na kuendesha akauti za benki.
26. Uwezo wa kukopa.
27. Makadirio.
28. Mwaka wa Fedha.
29. Hesabu.
30. Ukaguzi.
31. Ripoti ya mwaka.
32. Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asilia.

**SEHEMU YA NNE**
**SHUGHULI ZA UTAFUTAJI NA UENDELEZAJI WA MAFUTA NA GESI ASILIA**

33. Mgao wa eneo la ardhi na vitalu.
34. Ufunguzi, utambuzi mpya na ufungaji wa maeneo.

***(a) Kibali cha Utafiti wa Awali***

35. Ombi la kibali cha utafiti wa awali.
36. Muda wa kibali cha utafiti wa awali.
37. Kutoa kibali cha utafiti wa awali.
38. Shughuli zilizoidhinishwa na kibali cha utafiti wa awali.
39. Kuanza kwa shughuli za utafiti wa awali.
40. Kusitishwa kwa ruhusa ya utafiti wa awali.
41. Kusamehe kwa kumaliza kazi.
42. Kumalizika kwa kibali.
43. Umiliki wa taarifa.
44. Vikwazo vya rasilimali zisizokuwa mafuta na gesi asilia.
45. Haki za kipekee za Kampuni.
46. Watu wanaoweza kuingia ubia na Kampuni.
47. Shughuli za pamoja.
48. Mikataba katika kutoa haki.
49. Utaratibu wa zabuni.
50. Uhifadhi wa vitalu.

***(b) Leseni ya Utafutaji Mafuta na Gesi Asilia***

51. Uwezo wa Waziri wa kutoa leseni ya utafutaji wa mafuta na gesi asilia.
52. Kukataa kutoa leseni ya utafutaji wa mafuta na gesi asilia.
53. Notisi ya maamuzi ya maombi ya leseni ya utafutaji wa mafuta na gesi.
54. Mambo yatakayoainishwa katika leseni ya utafutaji wa mafuta na gesi.
55. Haki na wajibu uliotolewa na leseni ya utafutaji mafuta na gesi asilia.
56. Uhalali wa masharti ya leseni ya utafutaji mafuta na gesi asilia.

57. Ombi la kuongeza muda wa leseni ya utafutaji wa mafuta na gesi asilia.
58. Maombi ya kuongeza muda kwa eneo lililopunguzwa.
59. Kutolewa au kukataliwa kuongeza muda.
60. Masharti ya kutoa leseni ya utafutaji wa mafuta na gesi asilia.
61. Kutolewa taarifa kwa ugunduzi wa mafuta na gesi asilia .
62. Tathmini na uchunguzi wa maeneo.

### *(c) Leseni ya Uendelezaji*

63. Maombi ya leseni ya uendelezaji.
64. Ushughulikiaji wa ombi.
65. Masharti ya utoaji wa leseni ya Uendelelzaji.
66. Notisi ya uamuzi kuhusiana na ombi la leseni ya uendelezaji.
67. Haki za mwenye leseni ya uendelezaji.
68. Muda wa leseni ya uendelezaji.
69. Ombi la kuongeza muda wa leseni ya uendelezaji.
70. Kutoa au kukataa kuengeza muda wa leseni ya uendelezaji.
71. Kibali cha uzalishaji.
72. Uzalishaji wa pamoja.
73. Masharti ya kusimamia haki ya leseni.
74. Kusalimisha leseni.
75. Athari za hati ya kusalimisha.
76. Usitishaji au ufutaji leseni.

### *(d) Masharti ya jumla*

77. Rajisi ya mafuta na gesi asilia.
78. Maslahi katika leseni kuwekwa katika maandishi.
79. Uhaulishaji wa maslahi ya leseni kuthibitishwa na Waziri.
80. Waziri anaweza kutoa maelezo.
81. Taarifa, maelezo na ripoti.
82. Utunzaji wa kumbukumbu.
83. Wajibu wa kusitisha leseni na kibali cha awali.
84. Upatikanaji wa taarifa kwa umma.
85. Usiri wa taarifa.
86. Maelezo ya ziada kuwasilishwa.
87. Kushindwa kuwasilisha maelezo.
88. Fursa ya mtu wa tatu.
89. Wajibu wa usambazaji nchini.
90. Tathmini ya bei ya mafuta na gesi asilia.
91. Uzowefu wa kazi kwa Mkandarasi.
92. Adhabu ya ukiukaji.
93. Ukarabati wa miundombinu.
94. Uchimbaji wa mafuta na gesi asilia karibu na mipaka.

95. Utafiti wa visima.
96. Udhibiti wa mkandarasi.
97. Uwezo wa kuingia.
98. Haki ya matumizi ya ardhi kwa mkaazi halali.
99. Fidia kwa usumbufu.
100. Haki ya ardhi ambayo haijagaiwa.
101. Mrahaba wa mafuta na gesi asilia.
102. Ada ya mwaka.
103. Malipo ya ziada.
104. Kodi.
105. Mipaka ya urejeshaji wa gharama.
106. Masharti ya malipo.
107. Adhabu kwa ucheleweshaji wa malipo.
108. Urejeshwaji wa malipo chini ya Sheria hii.
109. Dhamana ya utekelezaji.

## SEHEMU YA TANO
## UKOMO WA SHUGHULI ZA UTAFUTAJI WA MAFUTA NA GESI ASILIA

110. Mpango wa ukomo wa shughuli za utafutaji wa mafuta na gesi asilia.
111. Mfuko wa ukomo wa shughuli za utafutaji wa mafuta na gesi asilia.
112. Taarifa ya kusitisha matumizi.
113. Kuondosha miundombinu ya ukomo wa shughuli za mafuta na gesi asilia.
114. Uondoshaji wa mali za Kampuni na Mkandarasi.
115. Uondoshaji na uuzaji wa mali.
116. Dhima ya fidia ya uondoshaji wa ukomo wa miundombinu ya shughuli za mafuta na gesi asilia.
117. Kuchukuliwa kwa miundombinu kwa Serikali.

## SEHEMU YA SITA
## AFYA NA USALAMA KAZINI NA MISINGI YA MAZINGIRA

118. Afya na usalama kazini.
119. Mahitaji ya jumla kwa ajili ya maandalizi ya dharura.
120. Maandalizi ya dharura dhidi ya mashambulizi ya makusudi.
121. Maeneo ya usalama.
122. Usitishaji wa shughuli za mafuta na gesi asilia.
123. Tume ya uchunguzi.
124. Kufuata misingi ya mazingira.
125. Athari za uchafuzi na uharibifu wa mazingira.
126. Dhima kwa uchafuzi na uharibifu wa Mazingira.
127. Dhima ya kuharibu uchafuzi wa mazingira bila ya leseni au kibali.
128. Madai ya fidia.
129. Madai ya fidia kwa uchafuzi wa mazingira.
130. Mamlaka.
131. Usimamizi wa mazingira.

132. Uvujaji wa mafuta na gesi asilia.
133. Umwagikaji wa Mafuta na gesi asilia na vinavyotokana navyo.

**SEHEMU YA SABA**
**THAMANI YA WADAU WA NDANI, JUKUMU LA USHIRIKISHAJI JAMII NA KIAPO CHA UADILIFU**

134. Maendeleo ya jamii na masharti ya bidhaa na huduma.
135. Mafunzo na ajira.
136. Mafunzo na uhaulishaji taaluma.
137. Jukumu la ushirikishaji wa jamii.
138. Kiapo cha uadilifu.

**SEHEMU YA NANE**
**MAKOSA NA ADHABU**

139. Kumzuia Afisa aliyeidhinishwa.
140. Kuzuia Kampuni na mkandarasi.
141. Makosa yaliyofanywa na taasisi au mtu binafsi.
142. Amri ya kutaifisha.
143. Kwenda kinyume na maamuzi na kutoa amri chini ya Sheria hii
144. Makosa ya jumla.
145. Makosa na adhabu.
146. Muunganisho wa Makosa kwa Mamlaka.

**SEHEMU YA TISA**
**UTATUZI WA MIGOGORO**

147. Mamlaka inaweza kutatua migogoro.
148. Utekelezaji wa hukumu na amri za Mamlaka.
149. Kutenganishwa kwa uwezo wa Mahakama.
150. Taratibu zinazohusiana na madai.

**SEHEMU YA KUMI**
**MASHARTI YA MPITO**

151. Mikataba iliyoingiwa awali.

**SEHEMU YA KUMI NA MOJA**
**MASHARTI YA JUMLA**

152. Kutumika leseni kama dhamana.
153. Mgogoro wa maslahi.
154. Mfuko wa mapato ya mafuta na gesi asilia.
155. Kanuni.

**JADWELI LA I - II**

SHERIA NAMBA 6 YA 2016

NIMESAINI

A Shein

{DR. ALI MOHAMED SHEIN}

RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI

WA BARAZA LA MAPINDUZI

15th November, 2016

# SHERIA YA USIMAMIZI (UTAFUTAJI NA UCHIMBAJI) WA MAFUTA NA GESI ASILIA, KUANZISHA MAMLAKA YA UDHIBITI WA SHUGHULI ZA UTAFUTAJI NA UCHIMBAJI WA MAFUTA NA GESI ASILIA, KUANZISHA KAMPUNI YA MAENDELEO YA MAFUTA NA KUHAKIKISHA UWAJIBIKAJI WA TAASISI ZA MAFUTA NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NAYO

---

**IMETUNGWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

## SEHEMU YA KWANZA
## VIFUNGU VYA AWALI

Jina fupi na kuanza kutumika.

**1.** Sheria hii itajulikana kama ni Sheria ya (Utafutaji na Uchimbaji) Mafuta na Gesi Asilia, 2016 na itaanza kutumika mara baada ya Waziri kutangaza katika Gazeti Rasmi la Serikali.

Matumizi.

**2.** Sheria hii itatumika katika masuala ya mafuta na gesi asilia yaliyokuwepo katika eneo la ardhi, visiwa, maji ya ndani, eneo la bahari, mipakani, ukanda wa uchumi na eneo lolote kama ilivyoainishwa katika Katiba na lililopatikana kutokana na sheria nyengine yoyote inayotumika, na kama litakavyoongezwa na kutambulika na sheria ya kimataifa.

Ufafanuzi.

**3.** Katika Sheria hii, isipokuwa kama maelezo yatahitaji vyenginevyo:

"ardhi" maana yake ni kama ilivyotafsiriwa katika Sheria inayohusiana na masuala ya Umiliki wa Ardhi na inajumuisha ardhi iliyo chini ya maji, kontinentali shelfu na eneo lililoengezwa la kontinentali shelfu;

"Baraza la Mapinduzi Zanzibar" maana yake ni Baraza la Mawaziri kama ilivyotafsiriwa na Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984;

"Bodi" maana yake ni Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 12(1) cha Sheria hii;

"eneo la bahari" maana yake ni eneo la bahari lenye kina cha maji kilichozidi mita 200;

"eneo la leseni" maana yake ni kitalu au sehemu iliyoainishwa katika mkataba wa mafuta na gesi asilia;

"eneo la makubaliano" maana yake ni eneo ambalo limetolewa leseni kwa ajili ya utafutaji au uendelezaji wa mafuta na gesi asilia kwa Kampuni au kama itakavyoelezwa katika mkataba husika;

"eneo la utafutaji" maana yake ni eneo linalojumuisha vitalu ambavyo au inaweza kuhusisha leseni ya utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia;

"fukwe" maana yake ni eneo lote, nchi kavu na maji lenye kina cha maji kisichozidi mita mia 200;

"gesi asilia" maana yake ni haidrokaboni yoyote iliyozalishwa kutoka eneo la mkataba kutokana na msukumo wa hewa na kiwango cha nyuzi joto 60 faranihaiti katika mfumo wa hewa juu ya kisima, na inajumuisha mabaki ya gesi baada ya uchimbaji wa haidrokaboni ya maji maji, gesi iliyochanganyika na isiyo changanyika, viasilia vyake vyote vilivyozalishwa kutoka kisima chochote katika mkataba na vile visivyokuwa na viasilia vya haidrokaboni;

"gesi husishwa" maana yake ni gesi asilia iliyopo pamoja na mafuta ghafi ndani ya hifadhi na inajumuisha gesi ambayo inapatikana juu ya mafuta ghafi;

"gesi isiyochanganyika" maana yake ni gesi asilia iliyozalishwa kutokana na hifadhi ya mafuta na gesi asilia iliyoendelezwa awali kwa ajili ya kuzalisha gesi asilia;

"gesi" maana yake ni mchanganyiko wa gesi ya haidrogini unaopatikana katika hali ya kimaumbile ya gesi;

"haidrokaboni" maana yake ni uwepo wa kimaumbile kaboni-haidrogini baadhi ya wakati mchanganyiko wa oksigini ikiwa katika hali ya ugumu, umaji maji au gesi;

"Kampuni" maana yake ni Kampuni ya maendeleo ya mafuta ya Zanzibar inayoazishwa chini ya kifungu cha 32(1) cha Sheria hii;

"Katiba" maana yake ni Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984;

"kazi za uendelezaji" maana yake ni shughuli zinazohusiana na uzalishaji wa mafuta na gesi asilia na zinajumuisha kazi za kuandaa mpango wa maendeleo na kazi zinazofanywa baada ya kupewa leseni ya uendelezaji inayohusiana na uendelezaji wa eneo na itajumuisha:

(a) tafiti za hifadhi, miamba na jiofizikia;

(b) uchimbaji wa visima vya uzalishaji na visima vya kuongeza nguvu za uzalishaji; na

(c) ubunifu, ujenzi, ufungaji, uunganishaji na majaribio ya awali ya vifaa, mabomba, mifumo, vifaa, viwanda na shughuli nyengine zote muhimu kwa ajili ya kuzalisha na kukiwezesha kisima kufanya kazi kuchukua, kuhifadhi, kuendesha, kusafirisha na kupokea mafuta na gesi asilia na kufanya majaribio ya kuongeza, kutengeneza upya na kazi nyengine zinazohitajika kwa ajili ya upatikanaji wa mafuta na gesi asili;

"kibali" maana yake ni kibali kilichotolewa chini ya Sheria hii na masharti ya mmiliki wa kibali yatafuatwa ipasavyo;

"kipindi cha utafutaji" maana yake ni muda uliotolewa kwa ajili ya kutekeleza shughuli za utafutaji wa mafuta na gesi asilia kama ulivyoelezwa katika leseni ya utafutaji wa mafuta na gesi asilia;

"kisima cha uendelezaji" maana yake ni kisima kilichochimbwa kwa ajili ya uzalishaji wa mafuta na gesi asilia kutoka katika ugunduzi wa kibiashara na unajumuisha visima vya tathmini vilivyokamilika kwa uzalishaji au visima vya kuongeza nguvu za uzalishaji;

"kisima cha utafutaji" maana yake ni kisima kilichochimbwa kwa ajili ya shughuli za utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia isipokuwa kisima cha tathmini;

"kisima" maana yake ni kisima kilichochimbwa kwa ajili ya utafutaji, tathmini, uendelezaji, shughuli za uendelezaji na haitajumuisha mashimo yanayotumika kwa shughuli za mitetemo;

"kitenganishi" maana yake ni mtambo unaotumika kwa ajili ya kutenganisha maji maji na gesi yanayotokana na visima vya mafuta na gesi asilia;

"kontinentali shelfu" maana yake ni eneo linaloanzia ufukwe wa bahari hadi eneo la bahari ya Zanzibar ambapo ardhi ya chini ya bahari inayokwenda zaidi ya bahari ya ndani ya Zanzibar kupitia mtiririko wa asili wa eneo la Zanzibar au kwenye eneo la mwisho wa bahari ya Zanzibar au meli 200 za bahari kutoka ukingo wa bahari au isipokuwa kama itatokana na kanuni za sheria ya kimataifa zinazohusiana na kontinentali shelfu zaidi meli 200 za bahari kutoka kingo au kutokana na makubaliano na nchi jirani;

"kutathmini" maana yake ni kazi zinazofanywa baada ya ugunduzi wa mafuta na gesi asilia kwa lengo la kuainisha viwango vya mafuta, gesi asilia na hifadhi zinazohusiana na ugunduzi huo kama ni wa kibiashara au vyenginevyo na inajumuisha:

(a) uchimbaji wa visima na kuvifanyia majaribio;

(b) kukusanya sampuli za miamba na hifadhi za mafuta; na

(c) kufanya tafiti za ziada na kupata taarifa za sayansi ya miamba na taarifa nyenginezo pamoja na kuzifanyia uchambuzi wa taarifa hizo;

"leseni ya uendelezaji" maana yake ni leseni iliyotolewa chini ya kifungu cha 64 cha Sheria hii;

"leseni ya utafutaji" maana yake ni leseni iliyotolewa chini ya kifungu cha 51 cha Sheria hii;

"leseni" maana yake ni leseni iliyotolewa chini ya Sheria hii;

"mafuta na gesi asilia" maana yake ni mkusanyiko wowote wa kimaumbile wa haidrokaboni ukiwa katika hali ya gesi, maji maji, hali ya ugumu au mchanganyiko wowote wa kimaumbile wa haidrokaboni lakini haujumuishi mkaa wa mawe au kitu chochote kinachoweza kutokana na mkaa wa mawe au miamba;

"mafuta" maana yake ni umaji maji wa asili uliofanyika kutokana na haidrokaboni (mafuta ghafi);

"makubaliano ya mafuta na gesi asilia" maana yake ni makubaliano baina ya Serikali, Kampuni ya Mafuta ya Taifa na mkandarasi anaehusika na eneo la leseni ya mafuta na gesi asilia;

"makubaliano ya pamoja" maana yake ni makubaliano yaliyofanywa baina ya pande zinazojumuisha mkandarasi na Kampuni;

"Mamlaka" maana yake ni Mamlaka ya Udhibiti wa Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 7(1) cha Sheria hii;

"mazingira" maana yake ni kama ilivyoelezwa chini ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Zanzibar;

"muombaji" maana yake ni Kampuni inayomiliki leseni;

"mfumo usiounganishwa" maana yake ni mfumo ambao haukuunganishwa na mfumo wowote unaomilikiwa na mtu asiyekuwa mmiliki wa mfumo wa awali au mshiriki;

"mkandarasi mdogo" maana yake ni taasisi yoyote ya biashara iliyokodiwa na mkandarasi kufanya kazi yote au sehemu ya kazi za uendeshaji wa mafuta na gesi asilia kama zilivyothibitishwa na mkandarasi katika masharti ya makubaliano;

"mkandarasi" maana yake ni mtu au kampuni ambae maslahi yake ya leseni yanaweza kuhaulishwa katika makubaliano husika;

"Mkurugenzi Mwendeshaji" maana yake ni Mtendaji Mkuu wa Mamlaka alieteuliwa kwa masharti ya kifungu cha 17(1) cha Sheria hii;

"mpango wa maendeleo" maana yake ni mpango unaoambatana na maombi ya leseni ya uendelezaji yanayojumuisha maombi ya ujenzi, uanzishaji na utekelezaji wa vifaa na huduma kwa ajili ya upatikanaji, uendelezaji, uhifadhi, usafirishaji wa mafuta na gesi asilia kutoka katika eneo la uendelezwaji unaopendekezwa;

"mshirika" maana yake mtu yeyote ambae moja kwa moja au vyenginevyo, kupitia mtu mmoja au zaidi, anasimamia au anasimamiwa au yupo chini ya mamlaka ya usimamizi wa mtu mwengine;

"mwendeshaji" maana yake ni mtu aliyepewa jukumu kama ni mwendeshaji chini ya makubaliano ya pamoja na yanayotekelezwa na watu wanaojumuisha mkandarasi au makubaliano ya uendeshaji yanayotekelezwa na shirika na mkandarasi kwa mujibu wa makubaliano husika;

"Rais" maana yake ni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi;

"rasilimali" maana yake ni mkusanyiko au upatikanaji wa vifaa vyenye maslahi ya kiuchumi ardhini;

"ruhusa ya uzalishaji" maana yake ni ruhusa iliyotolewa chini ya kifungu cha 71(1) cha Sheria hii;

"sehemu ya upokeaji" maana yake ni sehemu mahsusi iliyokubalika katika mpango wa maendeleo au katika mkataba wa mafuta kwa ajili ya kupokea kiwango cha ubora wa mafuta na gesi asilia ndani au nje ya eneo la makubaliano kwa malengo maalum yakiwemo uuzaji, uhifadhi au usafishaji;

"sehemu za graticular" maana yake ni kama ilivyoelezwa katika kifungu cha 33 cha Sheria hii;

"Serikali" maana yake ni Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar;

"shughuli za utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia" maana yake ni shughuli zote zinazohusisha masuala kabla ya utoaji leseni, wakati wa utoaji leseni, utafiti, tathmini, uendelezaji, uzalishaji na ukomo wa shughuli za mafuta na gesi asilia;

"shughuli za utafutaji" maana yake ni shughuli yoyote inayohusiana au inayohusishwa na utafutaji wa mafuta na gesi asilia;

"shughuli za uzalishaji" zinajumuisha:

(a) uendeshaji, utowaji huduma, matengenezo na ukarabati wa visima vilivyokamilika, zana, mabomba, mifumo, nyenzo, viwanda vilivyojengwa na kutumika baada ya uendelezaji wa shughuli za mafuta na gesi asilia;

(b) shughuli zote zinazohusiana na mipango, ratiba, usimamizi, upimaji, majaribio na mtiririko wa mwenendo wa mafuta, kusarifu, kutenganisha, kusafirisha, kuhifadhi, kusambaza mafuta na gesi asilia kutoka kwenye hifadhi za mafuta na gesi asilia zilizo chini ya ardhi kwenda katika kituo husika na shughuli zote muhimu kwa ajili ya uzalishaji na uuzaji wa mafuta na gesi asilia; na

(c) upatikanaji wa mali na huduma zinazohitajika kwa ajili ya uzalishaji wa mafuta na gesi asilia na shughuli zote za kufikia ukomo wa uendeshaji wa mafuta na gesi asilia;

"taarifa za awali" maana yake ni uchunguzi uliofanywa kwa lengo la kupata taarifa au takwimu za sayansi ya ardhi katika shughuli za awali za mafuta na gesi asilia;

"takwimu za mafuta na gesi asilia" maana yake ni takwimu zote na taarifa zinazohusiana na ugunduzi wa awali, utafutaji, uendelezaji au uzalishaji wa mafuta na gesi asilia ukijumuisha sampuli ya miamba, sampuli za maji maji na mipango inayohusiana na uendeshaji wa masuala ya mafuta na gesi asilia;

"tathmini ya kisima" maana yake kisima chochote kilichochimbwa baada ya uguduzi wa mafuta na gesi asilia katika eneo la makubaliano kwa madhumuni ya kukadiria wingi na ukubwa wa eneo la mafuta na gesi asilia katika hifadhi ambayo ugunduzi huo umehusisha;

"thamani ya wadau wa ndani" maana yake ni kiwango cha ongezeko la thamani, kilichotokana na uchumi wa Zanzibar kupitia matumizi ya makusudi ya rasilimali watu, zana na huduma katika uendeshaji wa shughuli za mafuta na gesi asilia kwa madhumuni ya kuchochea uwekezaji na ushiriki wa ndani;

"uchimbaji" maana yake ni utoboaji wa ardhi kwa madhumuni ya kufanya ugunduzi, ili kuweza kupata ugunduzi au uzalishaji wa mafuta na gesi asilia uliogunduliwa;

"uchunguzi wa mawimbi mtetemo" maana yake ni utafiti wa kijio-fizikia unaotumia mawimbi mtetemo kwa ajili ya kupata sura halisi ya kijiologia ya sehemu inayoainisha sehemu na ukubwa wa upatikanaji wa hifadhi ya mafuta na gesi asilia;

"uendelezwaji wa eneo" maana yake ni sehemu ya ardhi katika kitalu au vitalu vilivyotolewa leseni kwa ajili ya uendelezaji wa shughuli za utafutaji wa mafuta na gesi asilia;

"uendeshaji wa mafuta na gesi asilia" maana yake ni uendeshaji na shughuli zote zinazohusiana na utafutaji, uthamini, uendelezaji na uzalishaji unaojumuisha ukomo wa shughuli za mafuta;

"uhifadhi wa mafuta na gesi asilia" maana yake ni mkusanyiko wa kimaumbile wa haidrokaboni ukiwa katika hali yoyote ile;

"ukomo wa shughuli za mafuta" maana yake ni uondoaji wa majengo, na vifaa vilivyotumika ikijumuisha mabomba, majukwaa na vitu vyengine vyovyote vilivyotumika katika utafutaji na uchimbaji katika eneo husika, usafishaji wa eneo, ufungaji wa visima ili viwe salama na uhuwishaji wa ardhi, kuhusiana na uondoaji au usitishaji au sehemu ya usitishaji wa shughuli za mafuta na gesi asilia katika eneo au sehemu ya eneo ya shughuli hizo;

"usafirishaji" maana yake ni usafirishaji wa mafuta na gesi asilia kutoka sehemu moja kwenda nyengine kwa kutumia mabomba, meli au njia nyengine;

"uwendeshaji wa pamoja" maana yake ni uwendeshaji wa shughuli za mafuta na gesi asilia ikijumuisha kampuni iliyoteuliwa kuchangia gharama au kufanya kazi za ukandarasi;

"uzoefu wa kimataifa wa mafuta na gesi asilia" maana yake ni uzoefu uliopo ambao unakubalika duniani kuwa ni mzuri, salama, wa uwazi na wenye ufanisi katika shughuli za utafutaji na uchimbaji;

"vifaa" maana yake ni kiwanda, jengo, au vifaa vinavyopatikana na kutumiwa katika shughuli za utafutaji wa mafuta na gesi asilia katika maeneo yaliyotolewa leseni;

"vitalu" maana yake ni eneo lililoelezwa chini ya kifungu cha 33 cha Sheria hii;

"Waziri" maana yake ni Waziri anaehusika na masuala ya mafuta na gesi asilia Zanzibar;

## SEHEMU YA PILI
## HAKI ZA MAFUTA NA GESI ASILIA KUSIMAMIWA NA SERIKALI

Dhamana ya haki ya mafuta na gesi asilia.

**4.-(1)** Kwa madhumuni ya masharti ya Sheria hii, mali yote na udhibiti wa mafuta na gesi asilia katika uasilia wake, yakiwa ndani, juu au chini ya ardhi yoyote au katika eneo la maji ya Zanzibar na eneo lilopatikana kutokana na sheria yoyote ya kimataifa itakuwa katika dhamana ya Serikali kwa niaba ya watu wa Zanzibar.

(2) Kwa ajili ya kuepuka utata, rasilimali ya mafuta na gesi asilia ni mali ya watu wa Zanzibar na Serikali itakuwa na haki zote zinazohusiana na mafuta na gesi asilia kwa maslahi ya watu wa Zanzibar.

Makubaliano na Serikali.

**5.** Serikali kupitia Kampuni inaweza kuingia katika makubaliano na mkandarasi au mtu yeyote anaejishughulisha na shughuli za mafuta na gesi asilia kwa kufuata Sheria hii kwa kuzingatia mambo yafuatayo:

(a) kutolewa kwa leseni;

(b) masharti ya kutoa, kufuta au kuongeza muda wa leseni;

(c) vitendo vya mtu anaejishughulisha na shughuli za mafuta na gesi asilia kwa niaba ya mtu yeyote amepatiwa leseni; na

(d) mambo mengine yoyote yanayotokea au kuhusiana na mambo yaliopo katika aya (a), (b) na (c).

Kazi na wajibu wa Waziri.

**6.-(1)** Waziri baada ya kushauriana na Mamlaka atatekeleza kazi na wajibu ufuatao:

.(a) atatoa, ataongeza muda, atasitisha na kufuta kibali kinachohusiana na utafutaji na uendelezaji wa mafuta na gesi asilia;

(b) ataandaa na kupitia upya kanuni zinazohusiana na mafuta na gesi asilia;

(c) ataruhusu kufanyika kwa uchunguzi pindipo ikitokea ajali au maafa yaliyosababishwa na shughuli za mafuta na gesi asilia;

(d) ataridhia makubaliano ya mafuta na gesi asilia;

(e) atatoa maelezo muhimu yanayohusiana na uendelezaji wa mafuta na gesi asilia mbele ya kamati za Baraza la Wawakilishi;

(f) ataridhia Mpango wa Uendelezaji na Mfumo wa Usimamizi wa Taarifa;

(g) atatayarisha sera zinazohusiana na mafuta na gesi asilia; na

(h) atafanya kazi nyengine zozote zinazohusiana na shughuli za uzalishaji wa mafuta na gesi asilia kama alivyotakiwa na Sheria hii au sheria nyengine.

(2) Bila ya kuathiri masharti ya jumla ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Waziri atasimamia kazi zifuatazo:

(a) kuongeza ushirikishaji wa jamii katika sekta;

(b) atahakikisha na kuendeleza uwazi katika sekta ndogo ndogo katika sekta ya mafuta na gesi asilia;

(c) atahakikisha mipaka sahihi ya maeneo yanayotumika katika shughuli za mafuta na gesi asilia;

(d) kwa kushauriana na Waziri mwenye dhamana ya fedha atahakikisha uwajibikaji, uwazi na ufanisi katika kuendeleza mfumo wa usimamizi wa mapato na ukusanyaji wa kodi na mipango ya matumizi;

(e) atajihusisha katika mikutano ya kimataifa ya uwekezaji na upatikanaji wa taarifa zinazohusiana na mafuta na gesi asilia;

(f) atawezesha mipango shirikishi baina ya sekta ya mafuta na gesi asilia na sekta nyengine za kiuchumi Zanzibar;

(g) atahakikisha kwamba kuna uwiano baina ya mahitaji ya ndani na usafirishaji wa nje ya nchi wa mafuta na gesi asilia ; na

(h) atahakikisha uelewa na ufahamu wa jamii katika masuala ya mafuta na gesi asilia.

## SEHEMU YA TATU
## MAMLAKA YA UDHIBITI (UTAFUTAJI NA UCHIMBAJI) WA MAFUTA NA GESI ASILIA NA KAMPUNI YA MAENDELEO YA MAFUTA NA GESI ASILIA

Mamlaka ya Udhibiti (Utafutaji na Uendelezaji) wa Mafuta na Gesi Asilia.

**7.-(1)** Kunaanzishwa Mamlaka itakayojulikana kama Mamlaka ya Udhibiti (Utafutaji na Uendelezaji) wa Mafuta na Gesi Asilia na ufupisho wake utasomeka ZPRA.

(2) Mamlaka itakuwa ni chombo kinachojitegemea, endelevu na chenye muhuri wake na kwa jina lake litaweza:

(a) kushtaki na kushtakiwa;

(b) kumiliki, kuhodhi, kununua au kuuza mali yoyote inayohamishika na isiyohamishika;

(c) kuingia katika mkataba wowote au shughuli ya kibiashara kwa mujibu wa Sheria;

(d) kukopa kiasi chochote cha fedha katika taasisi ya kifedha; na

(e) kufanya tendo lolote ambalo chombo chenye kujitegemea kinaweza kufanya kwa mujibu wa sheria.

Kazi na Wajibu wa Mamlaka.

**8.-(1)** Kazi za Mamlaka itakuwa ni kufuatilia na kudhibiti utafutaji, uendelezaji na uzalishaji wa mafuta na gesi asilia Zanzibar.

(2) Bila ya ukomo wa masharti ya jumla ya kifungu kidogo (1) cha kifungu hiki, Mamlaka:

(a) itafatilia na kudhibiti shughuli za mafuta na gesi asilia ikijumuisha makisio ya hifadhi na vipimo vya mafuta na gesi asilia yaliyozalishwa;

(b) itapitia na kuridhia shughuli ya utafiti iliyopendekezwa na kuwemo katika mpango kazi, mpango wa tathmini na makadirio ya uzalishaji uliowasilishwa na Kampuni;

(c) itapitia na kuidhinisha bajeti zilizo wasilishwa na Kampuni;

(d) itatathimini mipango ya maendeleo na kutoa mapendekezo kwa Waziri kwa ajili ya kuidhinisha, kurekebishwa au kukataliwa;

(e) itamshauri Waziri katika kutoa na kufuta leseni;

(f) itatathimini hatua za mwisho za uzalishaji, usitishaji, pamoja na ukomo wa shughuli za mafuta na gesi asilia;

(g) itaandaa ramani ya muongozo itakayoweza kupitiwa mara kwa mara inayoonesha maeneo yenye uwezekano wa utafutaji na uzalishaji wa mafuta na gesi asilia;

(h) itashiriki upimaji wa mafuta na gesi asilia na kuruhusu makisio na tathmini ya mrahaba na faida ya mafuta au gesi kwa maslahi ya nchi na itahusika kuidhinisha zoezi hilo;

(i) itahakiki gharama za mafuta au gesi za kampuni;

(j) itahakikisha kwamba kampuni zinafuata sheria, kanuni, taratibu na masharti ya mkataba;

(k) itafanya au itawezesha kufanyika utafiti wa awali na kutathmini maeneo muhimu ya mafuta na gesi asilia;

(l) itasimamia mikataba ya mafuta na gesi asilia;

(m) itahakikisha uvunaji wa hali ya juu wa raslimali za mafuta na gesi asilia;

(n) itaendeleza mipango mizuri inayotekelezeka kwa gharama nafuu;

(o) itahakikisha matumizi mazuri ya miundo mbinu iliyopo na iliyopangwa;

(p) itahakikisha uanzishwaji wa kituo kikuu cha mfumo wa taarifa kwa watu wanaohusika na shughuli za mafuta na gesi asilia, kusimamia taarifa za mafuta na gesi asilia na kutoa taarifa na machapisho ya kila siku kuhusu shughuli za mafuta na gesi asilia;

(q) itachukua hatua za ulazima kutekeleza matakwa ya leseni au kanuni zozote na kulinda afya na usalama wa wafanyakazi na jamii;

(r) itahakikisha na kuwezesha ushindani, upatikanaji na matumizi ya miundombinu kwa wengine;

(s) itafuatilia masharti ya waendeshaji na shughuli zao za kibiashara kwa kuhakikisha kwamba ushindani na haki inalindwa;

(t) itahakikisha washiriki wanafuata Sheria hii na kutoa adhabu kwa wanaopinga au wanaovunja kanuni, amri, taratibu au masharti ya mkataba; na

(u) itafanya mambo mengine yote ambayo ni muhimu, ya kuharakisha au ambayo ni muafaka ili kufikia malengo ya Sheria hii.

(3) Pamoja na kazi zilizoelezwa katika kifungu kidogo cha (1), Mamlaka itakuwa na majukumu yafuatayo:

(a) kumshauri Waziri katika kutoa, kuongeza muda, kusitisha na kufuta leseni ya utafutaji mafuta na gesi asilia, leseni ya uendelezaji na kibali cha uzalishaji;

(b) kutoa taarifa kwa Mamlaka husika kwa ajili ya ukusanyaji kodi na tozo zinazotokana na shughuli za mafuta na gesi asilia;

(c) kuishauri Serikali juu ya mipango endelevu, uendelezaji miundombinu, mipango ya hatua za mwisho na ukomo wa miundombinu iliyowasilishwa na Kampuni.

Miongozo ya Waziri.

**9.** Waziri anaweza kutoa miongozo kwa maandishi kwa Mamlaka inayohusiana na Sera ya Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar kwa kulinda maslahi ya jamii na kutekelezwa na Mamlaka na muongozo mwengine wowote chini ya Sheria hii.

Miongozo ya Mamlaka kwa Kampuni na Mkandarasi.

**10.-(1)** Mamlaka, kwa notisi ya maandishi itatoa miongozo kwa Kampuni au mkandarasi inayoendana na sheria inayotumika na uzoefu unaokubalika kuhusiana na shughuli za mafuta na gesi kwa kuhakikisha kwamba uzalishaji mzuri na sahihi wa mafuta na gesi asilia na kuhamasisha utunzwaji wa uzoefu huo katika sehemu zilizopatiwa leseni.

(2) Notisi iliyotolewa katika kifungu kidogo (1) cha kifungu hiki itaainisha vigezo na masharti, na muda ambao Kampuni au mkandarasi anatakiwa kuzingatia.

Utii wa Miongozo.

**11.-(1)** Endapo Kampuni au mkandarasi ameshindwa au amekataa kutii miongozo iliyotolewa na mamlaka chini ya Sheria hii, Mamlaka inaweza kufanya mambo yote au sehemu ya mambo hayo yaliyotakiwa kufanywa katika muongozo.

(2) Gharama zilizoingiwa chini ya kifungu kidogo cha (1), ni deni la Mamlaka na inaweza kudai katika mahakama yenye mamlaka bila ya kujali kama Kampuni na mkandarasi wametiwa hatiani chini ya Sheria hii.

Bodi ya Wakurugenzi.

**12.-(1)** Kutakuwa na Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ambayo itakuwa na mamlaka ya kusimamia mambo yote ya Bodi na itakuwa na wajumbe wasiozidi saba (7) wenye tabia nzuri, waadilifu na wenye uwezo katika fani husika.

(2) Bodi itakuwa na wajumbe wafuatao:

(a) Mwenyekiti atakaechaguliwa na Rais kwa mujibu wa Sheria hii;

(b) Mkurugenzi Mwendeshaji wa Mamlaka kutokana na nafasi yake;

(c) Afisa mwandamizi kutoka Wizara inayohusiana na Mazingira;

(d) Wakili wa Serikali kutoka Afisi ya Mwanasheria Mkuu atakaependekezwa na Mwanasheria Mkuu;

(e) Afisa mwandamizi mmoja kutoka Wizara inayohusiana na Mafuta na Gesi;

(f) Afisa mwandamizi mmoja kutoka Wizara ya Fedha;

(g) Afisa mwandamizi mmoja kutoka Wizara inayohusiana na Afya na Usalama kazini; na

(h) Mjumbe mmoja kutoka Sekta binafsi mwenye uzoefu wa utafutaji na uendelezaji wa mafuta na gesi asilia.

(3) Wajumbe waliotajwa katika aya (c), (d), (e), (f) na (g) watateuliwa na Waziri kwa kushauriana na Waziri wa Wizara husika na uteuzi huo kadri itakavyowezekana utazingatia jinsia.

(4) Uteuzi wa Katibu wa Bodi utafanywa kama ilivyoelekezwa katika Jadweli la Kwanza.

Kazi za Bodi.

**13.** Bodi itafanya kazi ifuatazo:

(a) kusimamia shughuli za mamlaka;

(b) kumshauri Waziri kuhusiana na Sera ya Mafuta na Gesi Asilia na masuala mikakati yanayohusiana nayo;

(c) kupitia na kuidhinisha mipango ya biashara na uendeshaji, bajeti, ripoti na ripoti ya utekelezaji ya mwaka ya Mamlaka;

(d) kutoa muongozo kwa Mkurugenzi mwendeshaji na wafanyakazi wa Mamlaka;

(e) kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma, itaanzisha na kuthibitisha kanuni na taratibu za uteuzi, upandishaji vyeo, kufuta kazi, kusimamia nidhamu, vigezo na masharti ya wafanyakazi wa Mamlaka;

(f) kuanzisha na kusimamia Kanuni za Wafanyakazi na Kanuni za Fedha za Mamlaka;

(g) kuhakikisha kwamba utawala bora, kanuni za maadili, uzoefu mzuri unakuwepo na kutekelezwa;

(h) kupendekeza muundo wa kitaasisi wa Mamlaka; na

(i) kufanya kazi nyengine yoyote iliyopewa na Sheria hii au ambayo ni muhimu katika kufikia malengo ya Sheria hii.

Uwezo wa Bodi.

**14.** Isipokuwa kwa Mkurugenzi Mwendeshaji, Bodi itakuwa ni mamlaka ya nidhamu kwa wafanyakazi wote wa Mamlaka, ukizingatia kwamba Bodi inaweza kupendekeza kwa Rais kupitia Waziri, hatua za kinidhamu zitakazochukuliwa dhidi ya Mkurugenzi Mwendeshaji itakapotokezea ukosefu wa nidhamu.

Sifa za Mwenyekiti na Wajumbe wa Bodi.

**15.-(1)** Mtu atakuwa na sifa za kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Bodi akiwa:

(a) Mzanzibari;

(b) Angalau Shahada ya kwanza ya Chuo Kikuu katika fani ya Uhandisi, Nishati, Sayansi ya Ardhi, Mchumi, Fedha au Sheria kutoka katika taasisi ya elimu inayokubalika; na

(c) Uzoefu usiopungua miaka kumi katika fani hiyo na utawala.

(2) Isipokuwa kwa Wajumbe wanaoingia kwa nafasi zao, wajumbe wengine wawe na fani moja kati ya zifuatazo:

(a) fani ya mafuta na gesi asilia;

(b) afya, mazingira na usalama kazini;

(c) utawala wa biashara au uongozi, uchumi, fedha au sheria; na

(d) uzoefu wa kazi katika fani husika kwa kipindi kisichopungua miaka saba.

Mienendo ya Bodi.

**16.** Masharti yanayohusiana na vikao, muda, akidi na mienendo mengine ya Bodi itakuwa kama itakavyoelezwa katika Jadweli la Kwanza la Sheria hii.

Uteuzi wa Mkurugenzi Mwendeshaji.

**17.-(1)** Kutakuwa na Mkurugenzi Mwendeshaji wa Mamlaka atakaeteuliwa na Rais kwa mujibu wa Sheria hii.

(2) Mtu hatoteuliwa kuwa Mkurugenzi Mwendeshaji isipokuwa awe:

(a) Mzanzibari;

(b) na angalau Shahada ya Kwanza ya Chuo Kikuu katika fani ya mafuta na gesi asilia katika Chuo kinachotambulika; na

(c) uzoefu wa kazi usiopungua miaka kumi katika fani husika.

(3) Mkurugenzi Mwendeshaji atateuliwa kushika nafasi kwa kipindi cha miaka mitano, iwapo utendaji wake ukiridhisha, atachaguliwa tena kwa kipindi cha miaka mitano.

Kazi za Mkurugenzi Mwendeshaji.

**18.-(1)** Mkurugenzi Mwendeshaji atakuwa ni afisa mtendaji mkuu wa Mamlaka na atawajibika kwa kazi za uendeshaji za kila siku na usimamizi wa Mamlaka.

(2) Bila ya kuathiri masharti ya jumla ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Mkurugenzi Mwendeshaji atakuwa na wajibu ufuatao:

(a) kuanzisha na kutekeleza sera na mipango ya mamlaka na kuripoti kwa Bodi;

(b) kusimamia matumizi ya fedha na mali za Mamlaka;

(c) kudhibiti na kusimamia wafanyakazi wa Mamlaka;

(d) kutayarisha mpango wa uendeshaji kwa ajili ya kuiongoza Mamlaka ili kufikia malengo na madhumuni yaliyoelezwa na Sheria hii;

(e) kushirikiana na wakala wengine wanaohusiana na sekta ya mafuta ndani na nje ya Zanzibar kuhusiana na masuala ya utafutaji na uendelezaji wa mafuta na gesi asilia;

(f) kupendekeza kwa Bodi juu ya masuala ya kiuchumi, ufanisi na gharama nafuu za uendeshaji za muundo wa Mamlaka;

(g) kuhakikisha kwamba malengo, shabaha viwango vya huduma za bodi zinafikiwa; na

(h) kufanya kazi nyengine yoyote ambayo ni muhimu kwa utekelezaji na kufikia lengo la Sheria hii.

(3) Mkurugenzi mwendeshaji katika utekelezaji wa kazi zake atawajibika kwa Bodi.

Idara na Vitengo vya Mamlaka.

**19.-(1)** Mamlaka inaweza katika kufikia malengo na utendaji bora wa kazi zake chini ya Sheria hii, na utekelezaji wa kazi zake, itaweza kuanzisha Idara na vitengo vitakavyoongozwa na wakuu na wafanyakazi wengine kama itakavyoamuliwa.

(2) Wakuu wa Idara au vitengo kadri itakavyokuwa, watateuliwa na Bodi kwa mujibu wa vigezo na masharti ya uwezo na kwa mujibu wa uwezo wa sheria nyengine yoyote inayohusiana na Utumishi wa Umma.

(3) Wakuu wa Idara katika kutekeleza kazi zao watawajibika kwa Bodi.

Wafanyakazi wa Mamlaka.

**20.** Wafanyakazi wa Mamlaka wataajiriwa na Bodi kwa mujibu wa vigezo na masharti yaliyomo katika kanuni za Utumishi za Mamlaka zilizoundwa kwa mujibu wa masharti ya Sheria yoyote inayohusiana na Utumishi wa Umma.

Kinga dhidi ya Wajumbe wa Bodi na Maafisa wa Mamlaka.

**21.** Mjumbe wa Bodi au afisa wa Mamlaka au mtu anaetekeleza maelekezo ya Bodi au afisa wa Mamlaka hatohusika yeye binafsi kwa kutenda au kuacha kutenda kwa nia njema katika utekelezaji wa kazi chini ya Sheria hii.

Wajibu wa kutokutoa taarifa.

**22.-(1)** Kwa mujibu wa Sheria hii, mtu ambae ni mjumbe wa Bodi au mfanyakazi wa Mamlaka hatotoa taarifa yoyote ambayo ameipata katika utendaji wa kazi yake.

(2) Mtu ambae amekoma kuwa Mjumbe wa Bodi au mfanyakazi wa Mamlaka hatotoa taarifa yoyote ya siri aliyoipata katika utendaji wa kazi yake.

(3) Mtu anaekiuka kifungu kidogo cha (1) au cha (2) amefanya kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua Shilingi Milioni Ishirini au kifungo kisichozidi miaka minne au adhabu zote mbili.

Fedha za Mamlaka.

**23.** Kutakuwa na fedha za Mamlaka zitakazojumuisha:

(a) fedha zitakazotengwa na Baraza la Wawakilishi kwa ajili ya Mamlaka;

(b) michango, ruzuku, wasia au mikopo iliyopatikana kihalali kutoka taasisi au jumuiya yoyote;

(c) mapato yanayotokana kwa kuuzwa kwa mali au vyanzo vyovyote vya mapato vilivyoainishwa na Mamlaka;

(d) asilimia yoyote ya mapato iliyokusanywa kutoka kwenye vyanzo vyengine;

(e) ada ya usimamizi kama zilivyoainishwa katika Kanuni;

(f) mapato mengine yoyote yanayopatikana kutokana na utendaji wa shughuli yoyote ya Mamlaka;

(g) fedha yoyote inayokusanywa kama adhabu inayolipwa kutokana makosa chini ya Sheria hii; na

(h) fedha nyengine yoyote iliyopatikana kisheria na Mamlaka.

Wajibu wa utendaji wa kusimamia misingi ya kifedha.

**24.** Mamlaka, katika kutekeleza kazi zake chini ya Sheria hii, itasimamia misingi ya kifedha.

Uwezo wa kufungua na kuendesha akauti za benki.

**25.-(1)** Kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Fedha:

(a) Mamlaka baada ya kuthibitishwa na Bodi itafungua na kusimamia akauti za Benki katika kutekeleza kazi za Mamlaka chini ya Sheria hii; na

(b) Mkurugenzi Mwendeshaji atahakikisha kwamba, fedha zote zinazopokelewa kwa niaba ya Mamlaka zinahifadhiwa benki kadri iwezekanavyo baada ya kupokelewa;

(2) Kwa mujibu wa miongozo ya Bodi, Mkurugenzi Mwendeshaji:

(a) ataidhinisha matumizi ya kila siku kwa kiwango kilichoamuliwa na Bodi; na

(b) atathibitisha mtaji ambao gharama zake hautozidi Shilingi Milioni Hamsini au kiwango ambacho Waziri anaweza kupanga mara kwa mara.

Uwezo wa kukopa.

**26.** Mamlaka inaweza kukopa fedha kutoka katika chanzo chochote kinachoona kitatimiza wajibu wake au kutekeleza kazi zake chini ya Sheria hii kwa mujibu wa Sheria ya Fedha za Umma.

Makadirio.

**27.-(1)** Mkurugenzi Mwendeshaji, ndani ya miezi mitatu kabla ya mwisho wa mwaka wa fedha, atawezesha kutayarishwa na kuwasilishwa katika Bodi kwa ajili ya kuthibitisha, makadirio ya mapato na matumizi ya Mamlaka.

(2) Bodi, ndani ya miezi miwili baada ya kupokea makadirio yaliyoainishwa katika kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki itawezesha kuwasilishwa kwa Waziri kwa ajili ya kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi kama yalivyoidhinishwa na Bodi.

Mwaka wa Fedha.

**28.** Mwaka wa fedha wa Mamlaka utakuwa ni sawa na mwaka wa fedha wa Serikali.

Hesabu.

**29.-(1)** Mkurugenzi Mwendeshaji, atawezesha kuwekwa vitabu vya hesabu na kumbukumbu za miamala ya kifedha ya Mamlaka kwa kuzingatia misingi ya hesabu inayokubalika.

(2) Kwa mujibu wa miongozo iliyotolewa na Bodi, Mkurugenzi Mwendeshaji atawezesha kutayarisha taarifa ya fedha ya mwaka inayoelezea misingi ya kifedha na ataainisha hatua za utekelezaji na sababu za utekelezaji huo.

(3) taarifa za hesabu zitajumuisha:

(a) mezania, mapato na matumizi ya hesabu, chanzo na maombi ya fedha ya Mamlaka; na

(b) taarifa nyengine zozote zinazohusiana na mambo ya fedha ya Mamlaka kama Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu au Mkaguzi aliyechaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu Hesabu atakavyohitaji kwa maandishi.

Ukaguzi.

**30.-(1)** Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu au Mkaguzi atakaeteuliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu kila mwaka wa fedha atakagua hesabu za Mamlaka kwa mujibu wa sheria inayohusiana na ukaguzi.

(2) Bodi itahakikisha kwamba miezi mitatu baada ya mwisho wa kila mwaka wa fedha, taarifa za hesabu zitawasilishwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu au Mkaguzi alieteuliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu kwa ajili ya ukaguzi.

Ripoti ya mwaka.

**31.-(1)** Bodi itawasilisha kwa Waziri kadri iwezekanavyo kwa kipindi kisichozidi miezi minne baada ya mwisho wa kila mwaka wa fedha taarifa kamili ya shughuli na uendeshaji wa Mamlaka kwa kipindi cha mwaka ambao ripoti hiyo inahusika ikijumuisha ukaguzi wa hesabu.

(2) Taarifa iliyoelezwa katika kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki itajumuisha:

(a) makadirio ya hifadhi ya mafuta na gesi asilia;

(b) kiwango cha mafuta na gesi asilia kilichozalishwa na kinachokadiriwa; na

(c) taarifa nyengine kama Bodi itakavyoona inafaa.

(3) Waziri ndani ya miezi miwili baada ya kupokea taarifa ya mwaka ataiwasilisha taarifa hiyo katika Baraza la Wawakilishi pamoja na taarifa nyengine ambazo ataona inafaa kwa ajili ya kujadiliwa.

Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asilia.

**32.-(1)** Kunaanzishwa Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar ambapo kifupisho chake kitakuwa ZPDC ambayo itashiriki katika shughuli za utafutaji na uendelezaji wa mafuta na gesi asilia kwa niaba ya Serikali.

(2) Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar itatekeleza shughuli za mafuta na gesi asilia kwa mujibu wa Sheria hii.

(3) Sheria hii itatumika kwa Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar sawa na Sheria hii itakavyotumika kwa Kampuni na mkandarasi mwengine yoyote.

(4) Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar itasajiliwa kama Kampuni chini ya Sheria za Zanzibar zenye ukomo wa hisa ambazo zote zitamilikiwa na Serikali kwa niaba ya Watu wa Zanzibar.

(5) Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar kwa niaba ya Serikali itakuwa kama ni chombo cha biashara na kulinda maslahi ya taifa katika shughuli za mafuta na gesi asilia.

## SEHEMU YA NNE
## SHUGHULI ZA UTAFUTAJI NA UENDELEZAJI WA MAFUTA NA GESI ASILIA

Mgao wa eneo la ardhi na vitalu.

**33.-(1)** Kwa madhumuni ya Sheria hii, eneo la ardhi litagawiwa katika mgao utakaojumuisha eneo la utafutaji, na kila eneo litajumuisha kama ilivyoelezwa katika Kanuni.

(2) Mamlaka itatayarisha ramani itakayopitiwa mara kwa mara, inayoonesha eneo lenye uwezekano wa utafutaji na uzalishaji wa mafuta na gesi asilia.

(3) Ramani iliyotayarishwa kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki, itawekwa na kupatikana kwa umma katika ofisi za Mamlaka na tovuti yake.

(4) Wakati wa uchapishaji wa ramani, kumbukumbu zozote zinazohusiana na kibali cha utafiti wa awali, leseni ya utafutaji na uendelezaji iliyotolewa na Sheria hii, katika vitalu vilivyoainishwa, vitachukuliwa kama kumbukumbu ya kitalu kilichoainishwa katika ramani ya kumbukumbu.

(5) Mamlaka inaweza kuthibitisha ramani iliyoandaliwa chini ya kifungu kidogo cha (2) kuwa nakala halisi na nakala hiyo inaweza kukubaliwa katika mwenendo wa kesi mbele ya Mahakama yoyote au Baraza la usuluhishi kama ushahidi wa yaliyomo katika ramani hiyo.

Ufunguzi, utambuzi mpya na ufungaji wa maeneo.

**34.-(1)** Uamuzi wa kufungua eneo kwa ajili ya shughuli za mafuta na gesi asilia utafanywa na Waziri baada ya kuidhinishwa na Baraza la Mapinduzi la Zanzibar.

(2) Kabla ya ufunguzi wa maeneo kwa ajili ya shughuli za mafuta na gesi asilia, Waziri akishirikiana na Mamlaka husika na kwa kushirikiana na Waziri anaehusika na mazingira, atafanya tathmini na maslahi tafauti katika maeneo yaliyomo katika ripoti ya tathmini.

(3) Ripoti ya tathmini itajumuisha:

(a) tathmini ya eneo lenye uwezekano mkubwa wa kuwepo mkusanyiko wa mafuta na gesi asilia; na

(b) tathmini ya mkakati wa athari za kijamii na mazingira kwa shughuli muhimu za mafuta na gesi asilia kuhusu:

(i) maendeleo ya taifa;

(ii) jamii;

(iii) mazingira na hatari ya uchafuzi;

(iv) biashara na utalii;

(v) kilimo na uvuvi;

(vi) uchumi na hathari za kijamii zinazotokana na shughuli za mafuta na gesi asilia; na

(vii) shughuli nyengine zozote zinazohusiana na sekta ya mafuta na gesi asilia.

(4) Ripoti ya tathmini itaainisha maeneo yaliyopendekezwa kuwa wazi kwa shughuli za mafuta na gesi asilia, uasilia na kiwango cha shughuli za mafuta na gesi asilia na athari za shughuli zake katika shughuli zinazohusiana na maslahi ya shughuli husika na jamii.

(5) Waziri atatangaza eneo litakalofunguliwa kwa shughuli za mafuta na gesi asilia katika gazeti linalosambazwa Zanzibar na katika tovuti ya Mamlaka.

(6) Mtu aliye na maslahi chini ya kifungu hiki anaweza kuwasilisha mitazamo na hoja kuhusiana na ripoti ya tathmini ndani ya kipindi cha siku thalathini kuazia tarehe iliyotangazwa.

(7) Waziri baada ya kuzingatia ripoti na maoni ya mtu mwenye maslahi atawasilisha ripoti inayoeleza maeneo ya kufunguliwa kwa shughuli za mafuta na gesi asilia, tathmini zilizofanywa za athari za kijamii na kimazingira na mapendekezo yake yatawasilishwa kwa Baraza la Mapinduzi Zanzibar kwa ajili ya kuidhinishwa.

(8) Waziri atatangaza maamuzi ya Baraza la Mapinduzi katika Gazeti Rasmi, tovuti ya Wizara na Mamlaka au njia nyengineo atakayoamua Waziri.

(9) Uamuzi wa kuitambua mipaka au kufunga eneo kwa shughuli za mafuta na gesi asilia utafanywa na Waziri kwa kushauriana na Mamlaka.

(10) Masharti yaliyomo katika kifungu kidogo cha (1) mpaka cha (9) yatatumika sawa sawa na maamuzi ya Waziri ya kuitambua upya na kufunga eneo la shughuli za mafuta na gesi asilia.

(11) Iwapo maamuzi ya kuitambua upya mipaka au kufunga maeneo yatakayokuwa na athari kwa eneo jengine ambalo inahusu leseni iliyopo wakati wa maamuzi, Kampuni itashauriwa na Mamlaka kabla ya maamuzi ya Waziri.

***(a) Kibali cha Utafiti wa Awali***

Ombi la kibali cha utafiti wa awali.

**35.(1)** Mtu aliyekusudia kufanya utafiti wa awali ataomba kwa Mamlaka kibali cha kufanya utafiti huo.

(2) Ombi la kibali cha utafiti wa awali litakuwa kama lilivyoelezwa na Kanuni na litaambatana na malipo yaliyotajwa.

(3) Kibali cha utafiti wa awali kitakuwa katika eneo lililoainishwa.

(4) Vibali vya utafiti wa awali havitakuwa vya kipekee na vinaweza kutumiwa na watu tafauti kwa shuguli tafauti za utafiti wa awali kwenye eneo moja.

(5) Kibali cha utafiti wa awali kitaeleza:

(a) tarehe ya kutolewa kibali;
(b) eneo ambalo vibali vinahusika;
(c) aina ya taarifa ambazo kibali hicho kinatolewa;
(d) mashariti ya kutolewa kibali;
(e) muda wa kutunza taarifa za siri zilizokusanywa;
(f) tarehe ya kumaliza muda;na
(g) taarifa nyengine zozote kama Mamlaka itakavyoona inafaa.

Muda wa kibali cha utafiti wa awali.

**36.** Kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii, kibali cha awali kitatolewa kwa kipindi cha miaka mitatu.

Kutoa kibali cha utafiti wa awali.

**37.-(1)** Mamlaka inaweza kwa mujibu wa maombi yaliyofanywa kutoa kibali cha utafiti wa awali ndani ya siku tisini baada ya kupokea maombi.

(2) Mamlaka itatangaza kwa lugha ya Kiswahili na kiingereza kupitia vyombo vya habari au magazeti yanayosambazwa Zanzibar kujuilisha umma juu ya dhamira ya shughuli za utafiti wa awali zilizopangwa.

Shughuli zilizoidhinishwa na kibali cha utafiti wa awali.

**38.-(1)** Kibali cha utafiti wa awali kitatumika kwa aina maalum ya utafiti na kitajumuisha uchimbaji mdogo kwa madhumuni ya mlinganisho wa taarifa.

(2) Iwapo vibali vya utafiti wa awali vitatolewa kwa watu wawili tofauti au zaidi katika eneo moja, shughuli za mwenye kibali mmoja zisiathiri shughuli za mwenye kibali mwengine.

(3) Iwapo shughuli za utafiti wa awali zinafanyika katika eneo ambalo limetangazwa kuwa ni la hifadhi ya makaazi ya wanyama, viumbe vya baharini, hifadhi ya misitu na hifadhi nyengine yoyote kwa madhumuni hayo,shughuli zote hizo zitahitaji kufuatwa kwa matakwa ya kisheria kuzingatia uzazi na mwenendo wa uhamiaji wa viumbe hivyo katika eneo husika.

Kuanza kwa shughuli za utafiti wa awali.

**39.** Mtu hatoaza utafiti wa awali isipokuwa mtu huyo amefuata matakwa ya kisheria yanayohusiana na uhifadhi wa mazingira, yaliyoelezwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Zanzibar na Sheria nyenginezo husika.

Kusitishwa kwa ruhusa ya utafiti wa awali.

**40.** Mamlaka itasitisha kibali cha utafiti wa awali iwapo:

(a) mwenye ruhusa ameshindwa kutekeleza masharti ya ruhusa au sheria yoyote nyengine; au

(b) kuna matukio ambayo ya majanga ya kimaumbile ambayo yanafanya isiwezekane mwenye kibali kutekeleza majukumu yake.

Kusamehe kwa kumaliza kazi.

**41.** Kibali cha utafiti wa awali kinaweza kumaliza muda kwa mwenye kibali kukamilisha utekelezaji wa majukumu ya kisheria na wajibu uliopo kwenye kibali.

Kumalizika kwa kibali.

**42.** Kibali cha utafiti wa awali kitaendelea kuwa halali mpaka:

(a) kumalizika muda kwa vigezo na masharti kama ilivyotolewa katika kibali;

(b) kufa kwa mwenye kibali;

(c) kufutwa kwa kibali; au

(d) kusamehe kama ilivyo katika kifungu cha 41 cha Sheria hii.

Umiliki wa taarifa.

**43.-(1)** Bila ya kujali haki za mwenye kibali Kampuni na Mamlaka, taarifa zote za mafuta na gesi asilia zilizopatikana chini ya Sheria hii itakuwa ni mali ya Serikali.

(2) Mamlaka inaweza, juu ya utaratibu uliowekwa, kumruhusu mwenye kibali na Kampuni kutumia taarifa zilizoelezwa katika kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki baada ya makubaliano.

(3) Endapo mwenye kibali au Kampuni atauza taarifa zilizotajwa katika kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki, mapato kutokana na mauzo hayo yatagaiwa kwa utaratibu ulioelezwa katika makubaliano yaliyoelezwa katika kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki.

Vikwazo vya rasilimali zisizokuwa mafuta na gesi asilia.

**44.** Kwa kuepusha shaka, haki za mmiliki wa leseni na mkandarasi zitakuwa kwenye mafuta na gesi asilia tu na hazitohusisha haki nyengine zozote za madini.

Haki za kipekee za Kampuni

**45.-(1)** Haki za uendeshaji wa shughuli za mafuta na gesi asilia zitatolewa kwa Kampuni.

(2) Kampuni itakuwa na haki ya kipekee katika haki zote zilizotolewa chini ya sehemu hii.

(3) Leseni iliyotolewa kwa Kampuni haitahaulishwa kwa mtu mwengine yeyote.

(4) Kampuni inaweza, baada ya kupata ridhaa kwa Waziri na ushauri kwa Mamlaka kuingia ubia na taasisi ya Kitanzania au Kigeni kupitia utaratibu wa wazi wa tenda.

(5) Leseni iliyotolewa chini ya kifungu kidogo cha (1) itaitaka Kampuni kuwa na hisa za ushiriki zisizozidi asilimia Ishirini na Tano (25).

(6) kampuni inayokusidia kufanya shughuli za mafuta na gesi asilia Zanzibar, nje ya kibali cha utafiti wa awali italazimka kufanya shughuli hizo kwa kushirikiana na Kampuni.

(7) Kwa madhumuni ya Sheria hii, kampuni itaiomba Kampuni kuomba leseni au kibali na itawasilisha kwa Kampuni taarifa zilizoelezwa katika leseni au kibali husika.

Watu wanaoweza kuingia ubia na Kampuni.

**46.** Mtu anafaa kuingia katika ubia na Kampuni iwapo:

(a) ni chombo kinachojitegemea kilichosajiliwa kwa mujibu wa Sheria za Makampuni, Zanzibar au sheria nyenginezo; na

(b) chombo hicho kina uwezo unaokubalika, utaalamu na uwezo wa kifedha.

Shughuli za pamoja.

**47.-(1)** Endapo waombaji wawili au zaidi kwa pamoja wamekusudia kuomba eneo la utafiti wa mafuta na gesi asilia lililotolewa, waombaji wataingia katika makubaliano kwa pamoja kwa shughuli za mafuta na gesi asilia ambayo yatawasilishwa kwa Waziri kama ni sharti la kuingia katika makubaliano.

(2) Waziri anaweza kutaka taarifa za ubia wa Makampuni husika kutoka kwa muombaji ikiwa ni sharti la kupata eneo la utafiti wa mafuta na gesi asilia.

Mikataba katika kutoa haki.

**48.-(1)** Waziri anaweza baada ya ushauri wa Mamlaka kuingia katika makubaliano na Kampuni na wabia wake kuhusiana na mambo yote au miongoni mwa mambo yafuatayo:

(a) kutoa leseni;

(b) Masharti ya kutoa au kuongeza muda wa leseni; au

(c) Mambo mengine muhimu au yanayohusiana na aya (a) na (b).

(2) Bila ya kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki Waziri hataingia katika makubaliano bila ya kupata ridhaa ya Baraza la Mapinduzi.

(3) Mamlaka itatayarisha na kuwasilisha kwa Waziri mikataba ya muundo ya ubia wa uzalishaji au mikataba ya muundo wa mafuta na gesi asilia utakaoridhiwa na Baraza la Mapinduzi.

(4) Mikataba ya Muundo ya Ubia wa Uzalishaji au mikataba ya aina ya muundo wa mafuta na gesi asilia yaliyoidhinishwa na Baraza la Mapinduzi yatakuwa muongozo katika majadiliano ya makubaliano chini ya kifungu hiki.

Utaratibu wa zabuni.

**49.-(1)** Mikataba ya mafuta na gesi asilia itaingiwa kwa uwazi na kwa namna ya ushindani baada ya kukamilisha utaratibu wa zabuni.

(2) Mamlaka itawezesha kuchapishwa katika gazeti linalosambazwa Zanzibar, mialiko ya zabuni au chini ya kifungu cha (3), nia ya kuanzisha majadiliano ya moja kwa moja.

(3) Endapo eneo lote au sehemu ya eneo hilo lilotangazwa zabuni kwa njia ya ushindani wa wazi na makubaliano hayakufikiwa katika utekelezaji, na kwa maslahi ya umma, Mamlaka inaweza baada ya idhini ya Waziri na ridhaa ya Baraza la Mapinduzi kuanzisha majadiliano ya moja kwa moja kwa kampuni yenye sifa na uwezo.

(4) Waziri anaweza, kupitia Kanuni, kueleza namna ya utaratibu wa kusimamia zabuni.

Uhifadhi wa vitalu.

**50.(1)** Waziri anaweza, kupitia notisi iliyochapishwa katika Gazeti Rasmi, kutangaza kitalu kuwa hifadhi kwa maslahi ya umma au kutolewa moja kwa moja kwa Kampuni.

(2) Kitalu kilichohifadhiwa chini ya kifungu kidogo cha (1), hakitotolewa leseni mpaka tangazo litakapofutwa.

(3) Waziri anaweza kupitia notisi iliyochapishwa katika Gazeti Rasmi, kubadilisha, kurekebisha au kufuta notisi iliyochapishwa chini ya kifungu hiki na kutoa sababu za kufanya hivyo.

(4) Endapo leseni iliyotolewa moja kwa moja kwa Kampuni chini ya kifungu kidogo cha (1), utaratibu wa zabuni hautotumika.

(5) Uwezo chini ya kifungu kidogo cha (1) au cha (3) unaweza kutumika na Waziri kwa maamuzi yake mwenyewe au kutokana na ushauri wa Mamlaka.

### *(b) Leseni ya Utafutaji Mafuta na Gesi Asilia*

Uwezo wa Waziri wa kutoa leseni ya utafutaji wa mafuta na gesi asilia.

**51.-(1)** Waziri atatoa kwaKampuni leseni ya utafutaji mafuta na gesi asilia katika kitalu husika baada ya kukamilishwa masharti yafuatayo:

(a) mapendekezo ya kazi ya muombaji na matumizi ya kiwango cha chini katika kitalu husika yatakayoainishwa katika maombi;

(b) taarifa za utaalam na sifa za sekta ya mafuta na gesi asilia za muombaji na wafanyakazi wake;

(c) taarifa za utaalam na rasilimali za sekta ya mafuta na gesi asilia zilizopo kwa muombaji;

(d) taarifa za aina za rasilimali fedha zilizopo kwa muombaji, zikijumuisha mtaji, miundombinu na dhamana;

(e) mapendekezo ya mpango wa ushiriki wa jamii unaohusika na mafunzo na ajira ya watu wa Zanzibar; na

(f) mambo mengine ambayo muombaji atapenda Waziri kuyazingatia.

(2) Masharti ya kifungu kidogo cha (1) yatatumika pia wakati wa utaratibu wa zabuni wa kufungua eneo la utafutaji mafuta na gesi asilia kwa namna itakavyoelezwa na Kanuni.

Kukataa kutoa leseni ya utafutaji wa mafuta na gesi asilia.

**52.-(1)** Endapo masharti yaliyoainishwa katika kifungu cha 51 cha Sheria hii, hayakutimizwa, Waziri anaweza kuiomba Kampuni kutimiza masharti kabla ya kutoa leseni ya utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia.

(2) Leseni ya utafutaji wa mafuta na gesi asilia haitotolewa katika kitalu husika, wakati wa maombi ya leseni yanapofanywa:

(a) kitalu hicho kimo ndani ya leseni iliyokwishatolewa; au

(b) kimehifadhiwa kupitia tangazo lililofanywa chini ya kifungu cha 50 cha Sheria hii.

Notisi ya maamuzi ya maombi ya leseni ya utafutaji wa mafuta na gesi.

**53.-(1)** Kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (2), Waziri, ndani ya siku sitini baada ya tarehe ya kupokea maombi atamjuilisha muombaji uamuzi wake wa kutoa au kutokubali kutoa leseni.

(2) Waziri atatoa sababu za kukataa au masharti ya kutoa leseni.

Mambo yatakayoainishwa katika leseni ya utafutaji wa mafuta na gesi.

**54.** Leseni ya utafutaji mafuta na gesi asilia:

(a) itataja tarehe ya iliyotolewa leseni;

(b) itaainisha kitalu au vitalu vilivyojumuishwa katika leseni katika eneo la utafutaji;

(c) itataja masharti ya kutolewa leseni hiyo;

(d) kuainisha mkandarasi na muendeshaji ikiwa ni ubia; na

(e) itajumuisha mambo mengine ambayo Waziri ataona yanafaa kwa madhumuni ya Sheria hii.

Haki na wajibu uliotolewa na leseni ya utafutaji mafuta na gesi asilia.

**55.-(1)** Kampuni itakuwa na haki za kipekee za kutafuta mafuta na gesi asilia katika eneo la utafutaji, kuendesha na kutekeleza kazi zinazohitajika.

(2) Kufuatia makubaliano yalioingiwa chini ya kifungu 45 cha Sheria hii, Kampuni inaweza kumpa mkandarasi haki za kipekee kwa ajili ya kufanya shughuli za utafutaji katika eneo la mkataba isipokuwa pale ambapo shughuli za pamoja zimeazishwa katika makubaliano, mkandarasi atakuwa na haki za kipekee za kufanya shughuli za kutafuta mafuta na gesi asilia katika eneo la mkataba kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii kwa niaba ya Kampuni.

(3) Kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki, wajibu wa Kampuni kwa mujibu wa Sheria hii utazingatiwa kuwa ni wajibu wa mkandarasi.

Uhalali wa masharti ya leseni ya utafutaji mafuta na gesi asilia.

**56.** Kwa mujibu wa sehemu hiina masharti yoyote yaliyoelezwa katika leseni ya utafutaji itakuwa halali:

(a) kwa kipindi kisichozidi miaka minne kuazia tarehe iliyotolewa leseni; na

(b) iwapo leseni imeongezwa muda, kwa kipindi kingine, kipindi hicho hakitozidi miaka mitatu kwa mara ya kwanza, na iwapo leseni imeongezwa muda kwa kipindi kingine, kipindi hicho hakitozidi miaka miwili kwa mara ya pili.

Ombi la kuongeza muda wa leseni ya utafutaji wa mafuta na gesi asilia.

**57.-(1)** Kampuni iliyopewa leseni ya utafutaji wa mafuta na gesi asilia inaweza kuomba kuongezwa muda ***wa*** ziada kwa kuzingatia kitalu chochote katika eneo la utafutaji wa mafuta na gesi asilia.

(2) Ombi chini ya kifungu hiki litakuwa:

(a) kwa mujibu wa masharti ya kifungu kidogo cha (4 ) cha kifungu hiki halitofanywa chini ya siku tisini kabla ya siku ambayo leseni itamaliza muda wake; na

(b) itaambatana na:

(i) taarifa za kazi zilizofanywa, kiasi cha fedha kilichotumika kwa ajili ya eneo la utafutaji kwa kipindi cha leseni na itajumuisha tarehe ya maombi au iwapo maombi ya kuongeza muda, yanafanywa kwa mara ya pili, taarifa za kazi zilizofanywa, kiasi cha fedha kilichotumika wakati muda ulipoongezwa kwa mara ya kwanza na itajumuisha tarehe ya maombi;

(ii) mapendekezo ya kutosha ya muombaji wa kazi na matumizi ya kiwango cha chini kwa kitalu kilichoainishwa katika maombi wakati wa kuongeza muda ulioombwa; na

(iii) mambo mengine ambayo muombaji anataka Waziri kuzingatia.

(3) Mkandarasi atawasilisha kwa Kampuni zilizoelezwa chini ya kifungu kidogo cha (2).

(4) Waziri anaweza kukubali maombi ya kuongeza muda wa leseni ya utafutaji wa mafuta na gesi asilia si zaidi ya siku tisini, na si kwa namna yoyote, baada ya kumaliza muda wa leseni.

(5) Matakwa yaliyoelezwa katika kifungu kidogo cha (2) (b) (ii) yaliyohusiana na mapendekezo yatachukuliwa kuwa yamekidhi haja iwapo mapendekezo hayo yameambatana na maombi yaliyoombwa kuhusu matakwa ya kazi na matumizi yaliyokuwemo katika makubaliano husika kuhusiana na utoaji leseni.

Maombi ya kuongeza muda kwa eneo lililopunguzwa.

**58.-(1)** Kwa mujibu wa makubaliano husika yanayohusiana na utoaji wa leseni:

(a) iwapo mkandarasi atachagua kuingia katika kuongeza muda kwa mara ya kwanza ndani ya muda wa utafutaji, eneo la mkataba kuanzia tarehe ya makubaliano ya shughuli za mafuta na gesi asilia litapunguzwa si chini ya asilimia hamsini;

(b) iwapo, baada ya kutolewa notisi ya maandishi kwa Waziri, mkandarasi atachagua kuingia katika kuongeza muda kwa mara ya pili ndani ya muda wa utafutaji, eneo la mkataba lililobakia litapunguwa si chini ya asilimia hamsini.

(2) Eneo lililorejeshwa litakuwa ni eneo kamili lenye kukidhi ukubwa na sura ambayo itaruhusu kutekelezwa kikamilifu kwa shughuli za mafuta na gesi asilia katika eneo lililorudishwa, isipokuwa vyenginevyo, kuamuliwa na Waziri baada ya kushauriana na Mamlaka.

(3) Serikali haitowajibika kwa gharama zozote zilizoingiwa au kulipwa na mkandarasi kwa ajili ya eneo la mikataba ambazo zimetokana na kurejeshwa kwa sehemu ya eneo la kitalu.

Kutolewa au kukataliwa kuongeza muda.

**59.-(1)** Waziri anaweza baada ya kushauriwa na Mamlaka, kuongeza muda wa leseni kufuatia maombi yaliyofanywa ya kuongeza muda wa leseni ya utafutaji mafuta na gesi asilia.

(2) Waziri anaweza, baada ya kushauriwa na Mamlaka, kukataa kuongeza muda wa leseni ya utafutaji wa mafuta na gesi asilia iwapo:

(a) Kampuni au mkandarasi amefanya makosa, isipokuwa Waziri amezingatia kwamba mazingira maalum yametokezea ambayo yamethibitisha kuongezwa kwa muda wa leseni bila kuzingatia kosa lililofanyika; au

(b) maombi yanayohusiana na kazi na matumizi wakati wa kuongeza muda ambayo yaliyoambatanishwa na maombi hayakujitosheleza.

(3) Waziri anaweza, baada ya kushauriwa na Mamlaka, kuruhusu kufanyika mabadiliko ya muda wa kazi kwa kuzingatia mazingira maalum yaliopo.

(4) Waziri hatokataa kuongeza muda wa leseni ya utafutaji wa mafuta na gesi asilia inapoombwa isipokuwa:

(a) muombaji amepatiwa notisi ya dhamira yake ambayo inaeleza mambo yafuatayo:

(i) taarifa za msingi wa kukataa kwake; na

(ii) tarehe ya mwisho ambayo muombaji anaweza kufanya marekebisho au mawasiliano yanayohusiana na sababu hizo;

(b) muombaji hakufanya marekebisho au mabadiliko yanayohitajika ya maombi yake au kufanya mawasisilisho ambayo, kwa maoni ya Waziri, yanaondoa uhalali wa kukataliwa maombi hayo.

(5) Waziri atamjulisha muombaji kwa maandishi dhamira yake ya kuongeza muda wa leseni ya utafutaji wa mafuta na gesi asilia.

(6) Taarifa ya kuongeza muda wa leseni ulioelezwa chini ya kifungu kidogo cha (5) itajumuisha masharit yoyote ya leseni yanayohitajika kutimizwakatika maombi ya kuongeza muda yakijumuisha marekebisho muda wa leseni.

(7) Baada ya kupokea notisi iliyoelezwa katika kifungu kidogo cha (5) kutoka kwa Waziri, muombaji anaweza, ndani ya siku sitini kueleza nia yake ya kukubali kuongezewa muda wa leseni ya utafutaji wa mafuta na gesi asilia na iwapo atashindwa kufanya hivyo muda utakuwa umemalizika.

(8) Endapo:

(a) maombi ya kuongeza muda wa leseni ya utafutaji wa mafuta na gesi asilia yamefanywa; na

(b) leseni imemaliza muda:

(i) kabla ya Waziri kutoa au kukataa kutoa muda wa kuongeza leseni; au

(ii) kabla ya maombi kumalizika muda ulioelezwa chini ya kifungu kidogo cha kifungu hiki,

leseni itaendelea kuwa halali mpaka pale ambapo Waziri ametoa au amekataa kuongeza muda wa leseni, au amekataa maombi, chochote kitakachotokeza mwazo, isipokuwa leseni imefutwa au maombi ya kuongeza muda yameondolewa.

Masharti ya kutoa leseni ya utafutaji wa mafuta na gesi asilia.

**60.-(1)** Kwa kuongezea masharti yaliyoelezwa katika leseni ya utafutaji wa mafuta na gesi asilia yaliyoelezwa chini ya kifungu cha 56(1) cha Sheria hii, au katika kipindi chochote cha kuongezwa muda wa leseni ulioainishwa chini ya kifungu cha 58 au 59 cha Sheria hii, mmiliki wa leseni:

(a) atawasilisha kwa Mamlaka si zaidi ya mwezi mmoja kabla ya kutimiza mwaka mmoja wa kupatiwa leseni, mpango uliojitosheleza kuhusiana na kazi na matumizi yatakayofanywa haraka iwezekanavyo na mpango huo uliowasilishwa utazingatiwa kuwa ni miongoni mwa matakwa ya leseni kuhusina na kazi na matumizi; na

(b) atakidhi matakwa ya leseni yake kuhusiana na kazi na matumizi ya eneo la utafutaji wa mafuta na gesi asilia kwa mujibu wa kifungu kidongo cha (3) cha kifungu hiki.

(2) Matakwa ya kifungu kidogo cha (1)(a) ya kifungu hiki, yatatakiwa yawe yanayojitosheleza na yatachukuliwa kwamba yametimia pale mpango ulowasilishwa utapokidhi matwaka kuhusiana na kazi na matumizi yaliyokuwemo katika makubaliano husika yanayohusiana na utowaji wa leseni.

(3) Waziri anaweza, kufuatia maombi yaliyofanywa na mmiliki wa leseni ya utafutaji wa mafuta na gesi asilia na baada ya kushauriwa na Mamlaka kuweka kikomo, kupunguza, kubadilisha au kusimamisha kwa muda wajibu wowote ulioelezwa katika kifungu kidogo cha (1)(b) cha kifungu hiki, ama kwa masharti au bila masharti.

Kutolewa taarifa kwa ugunduzi wa mafuta na gesi asilia.

**61.-(1)** Ikiwa mafuta na gesi asilia yatagunduliwa mkandarasi atalazimika kutoa taarifa kwa Kampuni kabla ya mtu mwengine yoyote, na Kampuni ndani ya masaa arobaini na nane baada ya taarifa:

(a) itawasilisha taarifa ya maandishi ya ugunduzi kwa Waziri na Mamlaka; na

(b) itawasilisha rasimu ya tangazo kwa Waziri.

(2) Mtu hatotoa tangazo lolote linalohusiana na ugunduzi wa mafuta na gesi asilia kabla ya tangazo la Waziri.

(3) Baada ya kupokea rasimu ya tangazo lililowasilishwa chini ya kifungu kidogo cha (1)(b) cha kifungu hiki, Waziri ataidhinisha tangazo lililopendekezwa ndani ya siku tano za kazi baada ya kushauriana na Mamlaka.

(4) Waziri, ndani ya siku mbili za kazi baada ya kushauriwa na Mamlaka atatangaza au atawezesha kutangazwa kwa tangazo.

(5) Ndani ya siku thelathini baada ya siku ya ugunduzi wa mafuta na gesi asilia, kuwasilisha kwa Mamlaka maelezo kwa maandishi ya ugunduzi na ndani ya siku tisini kuanzia tarehe ya ugunduzi kueleza kuwa ugunduzi unahitaji kufanyiwa tathmini au hauhitaji.

(6) Mtu atakaeshindwa au kukataa kutekeleza maelekezo yaliyotolewa chini ya kifungu kidogo cha (5) cha kifungu hiki, atakuwa amefanya kosa na ikithibitika atalazimika kulipa faini isiyopungua Dola za Kimarekani Ishirini na Tano Elfu au fedha za Kitanzania zinazolingana na hizo au kifungo cha muda wa miaka mitatu.

Tathmini na uchunguzi wa maeneo.

**62.-(1)** Mamlaka inaweza kuagiza kwa notisi ya maandishi kwa Kampuni yenye leseni ya utafutaji wa mafuta na gesi asilia, kufanya utafiti ndani ya kipindi kisichozidi miaka miwili kwa utafiti wa mafuta, na miaka mitatu kwa utafiti wa gesi asilia, kwa ajili ya kufanya tathmini ya upembuvu akinifu wa ujenzi, kuanzisha na kuendesha shughuli za ugunduzi wa mafuta na gesi asilia.

(2) Utafiti ulioainishwa katika kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, utajumuisha:

(a) mpango wa tathmini kwa madhumuni ya kuainisha mipaka ya hifadhi ya mafuta na gesi asilia ambayo ugunduzi huo unahusisha masharti yakiwemo kina, upana na wingi wa mafuta na gesi asilia ambayo yanaweza kuzalishwa kutoka katika hifadhi hiyo;

(b) upembuzi yakinifu wa kitaalamu na kiuchumi unaohusiana na taratibu za uzalishaji na usafirishaji wa mafuta na gesi asilia kutoka katika eneo hilo;

(c) utafiti wa maeneo yaliyopendekezwa kwa ajili ya miundombinu ambayo inahitajina na sekta ya mafuta iliyoainishwa katika kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki;

(d) tafiti za bandari au miundombinu ya uegeshaji wa meli, barabara, mabomba au miundombinu mengine ya usafirishaji;

(e) uchunguzi katika:

(i) miundombinu mizuri ya maji na mifumo ya mabomba kwa ajili ya shughuli za kazi;

(ii) eneo na usanifu unaohusiana na viwanja vya ndege na na miundombinu yake, iwapo inahitajika kwa kazi hizo; na

(iii) Uzalishaji na usambazaji wa umeme kama inavyohitajika kwa kazi hizo;

(f) uchunguzi katika uendelezaji wa makaazi ya nchi kavu, iwapo unahitajika, kwa ajili ya shughuli zilizoainishwa katika kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, ikijumuisha usanifu wa miundombinu, huduma za makaazi na huduma za kijamii na kitamaduni;

(g) uchunguzi wa kazi nyengine zozote, huduma zinazohitajika kwa kazi hiyo zinazohusiana na eneo husika;

(h) utafiti wa baadae kwa mahitaji ya wafanyakazi unaohusiana na kazi hiyo; na

(i) utafiti wa athari za kimazingira zinazoweza kujitokeza kuhusiana na sekta ya mafuta na gesi asilia.

(3) Kampuni ya utafutaji wa mafuta na gesi asilia itawasilisha kwa Mamlaka, ndani ya kipindi kilichoainishwa katika notisi iliyoelezwa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, ripoti, uchambuzi na taarifa zinazotokana na uchunguzi na tafiti zilizofanywa chini ya kifungu hiki kama Mamlaka, kwa notisi ya maandishi, kuitaka Kampuni kufanya hivyo.

(4) Endapo mmiliki wa leseni ameona kwamba ugunduzi hauna faida kibiashara kutokana na tathmini za kitaalamu na kiuchumi zilizofanywa katika eneo ambalo ugunduzi umefanyika, mmiliki wa leseni hiyo atarejesha eneo la ugunduzi.

(5) Endapo mmiliki wa leseni ameona kwamba ugunduzi una faida kutokana na tathmini ya utaalamu na kiuchumi zilizofanywa katika eneo ambalo ugunduzi umefanyika mmiliki wa leseni ataomba leseni ya uendelezaji ndani ya kipindi kilichoainishwa katika Kanuni.

### *(c) Leseni ya Uendelezaji*

Maombi ya leseni ya uendelezaji.

**63.-(1)** Maombi ya leseni ya uendelezaji yataambatana na Mpango wa Uendelezaji wa Eneo la Uendelezaji utakaojumuisha mambo yafuatayo:

(a) mapendekezo ya muombaji kwa ajili ya uendelezaji na uzalishaji wa mafuta na gesi asilia kutoka kwenye hifadhi, ikijumuisha mbinu za matumizi au uondoshaji wa gesi husika;

(b) mapendekezo yaliyojitosheleza yanayotokana na muombaji kwa ajili ya ujenzi, uanzishaji wa miundombinu na huduma zitokanazo na uvunaji, kuchuja mafuta ghafi, hifadhi na usafirishaji wa mafuta na gesi asilia;

(c) tathmini ya muombaji ikiwa uendelezaji na uzalishaji kutoka katika hifadhi ya mafuta na gesi asilia kwa madhumuni ya uendeshaji wa pamoja kwa shughuli za mafuta na gesi asilia kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii;

(d) tathmini ya muombaji kuhusiana na namna ya kuratibu shughuli za mafuta na gesi asilia na mtu mwengine, ikijumuisha matumizi ya pamoja ya miundombinu kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii na Sheria nyengine;

(e) fedha za kugharamia uendelezaji na uzalishaji wa mafuta na gesi asilia kutoka katika hifadhi yake;

(f) maombi ya muombaji yanayohusiana na upangaji, uchimbaji na ukamilishaji wa visima na miundombinu inayohitajika kwa ajili ya uzalishaji wa mafuta na gesi asilia ikijumuisha:

(i) makisio ya idadi, ukubwa na uwezo wa miundombinu ya uzalishaji;

(ii) visima vya uzalishaji;

(iii) taarifa za vifaa na miundombinu za uzalishaji;

(iv) taarifa za njia mbadala za usafirishaji wa mafuta na gesi asilia ikijumuisha mabomba;

(v) taarifa za miundombinu inayohitajika kuwekwa nchi kavu na baharini ikijumuisha aina na vigezo au ukubwa wa miundombinu hiyo; na

(vi) taarifa za vifaa nyengine za kitaalam vinavyohitajika kwaajili ya uendeshaji.

(g) makisio ya taarifa ya uzalishaji wa mafuta ghafi au gesi asilia kutoka katika hifadhi yake;

(h) makadirio ya gharama za mtaji na matumizi ya kawaida ya mradi;

(i) tafiti za upembuzi yakinifu za kiuchumi zilizofanywa na Kampuni kuhusiana na ugunduzi wa mafuta na gesi asilia kwa kuzingatia:

(i) mahala;

(ii) kina cha maji, kama kipo;

(iii) taarifa za hali ya hewa;

(iv) makadirio ya gharama za mtaji na matumizi ya kawaida ya upembuzi akinifu; na

(v) taarifa zozote nyengineyo zinazohusika na tathmini ya taarifa hizo;

(j) matumizi ya njia za usalama za uendelezaji na uzalishaji wa mafuta ya gesi asilia, ikijumuisha njia zitakazohusika na dharura;

(k) tathmini ya athari za kimazingira kuhusiana na uendelezaji, ikiwa ni pamoja na hatua muhimu zitakazochukuliwa kwa ajili ya kulinda mazingira;

(l) mapendekezo ya muombaji kwa ajili ya ajira na mafunzo ya kujenga uwezo wa watumishi wazalendo;

(m) mapendekezo ya muombaji yanayohusiana na manunuzi ya bidhaa na huduma za ndani;

(n) tathmini ya muda unaohitajika kila awamu ya mpango wa uendelezaji;

(o) athari ya matumizi ya ardhi;

(p) taarifa ya namna ya kuondoa miundombinu pale shughuli za mafuta na gesi asilia zitaposita;

(q) uendelezaji ukiwa umepangwa kwa awamu mbili au zaidi, taarifa hizo zitazingatia uendelezaji kamili kadri itakavyowezekana; na

(r) mambo mengine yoyote kama Waziri atakavyoona inafaa.

(2) Mkandarasi atawasilisha kwa Kampuni taarifa zote zinazohitajika chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki.

(3) Iwapo mkandarasi hakuitaka Kampuni kuomba leseni ya uendelezaji ndani ya muda ulioelezwa katika Kanuni, eneo lilolotangazwa kwa ajili ya uendelezwaji litarejeshwa Serikalini.

Ushughulikiaji wa ombi.

**64.-(1)** Kwa mujibu wa kifungu hiki, masharti ya kifungu cha 65 cha Sheria hii na makubaliano yoyote yanayohusiana na utoaji wa leseni:

(a) kwa ombi lililofanywa chini ya kifungu cha 57(1) cha Sheria hii, Waziri atatoa leseni ya uendelezaji chini ya masharti atakayoona yanafaa ili kuwezesha maombi ya leseni, yanayojumuisha marekebisho yake; au

(b) kwa ombi lililofanywa chini ya kifungu cha 57(3) cha Sheria hii, Waziri anaweza kutoa au kukataa kutoa leseni ya uendelezaji chini ya masharti hayo kwa kitalu chochote kilichopo ardhini ambacho Sheria hii inatumika.

(2) Kwa madhumuni ya kushughulikia maombi ya utoaji wa leseni na uendelezaji, Waziri anaweza kwa notisi ya maandishi kumtaka muombaji kuwasilisha, ndani ya muda ulioainishwa katika notisi, pendekezo, pamoja na namna ya kubadilisha pendekezo lolote lililowasilisha awali kama vile Waziri atakavyoainisha katika notisi, ikijumuisha jambo lolote linalohusiana na pendekezo lililoelezwa katika kifungu cha 57(2) cha Sheria hii.

(3) Waziri hatatoa leseni ya uendelezaji chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki bila ya kupata idhini ya Baraza la Mapinduzi Zanzibar.

Masharti ya utoaji wa leseni ya Uendelelzaji.

**65.-(1)** Leseni ya uendelezaji haitotolewa kwa muombaji isipokuwa:

(a) mapendekezo ya muombaji yanathibitisha ufanisi wa hali ya juu, manufaa na matumizi ya rasilimali husika kwa wakati;

(b) muombaji ana uwezo wa kutosha wa fedha, utaalamu, uwezo wa viwanda na uzoefu wa shughuli za uzalishaji;

(c) kama muombaji anaweza na kuwa tayari kufuata masharti ya leseni iliyotolewa;

(d) kama haki yoyote iliyotolewa, imesimamiwa na kutekelezwa au maandalizi yamefanywa kwa ajili hiyo au haki hiyo imeondolewa; na

(e) kama muombaji hajashindwa kutekeleza masharti.

(2) Waziri hatokataa ombi la leseni ya uendelezaji iliyoelezwa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki isipokuwa kama notisi imetolewa kwa muombaji juu ya nia ya kukataa kutoa leseni na kueleza sababu za kukataa huko.

Notisi ya uamuzi kuhusiana na ombi la leseni ya uendelezaji.

**66.-(1)** Waziri anaweza baada ya kupata ushauri kutoka kwa Mamlaka:

(a) kutoa notisi ya uamuzi wake kwa muombaji wa leseni ya uendelezaji; na

(b) iwapo Waziri anajiaandaa kutoa leseni, atatoa taarifa kamili za leseni inayopendekezwa.

(2) Iwapo Waziri anajiandaa kutoa leseni kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1) na muombaji ameshindwa kumtaarifu Waziri juu ya kukubali kwake kupokea leseni ya uendelezaji inayopendekezwa ndani ya siku sitini baada ya muombaji kupewa notisi, ombi lake litakuwa limemaliza muda.

Haki za mwenye leseni ya uendelezaji.

**67.** Leseni ya uendelezaji itaipa Kampuni haki ya kipekee ya kufanya ifuatavyo:

(a) shughuli za utafutaji wa mafuta na gesi alisia katika eneo la uendelezaji;

(b) shughuli za uendelezaji wa mafuta na gesi asilia katika eneo la uendelezaji;

(c) shughuli katika eneo la uendelezaji ambazo ni muhimu au zinahusiana katika jambo lolote lililoelezwa katika aya ya (a) au (b).

Muda wa leseni ya uendelezaji.

**68.** Leseni ya uendelezaji itakuwa halali:

(a) kwa kipindi kisichozidi miaka ishirini na tano kuanzia tarehe ya leseni iliyotolewa; na

(b) iwapo leseni itaongezwa chini ya kifungu cha 69 cha Sheria hii, kipindi hicho hakitozidi miaka kumi na tano kama Waziri atakavyoona inafaa kuzalisha kutoka eneo la uendelezaji kiwango cha juu cha mafuta na gesi asilia kwa kuzingatia uzoefu mzuri unaokubalika kwa mujibu wa shughuli za mafuta na gesi asilia.

Ombi la kuongeza muda wa leseni ya uendelezaji.

**69.-(1)** Ombi la kuongeza muda wa leseni ya uendelezaji litafanywa kwa Waziri.

(2) Ombi chini ya kifungu hiki:

(a) kwa masharti ya kifungu kidogo cha (3) cha kifungu hiki litafanywa si zaidi ya miezi kumi na mbili kabla ya siku ya leseni hiyo kumaliza muda wake;

(b) litaambatana na maelezo yafuatayo:

(i) kazi zilizofanywa, mafuta na gesi asilia iliyopatikana na gharama zilizotumika na kupatikana katika eneo la uendelezaji husika mpaka na inajumuisha tarehe isiyozidi mwenzi mmoja kuanzia tarehe ya ombi; na

(ii) mapendekezo ya muombaji kwa kazi na matumizi kuhusiana na eneo la uendelezaji katika kipindi cha kuongezewa muda kinachoombewa; na

(c) kuweka mambo mengine yoyote ambayo muombaji anamtaka Waziri kuyazingatia.

(3) Waziri anaweza kukubali ombi la kuongeza muda kwa mwenye leseni ya uendelezaji zaidi ya miezi kumi na mbili iliyoelezwa kabla na sio tarehe ya kumalizika muda wa leseni.

Kutoa au kukataa kuengeza muda wa leseni ya uendelezaji.

**70.-(1)** Waziri kufuatia ombi la kuongeza muda wa leseni ya uendelezaji na baada ya kushauriwa na mamlaka na kuidhinishwa na Baraza la Mapinduzi la Zanzibar ataongeza muda wa leseni ya uendelezaji.

(2) Waziri baada ya kuidhinishwa na Baraza la Mapinduzi Zanzibar atatoa notisi kwa muombaji ya maamuzi yake ya kuongeza muda wa leseni ya uendelezaji, na endapo amejiandaa kuongeza muda huo, atatoa maelezo ya mabadiliko yoyote ya masharti ya leseni ambayo yanatakiwa kufanywa na muombaji kwa kuongezewa muda huko, ikiwa ni pamoja na marekebisho yake ambayo yatahusika na uongezaji muda huo.

(3) Ikiwa muombaji ndani ya siku sitini baada ya kutoa notisi kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki ameshindwa kumjulisha Waziri juu ya nia yake ya kuongeza muda wa leseni kama ilivyopendekezwa, ombi lake litakuwa limekwisha muda.

(4) Iwapo:

(a) ombi la kuongeza muda wa leseni ya uendelezaji umefanywa; na

(b) leseni imekwisha muda:

(i) kabla ya Waziri kutoa au kukataa kuongeza muda wa leseni; au

(ii) kabla ya ombi kumaliza muda wake chini ya kifungu kidogo cha (3),

leseni hiyo itaendelea kutumika mpaka Waziri atakapotoa au kukataa kuongeza muda wa leseni, au ombi ambalo muda wake umemaliza, chochote kitakachotokezea mwanzo.

(5) Waziri hatoweza kukataa kuongeza muda wa leseni ya uendelezaji kutokana na ombi lililofanywa chini ya kifungu 69 isipokuwa:

(a) ametoa notisi kwa muombaji kwa adhma yake ya kufanya hivyo:

(i) kwa kutoa notisi ya maelezo juu ya sababu ya kukataa kwake;na

(ii) kueleza tarehe ambayo kuwa muombaji anaweza kuchukua hatua muafaka au kufanya mawasilisho yanayohusiana na sababu hii;

(b) ikiwa muombaji hakutekeleza hayo, kabla ya tarehe iliyotajwa, kurekebisha kosa, au kutokana na notisi iliyotolewa na Waziri, kufanya mawasilisho ambayo kwa maoni ya Waziri kuondosha sababu za kukataa kwake.

Kibali cha uzalishaji.

**71.-(1)** Baada ya kushauriwa na Mamlaka, Waziri:

(a) kabla au baada ya kutoa leseni ya uendelezaji, atathibitisha mpango wa uzalishaji uliokuwemo katika mpango wa uendelezaji na kutoa kibali cha uzalishaji wa mwaka kwa Kampuni;

(b) kufuatia maombi yaliyofanywa na Kampuni, kuthibitisha katika muda maalum, kiwango cha mafuta na gesi asilia ambacho kinaweza kuzalishwa au kuingizwa katika kisima cha mafuta kwa muda wote;

(c) anaweza kuelezea kwamba uzalishaji uongezwe au upunguzwe kutokana na mpango wa uzalishaji uliothibitishwa na anaweza kugawa kilichoongezeka au kilichopungua kwa usawa baina ya hifadhi husika na kutoa mazingatio maalum kwa mikataba ya muda mrefu ya usambazaji wa mafuta na gesi asilia;

(d) anaweza kufuatia maombi yaliyofanywa na Kampuni kuthibitisha majaribio ya uzalishaji wa hifadhi ya mafuta na gesi asilia, muda kiwango na masharti mengine ya majaribio ya uzalishaji; na

(e) ataitaka Kampuni kutoa ripoti ya kazi inayohusiana ikijumuisha mpango mbadala kwa uvunaji wa ufanisi wa mafuta na gesi asilia.

(2) Ombi lilofanywa chini ya kifungu kidogo cha (1) (b) litawasilishwa katika fomu kulingana na muda na maudhui yaliyoelezwa katika Kanuni.

Uzalishaji wa pamoja.

**72.-(1)** Waziri anaweza kuelekeza kwamba, iwapo mkusanyiko wa mafuta na gesi asilia utapatikana katika eneo moja au zaidi la nje ya eneo la mkataba, au mikusanyiko hiyo itapatikana katika maeneo ya mikataba tofauti yataendelezwa na kuzalishwa kwa namna nzuri itakayohakikisha ufanisi mzuri wa shughuli za mafuta na gesi asilia.

(2) Kufuatia miongozo iliyotolewa na Waziri chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, wakandarasi husika watafanya makubaliano ya uzalishaji wa pamoja kwa uendelezaji na uzalishaji wa mkusanyiko au mikusanyiko ya ardhini ya mafuta na gesi asilia kama ni uendelezaji mmoja chini ya muendelezaji mmoja.

(3) Makubaliano ya uzalishaji wa pamoja yatawasilishwa kwa Waziri kwa kuidhinishwa.

(4) Iwapo wakandarasi wameshindwa kufikia makubaliano Waziri anaweza kuwaelekeza wakandarasi hao kuingia katika makubaliano ya pamoja chini ya masharti yatakayowekwa na Waziri.

(5) Iwapo mkusanyiko wa ardhini wa mafuta na gesi asilia umeendelea nje ya mamlaka ya Zanzibar Serikali itahitaji kufikia makubaliano na hiyo nchi nyengine kwa mtazamo wa kuhakikisha mgao sahihi wa mkusanyiko wa hifadhi wa mafuta na gesi asilia na katika uratibu mzuri wa shughuli za mafuta na gesi asilia.

Masharti ya kusimamia haki ya leseni.

**73.-(1)** Mkandarasi hatosimamia haki yoyote ya leseni au Sheria hii:

(a) bila ya kupata ridhaa ya maandishi kutoka kwa Waziri inayohusiana na :

(i) ardhi iliyokusudiwa au iliyotengwa kwa ajili ya matumizi ya jamii isipokuwa kutumika kwa shughuli za madini;

(ii) ardhi iliyokusudiwa kama ni sehemu ya makaburi;

(iii) ardhi iliopo katika eneo au ndani ya mita mia moja ya jengo, hifadhi ya mafuta na gesi asilia, au bwawa linalomilikiwa na Serikali;

(iv) ardhi ambayo ni sehemu iliyotolewa leseni au viwanja vya ndege vya serikali au viwanja wa serikali au ambayo ipo ndani ya mita elfu moja ya mipaka ya maeneo hayo;

(v) ardhi iliopo kwa ajili ya uwekaji miundombinu au ardhi iliyopo ndani ya mita mia moja ya mipaka ya maeneo hayo;

(vi) eneo lililotengwa au eneo lililohifadhiwa, na kutangazwa kwa mujibu wa sheria;

(b) kutokana na ardhi maalum iliyotengwa, kuhifadhiwa au , kulindwa kwa mujibu wa sheria inayotumika Zanzibar;

(c) kutokana na ardhi yoyote iliopo ndani ya jiji, manispaa, mji, vijiji au sehemu zilizotengwa kwa ajili ya biashara, isipokuwa kwa ridhaa ya maandishi ya Kampuni yenye haki ya matumizi ya ardhi na Waziri husika au Mamlaka husika;

(d) kutokana na mtaa, barabara, au barabara kuu, na ndani ya mita mia moja ya daraja, kivuko cha umma, mitaro au kalvati katika mtaa, au barabara au barabara kuu, bomba au njia za umeme, isipokuwa kwa ridhaa ya Waziri husika.

(2) Mgogoro wowote ama kutumika au kutokutumika kwa kifungu kidogo cha (1)(b) kinachohusiana na ardhi yoyote, utashughulikiwa kwa mujibu wa Sheria husika.

(3) Ridhaa ya Waziri au Waziri yeyote husika chini ya kifungu hiki, itatolewa bila ya masharti au kwa masharti yaliyoainishwa katika hati ya ridhaa.

(4) Kwa madhumuni ya kifungu hiki, "Waziri husika" maana yake ni Waziri mwenye jukumu wa jambo hilo.

Kusalimisha leseni.

**74.-(1)** Iwapo mkandarasi anataka kusalimisha vitalu vyote au sehemu ya vitalu hivyo kwa mujibu wa leseni ataitaka Kampuni kuomba kwa Waziri hati ya kusalimisha kuhusiana na kitalu si zaidi ya siku tisini kabla ya tarehe ya kutaka kusalimisha.

(2) Ombi chini ya kifungu kidogo cha (1):

(a) litaeleza tarehe ambayo muombaji anataka usalimishaji uanze kufanya kazi;

(b) ikitokezea vitalu kwa mujibu wa leseni kutakiwa kusalimishwa, litaainisha kitalu kile tu kinachokusudiwa kusalimishwa;

(c) litatoa maelezo ya utafutaji au uendelezaji wa utekelezaji wa shughuli itakayofanyika kuanzia tarehe iliyotolewa leseni au muda wa mwisho ulioongezwa, vyovyote iwavyo, inayohusiana na leseni inayokusudiwa kuwasilishwa; na

(d) liambatane na kumbukumbu na taarifa zinazohusiana na uendeshaji huo kama Waziri atakavyohitaji.

(3) Kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (4) na (5) cha kifungu hiki, endapo ombi limefanywa chini ya kifungu kidogo cha (1), Waziri atatoa hati ya kusalimisha kitalu ama bila ya masharti au kwa masharti yatakayoainishwa katika hati hiyo kuhusiana na vitalu vinavyohusika na ombi hilo.

(4) Waziri anaweza, kabla ya kutoa hati ya kusalimisha kitalu chini ya kifungu kidogo cha (3), kuomba ushauri wa Mamlaka.

(5) Waziri hatatoa hati ya kusalimisha kitalu:

(a) kwa muombaji mwenye makosa;

(b) kwa muombaji ambae ameshindwa kutekeleza matakwa ya Waziri kwa mujibu wa kifungu kidogo (2)(d);

(c) iwapo ukomo wa shughuli za mafuta na gesi asilia kwa mujibu wa Sheria hii, haukukamilika;

(d) iwapo Waziri hakuridhika kwamba muombaji ameacha vitalu kuvisalimisha kuhusiana na utafutaji au uendelezaji wa shughuli za mafuta na gesi asilia umefanyika kwa masharti ambayo ni salama na yanaendana na uzoefu wa kimataifa unaokubalika wa sekta ya mafuta na gesi asilia.

Athari za hati ya kusalimisha.

**75.-(1)** Endapo hati ya kusalimisha imetolewa, Waziri:

(a) ikiwa si vitalu vyote kwa mujibu wa leseni ya utafutaji wa mafuta na gesi asilia au leseni ya uendelezaji kusalimishwa, atarekebisha leseni ipasavyo;

(b) kwa hali nyengine yoyote ile, atafuta leseni.

(2) Bila ya kuathiri kifungu kidogo cha (1), endapo Waziri atarekebisha au kufuta leseni kama ni tokeo la utoaji wa hati ya kusalimisha, Waziri atatoa taarifa ya maandishi kwa muombaji juu ya kuhusiana na marekebisho au kufuta kwa leseni.

(3) Kitalu kinachohusiana na hati ya kusalimisha imetolewa, kitachukuliwa kuwa kimesalimishwa kuanzia tarehe ya notisi ya kusalimisha hati iliyotolewa kwa muombaji kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1).

(4) Usalimishaji wa kitalu hautoathiri haki yoyote inayositahiki au jukumu liliopo kabla ya tarehe ambayo usalimishaji umeanza kuhusiana na kitalu hicho.

Usitishaji au ufutaji leseni.

**76.-(1)** Endapo mkandarasi ameshindwa, Waziri, kwa kushauriana na Mamlaka na notisi ya maandishi iliyotolewa kwa Kampuni au mkandarasi anaweza kusitisha au kufuta leseni.

(2) Waziri hatositisha au kufuta leseni kwa sababu ya kushindwa isipokuwa:

(a) notisi iliyoainishwa katika kifungu kidogo cha (1) imetolewa ndani ya kipindi kisichopungua siku thelathini;

(b) tarehe iliyoainishwa imetajwa ambayo mkandarasi na Kampuni wanaweza kwa maandishi kuwasilisha jambo lolote ambalo wamekusudia Waziri azingatie; na

(c) Waziri awe amezingatia:

(i) hatua yoyote iliyochukuliwa na mkandarasi na Kampuni kuondosha sababu au kuepusha kutokezea sababu zilizo kuwa sawa; na

(ii) jambo lolote lililowasilishwa kwake na mkandarasi na Kampuni kwa mujibu wa aya (b).

(3) Waziri hatositisha au kufuta leseni kutokana na sababu za kushindwa kulipa fedha zozote zinazopaswa kulipwa chini ya Sheria hii iwapo mkandarasi, kabla ya tarehe iliyoainishwa katika notisi iliyoelezwa katika kifungu kidogo cha (2), kulipa kiwango cha fedha kinachokusudiwa pamoja na malipo ya riba.

(4) Waziri anaweza, baada ya kushauriana na Mamlaka na kwa notisi ya maandishi aliopatiwa mkandarasi na Kampuni kufuta leseni iwapo:

(a) mkandarasi ametangazwa kufilisika au ameingia kwenye mikataba mengine yoyote au kaingia kwenye mfumo wa wadai wake au kutumia fursa ya sheria nyengine yoyote kwa maslahi ya wadaiwa; au

(b) amri iliyotolewa au azimio lilopitishwa la kumaliza mahusiano na mkandarasi, isipokuwa kumalizika huko ni kwa madhumuni ya kuunganisha na Waziri awe ameridhia kuunganishwa huko; au

(c) kwa madhumuni ya kuanzisha upya na Waziri ametoa notisi ya kuanzisha upya huko.

(5) Endapo kuna watu wawili au zaidi wanamaslahi kuhusiana na leseni hiyo Waziri, chini ya kifungu kidogo cha (4) hatositisha kutoa leseni kuhusiana na mtu mmoja au zaidi wenye maslahi na leseni hii, endapo kuna mtu mwengine mwenye maslahi ya leseni hiyo na akamtosheleza Waziri kwamba huyo mtu ana nia na uwezo wa kutekeleza wajibu na masharti ya Kampuni.

(6) Kuhusiana na ufutaji wa leseni, haki za mkandarasi na Kampuni zitasita, lakini ufutaji huo hautoathiri dhima yoyote iliopo kabla ya kufuta leseni.

### *(d) Masharti ya jumla*

Rajisi ya mafuta na gesi asilia.

**77.-(1)** Mamlaka itaanzisha na kutunza rajisi ya mikataba ya mafuta na gesi asilia, leseni na ruhusa na mabadiliko yoyote ya kimaslahi katika mikataba iliopo ya mafuta na gesi asilia, leseni au mikataba midogo.

(2) Rajisi litakuwa wazi kwa umma, isipokuwa kama imeelezwa vyenginevyo na Sheria.

(3) Mikataba ya mafuta na gesi asilia na leseni yatatolewa katika karatasi tafauti za rajisi.

(4) Mamlaka itaweka jarida la nyaraka zilizosajiliwa.

Maslahi katika leseni kuwekwa katika maandishi.

**78.-(1)** Maslahi ya kisheria au usawa, yanayoathiri leseni hayataweza kuwekwa, kuhaulishwa, kugaiwa, kuathiriwa au kushughulikiwa kwa njia yoyote ya moja kwa moja au isiyokuwa moja kwa moja isipokuwa kwa hati ya maandishi.

(2) Kuwekwa maslahi ya kisheria au usawa katika, au kuathiri leseni, hakutoathiri dhima ya mkandarasi na ya Kampuni kwa ukiukwaji wowote wa masharti ya leseni au sharti lolote la Sheria hii.

Uhaulishaji wa maslahi ya leseni kuthibitishwa na Waziri.

**79.-(1)** Isipokuwa Waziri ameidhinisha hati ambayo inahusu maslahi ya kisheria au usawa, au kuathiri leseni iliyowekwa, kugaiwa, kuathiriwa au kushughulikiwa kwa njia yoyote ya moja kwa moja au vyenginevyo, uhaulishaji au hati kama inavyotumika, haitokuwa na athari.

(2) Ombi la kuidhinisha uhaulishaji wa hati litafanywa kwa Waziri na litaambatana na:

(a) uthibitisho wa kwamba anayehaulishiwa ana uwezo wa kutekeleza majukumu ya muhaulishaji;

(b) hati ya usajili wa Kampuni au hati ya kutimiza masharti ya usajili wa Kampuni kwa anayehaulishiwa;

(c) uhaulishaji wa makubaliano baina ya anayehaulishiwa na muhaulishaji;

(d) hati ya kulipa kodi kutoka katika mamlaka ya ukusanyaji kodi;

(e) kiapo cha uadilifu cha anayehaulishiwa;

(f) maelezo ya kitaalam na sifa za kisekta za mafuta na gesi asilia za anayehaulishiwa na waajiriwa wake;

(g) maelezo ya aina za rasilimali fedha zilizopo kwa anayehaulishiwa ikiwa ni pamoja mtaji, huduma za mikopo na dhamana iliyopo;

(h) maelezo ya kitaalam na maelezo ya kisekta ya mafuta na gesi asilia ziliopo kwa muombaji;

(i) mapendekezo yanayohusiana na mafunzo na uajiri wa wazalendo; na

(j) jambo jengine lolote ambalo Waziri ataona linafaa.

(3) Kampuni itakuwa na haki ya mwanzo ya kumkataa mwakilishi wa mkandarasi kupatiwa maslahi shirikishi kwa asiyehusika.

(4) Kwa mujibu wa masharti ya kifungu kidogo cha (5) na (6), juu ya ombi lililofanywa chini ya kifungu kidogo cha (2), Waziri anaweza kutoa au kukataa kutoa idhini chini ya sharti lolote kama atakavyoona inafaa kuweka.

(5) Waziri kwa kushauriana na Mamlaka anaweza kuidhinisha kwa uhaulishaji wa maslahi katika leseni iwapo anayehaulishiwa si mtu mwenye sifa ya kushikilia maslahi katika leseni chini ya sharti lolote la Sheria hii au Sheria nyengine yoyote.

(6) Mhaulishaji wa maslahi ya leseni atahakikisha uendelezaji wa shughuli ya mafuta na gesi asilia chini ya leseni hiyo mpaka pale ambapo shughuli hizo zitachukuliwa na anayehaulishiwa.

(7) Waziri atatangaza bila ya kuchelewa uthibitisho wa kutoa kazi au mabadiliko ya umiliki angalau katika gazeti moja linalosambazwa Zanzibar.

(8) Kwa madhumuni ya kifungu kidogo cha (2)(a) "uhaulishaji wa maslahi katika leseni" inajumuisha uhaulishaji wa maslahi ya leseni kwa mujibu wa Sheria.

Waziri anaweza kutoa maelezo.

**80.** Waziri anaweza kumtaka mtu yeyote anaefanya maombi kuwasilisha kwa Mamlaka maelezo ambayo yanamuwezesha kumaliza ombi na muombaji atatii matakwa hayo.

Taarifa, maelezo na ripoti.

**81.-(1)** Bila ya kuathiri masharti ya kifungu cha 43 cha Sheria hii, Kampuni na mkandarasi watatoa kwa Mamlaka nakala za taarifa, maelezo na ripoti zilizopatikana chini ya Sheria hii bila ya malipo.

(2) Mamlaka inaweza kuruhusu Kampuni, Mkandarasi na Mkandarasi mdogo kuuza haki ya matumizi ya taarifa kwa masharti watakayokubaliana.

(3) Kampuni au mkandarasi hatosafirisha nje sampuli za vipande vya mwamba, sampuli ya vipande vidogo vidogo vya mwamba, sampuli za mawe magumu, sampuli za maji maji au taarifa nyengine zozote zilizokusanywa bila ya idhini ya maandishi ya Mamlaka.

(4) Mamlaka itaanzisha kituo cha taarifa za rasilimali ya mafuta na gesi asilia kwa ajili ya kuhifadhi taarifa zilizopatikana chini ya Sheria hii.

(5) Kampuni na mmiliki wa kibali watawasilisha kwa Mamlaka ramani sahihi ya kimiamba na mipango, kumbukumbu za sayansi ya miamba na ufafanuzi unaohusiana na eneo la leseni.

(6) Mkandarasi na Kampuni watawasilisha kwa Mamlaka kwa namna kama itakavyohitaji:

(a) kipindi cha nusu mwaka kinachoaazia miezi sita baada ya kutoa leseni:

(i) muhtasari wa taarifa za miamba, kemikali za miamba na sayansi ya miamba juu ya kazi itakayofanywa;

(ii) muhtasari wa shughuli za uchimbaji wa mafuta na gesi asilia na matokeo yanayopatikana;

(iii) nakala za ramani, kukumbuku au taarifa nyenginezo za miamba, kemikali za miamba na sayansi ya miamba zilizotaarishwa kwa ajili ya Kampuni kuhusiana na kipindi husika;

(b) ndani ya miezi sita baada ya mwisho wa kila mwaka wa muda wa leseni:

(i) kumbukumbu zinazoelezea matokea ya shughuli za mafuta na gesi asilia zilizofanywa na Kampuni katika mwaka ambao leseni inahusika;

(ii) makadirio, yakiwepo, yanayohusiana na upatikanaji wa mafuta na gesi asilia ulio katika mfumo wa mafuta ghafi na gesi asilia mwisho wa mwaka ambao leseni inahusika;

(c) muhtasari wa taarifa ya visima vilivyochimbwa ikijumuisha lithological groups, aina ya mipaka na maeneo ya haidrokaboni, ndani ya miezi mitatu baada ya kukamilisha uchimbaji, au upande wa taarifa ambazo hazikupatikana katika kipindi hicho, ndani ya siku thelathini baada ya kuwasilisha muhtasari huo; na

(d) maelezo mengine yoyote, taarifa na ripoti kama zitakavyohitajika.

(7) Mkandarasi na Kampuni wataweka wazi kwa mamlaka teknolojia ambayo ni muhimu kwa ajili ya tathmini na ufahamu wa taarifa zozote, taarifa iliyofanyiwa kazi au iliyofafanuliwa, iliyotolewa kutoka katika Kampuni na mmiliki wa kibali waliyofanya kazi katika maeneo ya leseni.

Utunzaji wa kumbukumbu.

**82.** Mkandarasi na Kampuni watamjulisha na kuwasilisha kwa Mamlaka na kuweka kumbukumbu sahihi na kamilifu zenye taarifa za:

(a) shughuli za uchimbaji, kuziba au kuachana na visima;

(b) tabaka na ardhi ya chini ambayo visima vimechimbwa;

(c) bomba linalotumika kuingizwa katika visima na marekebisho yoyote yanayohusiana na bomba hilo;

(d) mafuta yoyote na gesi asilia, maji na madini au vitu vya hatari vilivyomo au ugunduzi wowote wa maana wa madini atoe taarifa;

(e) maeneo ambayo taarifa za miamba, kemikali za miamba na sayansi ya miamba katika kazi inayofanywa;

(f) ubora wa mafuta ghafi wowote na gesi asilia ghafi iliyopatikana;

(g) kima cha:

(i) mafuta ghafi;

(ii) gesi asilia; na

(iii) madini ya kibiriti upele, katika hali yoyote, au madini mengine yoyote au gesi asilia, maji maji au ugumu uliotolewa kwa njia ya mauzo au vyenginevyo, mazingatio yaliyofanyika, wingi wa kilichotolewa na jina la mtu aliepewa kiwango hicho;

(h) wingi wa mafuta na gesi asilia kilichoingizwa kwa madhumuni ya upatikanaji wa mafuta na gesi asilia au kutolewa;

(i) kima cha mafuta na gesi asilia kilichotumika wakati wa shughuli za mafuta na gesi asilia zaidi ya kima kilichoelezwa katika aya ya (h);

(j) mafuta na gesi asilia yaliyopelekwa katika hifadhi ya eneo la uzalishaji na yaliopelekwa katika viwanda vya kusarifu;

(k) wingi wa mafuta na gesi asilia kilichosafishwa Zanzibar na Kampuni au kwa niaba ya mkandarasi kwa ajili ya kuondosha maji maji na mafuta na gesi asilia na wingi wa gesi au ugumu uliopatikana kutoka kima hicho; na

(l) wingi wa gesi asilia uliochomwa au kutolewa.

Wajibu wa kusitisha leseni na kibali cha awali.

**83.** Endapo leseni au kibali cha awali kimesitishwa, kufutwa, au kumaliza muda, mtu ambaye alikuwa ni Kampuni au mmiliki wa kibali mara kabla ya kusitishwa, kufutwa au kumaliza muda wa leseni au kibali cha awali atawasilisha kwa Mamlaka katika mfumo unaokubalika kwa Mamlaka muundo unaokubalika na Mamlaka:

(a) kumbukumbu zote zinazohusiana na kibali;

(b) mipango au ramani za eneo la leseni ambazo zimeandaliwa na au maelekezo ya Kampuni au mmiliki wa kibali;

(c) kanda zote za kumbukumbu, maelezo ya Kampuni, chati ambayo imeandaliwa na Kampuni au mmiliki wa kibali; na

(d) nyaraka nyengine zozote na vifaa kama Mamlaka, kwa notisi iliyotolewa kwa Kampuni au mmiliki wa kibali inaweza kutaka kuwasilishwa.

Upatikanaji wa taarifa kwa umma.

**84.-(1)** Taarifa kuhusiana na shughuli za mafuta na gesi asilia zilizopo katika kumbukumbu za Mamlaka zitakuwa wazi kwa umma kwa mujibu wa utaratibu wa sheria husika.

(2) Mtu anaweza kuhitaji kupatiwa nyaraka za umma ambapo itakuwa bila malipo, ikiwa atapatiwa kwa ukaguzi katika majengo ya Mamlaka, na iwapo atataka kupatiwa nakala, kwa ada ili kufidia gharama za kurudufu nyaraka husika.

(3) Waziri atachapisha katika Gazeti Rasmi na kwa njia nyengine yoyote ili kuwajuilisha watu wenye maslahi:

(a) wito wa zabuni chini ya kifungu cha 49 cha Sheria hii;

(b) notisi ya kutoa leseni na makubaliano ya mafuta na gesi asilia na sababu za kutoa na muhtasari wa masharti ya leseni na makubaliano;

(c) muhtasari wa mpango wa uendelezaji na uendeshaji;

(d) notisi ya kusitisha leseni na makubaliano ya mafuta na gesi asilia; na

(e) sekta kuu zote za uzalishaji wa mafuta, mapato, ukusanyaji wa mapato na taarifa za matumizi.

Usiri wa taarifa.

**85.-(1)** Taarifa zinazowasilishwa kwa Mamlaka kutoka kwa Kampuni na mmiliki wa kibali zitachukuliwa kuwa ni siri na hazitotolewa au kuwekwa bayana kwa mtu mwengine chini ya Sheria hii, isipokuwa kwa idhini ya maandishi ya Waziri.

(2) Idhini iliyotajwa chini ya kifungu kidogo cha (1), haitazuiliwa au kucheleweshwa bila ya sababu za msingi.

(3) Taarifa zinazowekwa bayana kwa upande mwengine zitawekwa bayana kwa masharti na taratibu kama zitakazowekwa katika Kanuni, kuhakikisha kwamba zitachukuliwa kuwa ni siri kwa anayepokea.

Maelezo ya ziada kuwasilishwa.

**86.-(1)** Endapo Mamlaka inasababu za kuamini kwamba kuna mtu ana uwezo wa kutoa maelezo au kutoa nyaraka zinazohusiana na utafutaji au uendelezaji wa utafutaji wa mafuta na gesi asilia, Mamlaka inaweza, kwa notisi ya maandishi kumtaka mtu huyo:

(a) kuwasilisha maelezo kwa maandishi ndani ya kipindi na njia itakayoainishwa katika notisi; au

(b) kuhudhuria yeye mwenyewe au mtu aliyeainishwa katika notisi katika muda na mahala kwa ajili ya kujibu maswali yanayohusiana na uendeshaji wa mafuta na gesi asilia.

(2) Mtu hatosamehewa kuwasilisha maelezo, kujibu swali au kutoa waraka wakati anapohitajika kufanya hivyo chini ya kifungu hiki, itapelekea kuingia kwenye kosa la jinai au kumfanya kuwajibika na adhabu, na maelezo yaliyowasilishwa au majibu yake kuhusu swali hayatokubaliwa juu ya ushahidi uliotolewa dhidi yake katika mwenendo wowote isipokuwa mwenendo wa makosa.

Kushindwa kuwasilisha maelezo.

**87.** Mtu ambae:

(a) amekataa au ameshindwa kufuata matakwa yaliyomo katika notisi ambayo matakwa hayo yanamlazimu kuyatekeleza;

(b) anapaswa kutimiza matakwa yaliyoelezwa katika aya (a) kwa kujua au kutokujua kuwasilisha maelezo kwamba ni ya uongo au yenye kupotosha katika kadhia husika; au

(c) alipowasili katika Mamlaka au mtu yeyote kwa matakwa yaliyoelezwa katika aya (a) kwa kujua au kutokujua ametoa maelezo au nyaraka ambazo ni za uongo au zenye kupotosha kadhia husika,

atakuwa ametenda kosa na atalazimika kulipa faini isiyopungua shilingi milioni hamsini za Kitanzania au kutumikia kifungo kwa kipindi cha miaka mitatu au vyote kwa pamoja.

Fursa ya mtu wa tatu.

**88.-(1)** Mtu anayehitaji kutumia miundombinu inayomilikiwa na mtu mwengine atalazimika kwa malengo na bila ya masharti ya kubaguliwa atakuwa na haki ya kutumia miundombinu hiyo kwa mujibu wa makubaliano na masharti ya Sheria hiyo.

(2) Makubaliano yanayohusiana na matumizi ya miundombinu yatajengeka kwa faida ya uzalishaji uliopatikana kwenye eneo la uzalishaji na motisha za mmiliki ili kuongeza uwezo wa miundombinu na uwekezaji.

(3) Mazungumzo baina ya mmiliki na mtumiaji wa miundombinu yatafanywa kwa misingi ya usawa, mashirikiano mazuri na kwa nia safi.

(4) Makubaliano yanayohusiana na matumizi ya miundombinu yaliyoelezwa chini ya kifungu cha (2) yatawasilishwa kwa Mamlaka kwa kuidhinishwa.

(5) Mamlaka inaweza, baada ya kuthibitisha makubaliano yaliyofanywa chini ya kifungu kidogo cha (2), au pale ambapo hakuna makubaliano yaliyofikiwa ndani ya muda maalum kodi iliyoelezwa na masharti mengine au dharura yamerekebishwa masharti yale yaliyothibitishwa au kuelezwa kwa lengo la kuhakikisha utekelezaji wa miradi inafanyika kwa kuzingatia misingi inayohusiana na usimamizi wa rasilimali.

(6) Mamlaka inaweza kutoa maelezo kuhusiana na matumizi ya miundombinu kwa kuzingatia ufanisi, usimamizi wa rasili mali au maslahi kwa umma na miundombinu hiyo haitaleta athari kwa Kampuni au kwa mtu ambae ana haki ya kutumia.

Wajibu wa usambazaji nchini.

**89.-(1)** Mkandarasi na Kampuni itakuwa na wajibu wa kutosheleza soko la ndani ya Zanzibar kutokana na usawa wa viwango vya uzalishaji.

(2) Kiwango cha mafuta ghafi au gesi asilia ambacho kitahitajika kuuzwa kitakidhi matakwa ya soko la ndani isiyozidi hisa ya faida ya mafuta au gesi asilia ya Mkandarasi na Kampuni.

Tathmini ya bei ya mafuta na gesi asilia.

**90.** Bei ya sehemu ya uzalishaji kwa ajili ya jukumu la usambazaji wa mafuta nchini, katika kila robo mwaka, itaamuliwa kwa namna itakavyoelezwa katika Kanuni.

Uzowefu wa kazi kwa Mkandarasi.

**91.-(1)** Mkandarasi:

(a) atafanya shughuli za awali za utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia katika eneo ambalo limepatiwa kibali cha awali cha utafutaji na uchimbaji kwa misingi mizuri na kwa mujibu wa uzoefu unaokubalika kimataifa katika sekta ya mafuta na gesi asilia;

(b) atafanya shughuli zote za utafutaji katika eneo la utafutaji au uendelezaji kwa misingi mizuri, salama na kwa mujibu wa uzoefu unaokubalika kimataifa katika sekta ya mafuta na gesi asilia;

(c) atachukua hatua zote muafaka kwa ajili ya usalama, afya na masilahi ya watu waliohusika katika shughuli hizo za uendeshaji, utafutaji au eneo la uendelezaji; na

(d) atatekeleza kwa mujibu wa muongozo, makatazo au matakwa *yaliyotolewa* na Mamlaka chini ya Sheria hii.

(2) Kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1), Kampuni na Mkandarasi:

(a) watasimamia upatikanaji wa mafuta na gesi asilia, uchimbaji, mchanyanyiko wa maji au jambo jengine lolote na kuepusha upotevu katika utafutaji au uendelezaji wa mafuta na gesi asilia;

(b) watazuwia madhara katika matabaka ya mafuta na gesi asilia kwenye eneo ambalo leseni haihusiki;

(c) kutenganisha katika utaratibu ulioelezwa:

(i) kila hifadhi ya mafuta na gesi asilia iliyogunduliwa katika eneo la utafutaji au uendelezaji; na

(ii) vyanzo vya maji ikiwa vimegunduliwa katika eneo la utafutaji au uendelezaji kama ambavyo Waziri anaweza kuelekeza kwa notisi ya maandishi iliyotumwa kwa Kampuni;

(d) watazuwia maji au jambo lolote kuingia katika hifadhi ya mafuta na gesi asilia kupitia kwenye kisima katika eneo la utafutaji au uendelezaji isipokuwa pale atakapotakiwa kwa mujibu wa uzoefu unaokubalika kimataifa katika fani ya mafuta na gesi asilia;

(e) kuzuia uchafuzi wa maji yoyote ya kisima, chemchem, mto, mkondo, ziwa, hifadhi, chanzo cha maji, bandari au sehemu ya bahari kwa kuepusha mafuta na gesi asilia, maji ya chumvi, uchimbaji, madawa ya kulainisha, gesi isiyokuwa mafuta na gesi asilia au taka nyengine zozote zinazotokana na uzalishaji au zinazotiririka;

(f) kuwasilisha kwa Mamlaka kabla ya uchimbaji kisima,ripoti kamili ya kitaalamu itakayotumika, makadirio ya muda utakaotumika na dhana zitakazotumika na hatua za usalama zitakazochukuliwa wakati wa kuchimba kisima.

(3) Kampuni na Mkandarasi hawatowasha au kutoa mafuta na gesi asilia bila ya kupata ridhaa ya Mamlaka.

(4) Endapo ridhaa ya maandishi ya Mamlaka imepatikana, hakuna katika kifungu hiki kitakachomzuia mmiliki wa leseni na mkandarasi kuwasha mafuta na gesi asilia kwa mujibu wa masharti ya hati iliyoidhinisha.

(5) Kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (4), uchomaji wa gesi asilia unaweza kuhitajika kwa ajili ya kulinda afya na usalama wa watu katika mazingira ya dharura kwenye eneo la utafutaji na uendelezaji wa mafuta na gesi asilia na kuzuia hasara ya mali katika eneo la utafutaji na uendelezaji wa mafuta na gesi asilia.

(6) Kampuni na Mkandarasi watawasilisha kwa Mamlaka nia ya kurejesha kisima chochote, kufunga au kuziba kwa kisima na hatua zitachukuliwa kwa namna itakavyoelezwa kabla ya ridhaa ya Mamlaka.

(7) Kuchukua hatua zinazofaa kwa ajili ya kulinda usalama, afya, na masilahi ya watu waliohusika katika shughuli hizo za uendeshaji, katika eneo hilo.

Adhabu ya ukiukaji.

**92.** Kampuni, Mkandarasi na mmiliki wa kibali ambaye amekwenda kinyume na kifungu cha 91 atakuwa ametenda kosa na atalazimika kulipa Shilingi za Kitanzania sawa na Dola za Kimarekani zisizopungua Elfu Kumi.

Ukarabati wa miundombinu.

**93.-(1)** Kampuni, Mkandarasi na mmiliki wa kibali:

(a) ataweka katika hali nzuri na kurekebisha miundombinu yoyote kama hizo zinazotumika katika eneo la leseni au kibali;

(b) ataondosha katika maeneo miundombinu yote ambayo haitumiki katika shughuli za utafutaji wa mafuta na gesi asilia ambayo anajishughulisha nayo; na

(c) atachukua hatua muafaka kumtahadharisha mtu ambae yupo katika eneo la miundombinu inayopelekea majanga yanayotokana na miundombinu hiyo.

(2) Masharti yaliyoelezwa katika kifungu kidogo cha (1) hayatotumika kwa miundombinu yoyote ambayo haikuwasilishwa katika eneo ambalo linahusika na leseni, kibali au kwa idhini ya Kampuni au Mkandarasi.

(3) Mtu ambae ataenda kinyume na masharti yaliyomo katika kifungu kidogo cha (1)(a),(b) au (c) atakuwa ametenda kosa na atalazimika kulipa faini ya Dola za Kamarekani zisizopungua Elfu Tano au kifungo kisichopungua miezi sita au vyote kwa pamoja.

Uchimbaji wa mafuta na gesi asilia karibu na mipaka.

**94.-(1)** Kampuni na Mkandarasi hawatachimba kisima katika masafa yanayopungua mita elfu moja kutoka mpaka wa eneo lililopewa leseni isipokuwa kwa ridhaa ya maandishi ya Mamlaka na kwa mujibu wa masharti yaliyoelezwa katika ridhaa hiyo.

(2) Iwapo Kampuni na Mkandarasi watashindwa kutimiza masharti yaliyomo katika kifungu kidogo cha (1) Mamlaka inaweza kuielekeza kwa maandishi Kampuni na Mkandarasi kufanya shughuli moja au zaidi ndani ya muda ulioelezwa katika hati:

(a) kuziba kisima;

(b) kufunga kisima; au

(c) kufuata maelekezo yanayohusiana na uchimbaji au ukarabati wa kisima kama ulivyoainishwa kwa maandishi katika ridhaa hiyo.

(3) Mtu ambae atashindwa au kukataa kutii maelekezo yaliyoelezwa katika kifungu kidogo cha (2) atakuwa ametenda kosa na atalazimika kulipa faini ya Dola za Kimarekani zisizopungua Elfu Tano au kifungo kisichopungua miezi sita au vyote kwa pamoja.

Utafiti wa visima.

**95.-(1)** Mamlaka inaweza, wakati wowote kwa notisi ya maandishi kumuelekeza Mkandarasi na Kampuni:

(a) kufanya utafiti wa eneo la kisima au miundombinu iliyoainishwa katika notisi; na

(b) kuwasilishwa kwa Mamlaka ripoti ya maandishi inayohusiana na utafiti.

(2) Iwapo Mamlaka haitoridhishwa na ripoti ya utafiti iliyowasilishwa chini ya kifungu kidogo cha (1), Mamlaka inaweza kwa notisi ya maandishi kuielekeza Kampuni au Mkandarasi kuwasilisha taarifa kamili kwa maandishi inayohusiana na utafiti huo.

(3) Iwapo mtu ambae amepatiwa maelezo kwa mujibu wa kifungu kidogo (1) (a) ameshindwa au amedharau kutii maelekezo hayo, Mamlaka itawezesha kufanyika utafiti ulioainishwa katika notisi.

(4) Gharama zilizoingiwa kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (3) kufuatia utafiti uliofanyika itachukuliwa kama ni deni la Serikali na litalipwa bila ya kuzingatia kwamba Kampuni husika imepatikana na hatia ya kosa chini ya kifungu kidogo cha (5) cha kifungu hiki.

(5) Mtu ambae amepatiwa maelekezo yaliyoelezwa katika kifungu kidogo cha (1) au cha (2) ameshindwa au amedharau kufuata maelekezo hayo atakuwa ametenda kosa na atalazimika kulipa faini ya Dola za Kamarekani zisizopungua Elfu Ishirini au kifungo kisichopungua miaka mitano au vyote kwa pamoja.

Udhibiti wa mkandarasi.

**96.-(1)** Iwapo leseni ya uendelezaji imetolewa kwa Kampuni ikishirikiana na mkandarasi, mkandarasi huyo kuanzia tarehe iliotolewa leseni bila ya kupata kibali cha Waziri:

(a) hatasajili uhaulishaji wa hisa za mkandarasi kwa mtu mwingine yeyote au kwa mtu aliyeteuliwa nae; au

(b) hatoingia katika makubaliano yoyote na mtu mwengine yeyote, iwapo athari ya kufanya hivyo itampa udhibiti wa kampuni ya mkandarasi au mtu huyo au mtu aliyemteua.

(2) Waziri, kufuatia maombi yaliyofanywa chini ya kifungu hiki, atatoa au atakataa kutoa idhini baada ya kuzingatia maslahi ya umma.

(3) Kwa mujibu wa masharti yaliyomo katika kifungu kidogo cha (2), Waziri anaweza kutaka ombi lolote au taarifa anayohitaji.

(4) Kwa madhumuni ya kifungu hiki:

(a) mtu atachukuliwa kuwa na udhibiti wa kampuni ya mkandarasi ikiwa:

(i) mtu huyo au aliyemteua anamiliki hisa za mtaji ya asilimia ishirini (20%) au zaidi katika kampuni ya mkandarasi; au

(ii) mtu huyo au aliyeteuliwa ana haki ya kuteua au kuzuia uteuzi wa idadi ya Wakurugenzi inayotosheleza kufanya akidi ya mkutano wa Wakurugenzi;

(b) "hisa za mtaji" kuhusiana na kampuni ya mkandarasi, maana yake ni hisa za mkandarasi za kampuni zinazompa haki ya kupiga kura, na zinajumuisha hisa za upendeleo na sio hisa za upendeleo zisizomuwezesha kupiga kura;

(c) "hisa za upendeleo" maana yake ni hisa zinazotoa haki ya kulipwa mgao wa kiwango kilichowekwa, au kisichozidi kiwango kilichowekwa, katika kipaumbele cha ugawaji wa malipo kuhusiana na daraja au daraja nyengine za hisa, ama akiwa au kutokuwa na haki nyengine;

Uwezo wa kuingia.

**97.-(1)** Kwa madhumuni ya Sheria hii, Mamlaka inaweza, katika muda muafaka:

(a) kuingia katika eneo lolote au kuingia katika miundombinu ambayo inahusisiana na:

(i) shughuli za utafutaji wa mafuta na gesi asilia;

(ii) shughuli za uendelezaji wa mafuta na gesi asilia; au

(iii) shughuli za uzalishaji wa mafuta na gesi asilia;

(b) kukagua na kufanya majaribio kwa mtu mwenye sifa, chombo chochote au miundombinu kwa maoni yake inatumika kwa shughuli yoyote ya mafuta na gesi asilia iliyoelezwa katika aya (a);

(c) kuchukua au kuondosha kwa madhumuni ya kufanya uchambuzi, majaribio au kutumia kama ushahidi unaohusiana na kosa dhidi ya Sheria hii, sampuli za mafuta na gesi asilia, maji na sampuli nyenginezo zinazotokana na kisima;

(d) kukagua, kuchukua dondoo na kutoa nakala, nyaraka yoyote inayohusiana na shughuli za mafuta na gesi asilia iliyoelezwa katika aya (a);

(e) itatoa maelekezo na masharti kwa kampuni au kwa mtu yeyote alieajiriwa na kampuni hiyo kuhusiana na afya na usalama wa wafanyakazi walioajiriwa na kampuni au mkandarasi katika shughuli za mafuta na gesi asilia zilizoainishwa katika aya (a);

(f) kwa notisi ya maandishi:

(i) itatoa amri ya kusitisha shughuli za mafuta na gesi asilia au kumuondosha mtu yeyote katika eneo au miundombinu ambayo inatumika kwa shughuli za mafuta na gesi asilia kama zilivyoainishwa katika aya (a); au

(ii) itatoa amri ya kutokuendelea kutumia mashine yoyote au kifaa ambacho mamlaka itaona hakiko salama, mpaka hatua stahiki za kiusalama zilizoelezwa katika notisi, zitachukuliwa na kukamilishwa;

(g) kufanya uchunguzi unaohitajika ili kuhakikisha kwamba masharti ya Sheria hii, na maelekezo yaliyotolewa, makatazo yaliyowekwa au amri zilizotolewa chini ya Sheria hii, zinatekelezwa; na

(h) kupata na kunakili maelezo ya mashahidi, kuhudhuria wito au kufanya uchunguzi unaohusiana na ajali zilizotokea kutokana na shughuli yoyote iliyotajwa katika aya (a) na kuhudhuria mahojiano na kuwahoji mashahidi.

(2) Kabla ya kutumia uwezo ulioelezwa chini ya kifungu kidogo cha (1), iwapo kutakuwa na mtu mwenye dhamana ya eneo, miundombinu au jambo linalohusiana na uwezo ambao anataka kusimamia, mamlaka au afisa aliyepewa mamlaka atajitambulisha kwa mtu ambae ana mamlaka ya kutoa amri au miongozo.

(3) Mtu aliyeathirika na maamuzi, muongozo au amri ya Mamlaka iliyofanywa chini ya kifungu hiki, anaweza kuomba rufaa ya maandishi kwa Bodi.

(4) Iwapo hakuridhika na uamuzi, muongozo au amri iliyotolewa na Bodi, ataomba rufaa kwa Waziri ambae, haraka iwezekanavyo, atasikiliza na kuimaliza rufaa, isipokuwa kwamba kuletwa kwa rufaa hakutoathiri utekelezaji wa uamuzi, muongozo au amri iliyoombewa rufaa ambayo haijasikilizwa.

(5) Endapo rufaa imewasilishwa chini ya kifungu kidogo cha (3) na (4), Mamlaka au Waziri anaweza kufuta au kuthibitisha uamuzi, maelekezo au amri ambayo inaondoa rufaa au kutoa uamuzi, muongozo au amri mpya badala ya ile ya awali, na uamuzi, maelekezo au amri hiyo haitoombewa rufaa tena.

(6) Mtu ambaye ni mkaazi au mwenye dhamana ya jengo au sehemu yoyote, au ambae ni mdhamini mwenye dhamana ya chombo, ndege, mashine au zana zilizotajwa katika kifungu kidogo cha (1) atatoa kwa Mamlaka au afisa aliyeidhinishwa nyenzo zote za msingi na usaidizi ikijumuisha usafirishaji.

Haki ya matumizi ya ardhi kwa mkaazi halali.

**98.-(1)** Mkaazi halali wa ardhi yoyote katika eneo la utafutaji au uendelezaji wa shughuli za mafuta na gesi asilia atakuwa na haki ya kuchunga mifugo au mkulima juu ya ardhi iwapo kulima au kulima huko hakutoingilia shughuli za utafutaji au uendelezaji wa mafuta na gesi asilia.

(2) Mkaazi halali wa ardhi katika eneo la uendelezaji hatojenga jengo lolote katika eneo hilo bila ya ridhaa ya maandishi ya Kampuni, na iwapo Waziri ataona kwamba ridhaa imekataliwa bila sababu ya msingi anaweza kutoa ridhaa kwa mkaazi halali.

(3) Haki iliyotolewa katika leseni au katika hati ya ridhaa au kibali, haitotumiwa kuathiri maslahi ya mkaazi halali wa ardhi kwa mujibu wa shughuli za utafutaji kwa mujibu wa leseni au hati ya ridhaa.

(4) Bila ya kuathiri masharti ya jumla ya kifungu kidogo cha (3), anayefanya shughuli za utafutaji na uendelezaji wa mafuta na gesi asilia kwa mujibu wa leseni au hati ya ridhaa au kibali hatochukua hatua ambayo inaingiliana na:

(a) uvuvi;

(b) usafiri wa majini; au

(c) shughuli yoyote halali inayofanywa kwa njia ya utafutaji, upatikanaji au usafirishaji wa mafuta na gesi asilia au madini,

isipokuwa kwanza ametoa notisi ya maandishi kwa Mamlaka kuhusu jambo analotaka kufanya na muda atakaoutumia.

Fidia kwa usumbufu.

**99.-(1)** Endapo, katika shughuli za utafutaji au uendelezaji wa mafuta na gesi asilia, Kampuni na Mkandarasi wataingilia haki za mkaazi halali wa ardhi yoyote au watasababisha hasara kwa mazao, miti, majengo, ghala au kazi zinazofanywa kulingana na shughuli zinazofanyika, Kampuni na Mkandarasi watamlipa mkaazi halali fidia inayofaa kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi ya Ardhi.

(2) Endapo kiasi cha fidia kinachotakiwa kulipwa kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1) kinatofautiana, upande wowote unaweza kuwasilisha kadhia hii katika Mahakama ya Ardhi kwa maamuzi.

Haki ya ardhi ambayo haijagaiwa.

**100.** Waziri anaehusika na ardhi, iwapo akiridhika kwamba ni muhimu kwa shughuli za uendelezaji au kwa shughuli zinazohusiana na uendelezaji, anaweza kukodisha ardhi kwa mujibu wa masharti atakayoona yanafaa.

Mrahaba wa mafuta na gesi asilia.

**101.-(1)** Mkandarasi atalipa mrahaba na mgao wa mafuta na gesi asilia kama ilivyoelezwa katika Jadweli la Pili.

(2) Mtu ambae atashindwa kulipa mrahaba wa aina yoyote unaohitajika kulipwa chini ya Sheria hii, kabla au baada ya tarehe husika, Mamlaka inaweza kwa notisi ya maandishi iliyotumwa kwa Kampuni na Mkandarasi, kukataza uondoaji, au kujihusisha na shughuli yoyote ya mafuta na gesi asilia katika eneo husika la uendelezaji mpaka mrahaba wote umelipwa.

(3) Faida ya mafuta na gesi asilia itagawanywa baina ya Mkandarasi na Serikali kwa mujibu wa Jadweli la Pili.

(4) Waziri anaweza baada ya kupata idhini ya Baraza la Mapinduzi kurekebisha Jadweli la Pili.

Ada ya mwaka.

**102.-(1)** Kampuni na Mkandarasi watalipa kwa Mamlaka ada ya mwaka kwa leseni kama itakavyoelezwa katika Kanuni.

(2) Ada ya mwaka iliyoelezwa katika kifungu kidogo cha (1) itajumuisha:

(a) kodi ya eneo; na

(b) ada ya mafunzo na utafiti.

Malipo ya ziada.

**103.-(1)** Mkandarasi atalipa kwa Mamlaka malipo ya ziada kama ilivyoelezwa katika Kanuni au makubaliano ya mafuta na gesi asilia kama hali itakavyokuwa.

(2) Maamuzi ya malipo ya ziada yatafanywa na Waziri baada ya kuidhinishwa na Baraza la Mapinduzi.

Kodi.

**104.** Mtu yeyote au Mkandarasi anaejishughulisha na shughuli za mafuta au gesi asilia atalazimika kulipa kodi kwa mujibu wa Sheria itakayotungwa na Baraza la Wawakilishi kwa ajili hiyo.

Mipaka ya urejeshaji wa gharama.

**105.-(1)** Kampuni na mkandarasi wenye haki ya leseni ya utafutaji wa mafuta na gesi asilia au mwenye leseni zaidi ya moja ya uendelezaji ndani ya eneo la mkataba atarejesha gharama alizotumia kwa mujibu wa mipaka ya leseni husika.

(2) Gharama zitakazorejeshwa zilizoainishwa katika mkataba wa eneo la leseni au kitalu kilichopo ndani ya eneo la mkataba zinaweza kurejeshwa kutokana na mapato pekee ya mafuta na gesi asilia yaliyopatikana kutoka katika eneo la uendelezaji ambalo limepatikana kuanzia na wakati wa uzalishaji wa mafuta na gesi asilia kutoka katika eneo hilo la uendelezaji.

Masharti ya malipo.

**106.** Malipo kwa Serikali kwa mujibu wa Sheria hii yatakuwa katika Dola za Kimarekani.

Adhabu kwa ucheleweshaji.

**107.** Iwapo Mkandarasi atashindwa kufanya malipo chini ya Sheria hii kabla au wakati unaohitajika, Mkandarasi huyo atalazimika adhabu ya kulipa malipo ya ziada ya asilimia mbili (2%) ya kiwango ambacho hajakilipa kwa kila siku ambayo atashindwa kulipa.

Urejeshwaji wa malipo chini ya Sheria hii.

**108.** Malipo na kodi chini ya Sheria hii yatakuwa ni deni la Serikali na yatalipwa kwa mujibu wa Sheria zozote husika.

Dhamana ya utekelezaji.

**109.-(1)** Mkandarasi atawasilisha kwa Waziri bila ya masharti, dhamana isiyorejeshwa kutoka katika benki inayokubaliwa na Waziri.

(2) Waziri ataamua kiasi na namna ya dhamana kwa mujibu wa Kanuni na kwa mujibu wa masharti ya leseni iliyotolewa au masharti ya mkataba ***wa*** mafuta na gesi asilia ulioingiwa chini ya Sheria hii.

## SEHEMU YA TANO
## UKOMO WA SHUGHULI ZA UTAFUTAJI WA MAFUTA NA GESI ASILIA

Mpango wa ukomo wa shughuli za mafuta na gesi asilia.

**110.(1)** Kampuni na Mkandarasi watawasilisha mpango wa ukomo wa shughuli za mafuta na gesi asilia na marekebisho yake kwa Mamlaka:

(a) kabla ya kibali cha uzalishaji wa mafuta na gesi asilia au leseni maalum ya kuweka na kuendesha miundombinu havijamaliza muda wake au kusalimishwa; au

(b) angalau miaka mitano kabla ya kusitishwa kwa kudumu matumizi ya miundombinu.

(2) Mpango wa ukomo wa shughuli za mafuta na gesi asilia uliyoelezwa katika kifungu kidogo cha (1) yatajumuisha mapendekezo ya uzalishaji endelevu au kusitishwa kwa uzalishaji, miundombinu ya ukomo wa mafuta na gesi asilia na taarifa nyengine zilizoelezwa katika Kanuni au mikataba ya mafuta na gesi asilia kama hali itakavyokuwa.

(3) Ukomo wa matumizi ya miundombinu wa shughuli za mafuta na gesi asilia ulioelezwa katika kifungu kidogo cha (2), unaweza kujumuisha matumizi ya ziada ya miundombinu katika shughuli za mafuta na gesi asilia, matumizi mengine, kuondoa yote au sehemu ya miundombinu hiyo na kuharibu au kuangamiza.

(4) Mpango wa ukomo wa shughuli za mafuta na gesi asilia utakuwa na taarifa na tathmini zitazoonekana ni muhimu katika kutoa maelekezo chini ya kifungu cha 114(1).

(5) Mamlaka inaweza, baada ya kupokea mpango wa ukomo wa shughuli za mafuta na gesi asilia, kuhitaji taarifa nyengine na tathmini, au inaweza kuhitaji mpango mpya au uliorekebishwa wa ukomo wa shughuli za mafuta na gesi asilia.

(6) Kampuni na mkandarasi watauendeleza mpango wa ukomo wa shughuli za utafutaji wa mafuta na gesi asilia:

(a) unaohusiana na maombi ya baadae ya kibali, kuongeza au kufanya mabadiliko muhimu ya miundombinu;

(b) njia yoyote inayotarajiwa au gharama za kufanyia kazi ya ukomo wa shughuli za mafuta na gesi asilia zinazobadilika mara kwa mara kutokana na matokeo ya teknolojia mpya;

(c) iwapo teknolojia ya awali haikidhi haja au haruhusiki tena; au

(d) wakati inapotakiwa na Mamlaka ndani ya kipindi maalum kilichoainishwa katika maombi.

Mfuko wa ukomo wa shughuli za utafutaji wa mafuta na gesi asilia.

**111.-(1)** Kampuni na Mkandarasi wataanzisha mfuko wa ukomo wa shughuli za mafuta na gesi asilia wakila eneo la uendelezaji, au kwa miundombinu yoyote inayofanyakazi kuhusiana na uzalishaji baada ya kibali cha uzalishaji kutolewa kwa ajili ya kujua gharama zinazohusiana na utekelezaji wa mpango huo.

(2) Mfuko wa ukomo uwe unaojitosheleza kugharamia gharama za ukomo wa shughuli za mafuta na gesi asilia.

(3) Malipo ya mfuko wa kugharamia ukomo wa shughuli za mafuta na gesi asilia, yatachangiwa na Kampuni na mkandarasi kama makubaliano yatakavyoainishwa.

(4) Baada ya kukamilika shughuli zote za ukomo wa shughuli za mafuta na gesi asilia, ikitokezea kwamba fedha za mfuko wa ukomo ulioazishwa ni nyingi zaidi kuliko gharama za majukumu ya shughuli za ukomo zilizotumika, fedha zilizobakia zitagaiwa baina ya Kampuni na mkandarasi kwa mgao sawa kulingana na uchangiaji.

Taarifa ya kusitisha matumizi.

**112.** Kampuni na mkandarasi watatoa taarifa ya maandishi kwa Mamlaka muda wa kusitisha kwa miundombinu ikiwa matumizi ya miundombinu hiyo inatarajiwa kusitishwa moja kwa moja kabla ya leseni kumalizika muda wake.

Kuondosha miundombinu ya ukomo wa shughuli za mafuta na gesi asilia.

**113.(1)** Mamlaka inaweza kutoa miongozo juu ya uondoshaji wa miundombinu ya ukomo wa shughuli za mafuta na gesi asilia na itatoa muda juu ya kutimizwa kwa miongozo hiyo.

(2) Miongozo iliyotolewa na mamlaka chini ya kifungu kidogo cha (1) itahusiana na utaalam, usalama,mazingira na uchumi pamoja na kuzingatia watumiaji wengine.

(3) Kampuni, mkandarasi au mmiliki wa miundombinu atafuata miongozo inayohusiana na uondoshaji, isipokuwa imeelezwa vyenginevyo na Mamlaka.

(4) Wajibu wa kufuata maelekezo yanayohusiana na uondoshaji wa miundombinu ya ukomo wa shughuli za mafuta na gesi asilia itatumika hata pale ambapo miongozo itafanywa au itatekelezwa baada ya kumaliza muda wa leseni.

(5) Endapo maelekezo yameelekeza kwamba miundombinu iendelee kutumika katika shughuli za mafuta na gesi asilia au kwa madhununi mengine, Kampuni, mkandarasi au mmiliki wa miundombinu hiyo kwa pamoja watalazimika kuhakikisha kwamba miongozo ya baadae kuhusiana na uondoshaji wa miundombinu hiyo inafuatwa, isipokuwa kama yametolewa maelekezo mengine na Mamlaka.

(6) Endapo maelekezo yanahusiana na uondoshaji wa miundombinu hayakufanyika katika muda uliopangwa, Mamlaka inaweza kuchukua hatua sitahiki kwa niaba ya Kampuni, mkandarasi au upande mwengine unaohusika.

(7) Endapo Mamlaka imechukua hatua zozote stahiki chini ya kifungu kidogo cha (6) kwa niaba ya Kampuni, mkandarasi au upande mwengine husika, hasara yoyote au gharama iloingiwa kutokana na hatua hiyo, italipwa na Kampuni, mkandarasi au upande mwengine husika.

Uondoshaji wa mali za Kampuni na Mkandarasi.

**114.-(1)** Endapo leseni imesalimishwa au imemaliza muda, au kwa sababu ya kurejeshwa imesita kufanya kazi katika eneo ambalo leseni hiyo imetolewa, Waziri kwa notisi ya maandishi iliyotumwa kwa Kampuni ataelekeza ndani ya muda ulioainishwa katika notisi:

(a) kuondosha au kuwezesha kuondoshwa kutoka katika eneo ambalo mali imewekwa kupelekwa katika eneo ambalo mtu anafanyakazi au kujihusisha na shughuli za mafuta na gesi asilia au kufanya utaratibu ambao utairidhisha Mamlaka kuhusiana na mali hiyo;

(b) kuziba au kufunga, katika hali itakayoiridhisha Mamlaka, visima vyote vilivyochimbwa katika eneo ambalo mtu anajishughulisha au kujihusisha na shughuli zinazohusiana na mafuta na gesi asilia; na

(c) kuweka sharti, litakaloiridhisha Mamlaka kwa ajili ya uhifadhi na ulinzi wa mazingira na maliasili katika eneo hilo.

(2) Endapo mtu ambae amepewa muongozo kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1) amekataa au ameshindwa kutii muongozo ndani ya muda ulioainishwa katika notisi, mtu huyo atakuwa ametenda kosa na atalazimika adhabu inayolingana na kiwango cha fedha kilichoingiwa kutokana na shughuli iliyofanyika.

Uondoshaji na uuzaji wa mali.

**115.-(1)** Endapo Serikali itachukua miundombinu na maelekezao yaliyotolewa chini ya kifungu cha 113(1) na 114(1) hayakufuatwa, Mamlaka inaweza:

(a) kufanya au kuwezesha kufanyika mambo yote au sehemu ya mambo hayo yaliyotakiwa kufanywa kwa mujibu wa maelekezo;

(b) kuondosha au kuwezesha kuondosha kwa namna ambavyo Mamlaka inaona inafaa, mali zote au sehemu ya mali hizo kutoka katika eneo husika;

(c) kuondosha, kwa namna ambayo Mamlaka inaona inafaa, mali yote au sehemu ya mali hiyo kutoka katika eneo husika; na

(d) ikiwa imetuma nakala ya notisi ambayo maelekezo yametolewa kwa ambae Mamlaka imejiridhisha kuwa ni mmiliki wa mali au sehemu ya mali hiyo, itauza au kuwezesha kuuza kwa njia ya mnada au vyenginevyo mali yote au sehemu ya mali hiyo iliyoainishwa katika kifungu hiki kuwa inamilikiwa au kwamba Mamlaka inaamini inamilikiwa na mtu huyo.

(2) Mamlaka itakata kutoka kwenye mauzo ya mali chini ya kifungu kidogo cha (1):

(a) gharama na matumizi yaliyoingiwa na Mamlaka kuhusiana na mali hiyo;

(b) gharama na matumizi yaliyoingiwa na Mamlaka kuhusiana na kufanya jambo lolote lililotakiwa kwa mujibu wa maelekezo yaliyotakiwa kufanywa na mtu huyo, kwamba mtu huyo amekwishatiwa hatiani kwa kosa lililoainishwa chini ya kifungu hiki; na

(c) ada au kiwango cha malipo kinachopaswa kulipwa na mtu chini ya Sheria hii kwa ajili ya leseni.

(3) Gharama na matumizi yaliyoingiwa na Mamlaka chini ya kifungu kidogo cha (1):

(a) endapo zimeingiwa kutokana na kuondosha, kuharibu au kuuza mali, ni deni la mmiliki wa mali kwa Serikali; na

(b) ikiwa zimeingiwa kuhusiana na kufanya jambo lolote lililotakiwa kwa mujibu wa maelekezo chini ya Sheria hii kufanywa na Kampuni, mkandarasi au mmiliki wa

miundombinu, ni deni la mtu huyo kwa Serikali, na kwa kiwango ambacho hakijalipwa chini ya kifungu kidogo cha (2), kinaweza kulipwa kwa amri ya mahakama yenye uwezo wa kufanya hivyo.

Dhima ya fidia ya uondoshaji wa ukomo wa miundombinu ya shughuli za mafuta na gesi asilia.

**116.-(1)** Mtu ambae anaetakiwa kutekeleza maamuzi yanayohusiana na uondoshaji wa ukomo wa miundombinu ya shughuli za mafuta na gesi asilia atawajibika kwa hasara au usumbufu aliousababisha kuhusiana na uondoshaji wa miundombinu au utekelezaji mwengine wa maamuzi.

(2) Endapo Kampuni na mkandarasi wametelekeza miundombinu watawajibika kwa hasara waliyosababisha inayohusiana na utelekezaji wa miundombinu.

(3) Endapo kutakuwa na upande mmoja au zaidi unaowajibika chini ya kifungu kidogo cha (1) au cha (2) pande hizo zitaungana kwa pamoja au mmoja mmoja kuwajibika kwa majukumu yote yanayohusiana na fedha.

(4) Endapo kutatokea haja ya kutelekeza miundombinu, Kampuni, mkandarasi na Serikali itahakikisha kwamba matengenezo ya baadae, jukumu na wajibu utachukuliwa na Serikali kutokana na fidia ya fedha inayokubalika.

Kuchukuliwa kwa miundombinu kwa Serikali.

**117.-(1)** Serikali inaweza kuchukua miundombinu iliyotumiwa na mkandarasi iwapo:

(a) leseni imekwisha muda wake;

(b) leseni imesalimishwa au kufutwa;

(c) gharama za mkandarasi zimesharejeshwa; au

(d) matumizi ya miundombinu yamekatishwa moja kwa moja.

(2) Endapo uchukuwaji wa miundombinu umekusudiwa kutumiwa kwa haki ya mali ya mtu binafsi, fidia italipwa kwa mujibu wa sheria na taratibu zilizoelezwa katika Kanuni.

(3) Endapo Serikali itachukua miundombinu, miundombinu hiyo na nyenzo nyengine zitawekwa kwa namna ambayo shughuli zinaweza kuhitaji hali hiyo pamoja na matengenezo muafaka kama inavyohitajika kwa ajili ya kuhakikisha uwezo wa kufanyakazi miundombinu hiyo.

(4) Mgogoro wowote utakaotokea kuhusiana na fidia inayopaswa kulipwa kwa Serikali kwa kukosa kufanya ukarabati, fidia hiyo itaamuliwa na Mthamini wa Serikali au mamlaka nyengine yoyote husika.

(5) Endapo Serikali itachukua miundombinu, Mamlaka itaweka utaratibu wa namna ya miundombinu hiyo kuendelea kutumika.

## SEHEMU YA SITA
## AFYA NA USALAMA KAZINI NA MISINGI YA MAZINGIRA

Afya na usalama kazini.

**118.-(1)** Shughuli za mafuta na gesi asilia zitafanywa kwa namna ya kuwezesha kuwepo kwa usalama wa hali ya juu na kuendelezwa kwa mujibu ya maendeleo ya teknolojia, uzoefu na viwango vinavyokubalika katika sekta ya mafuta na gesi asilia, afya na usalama kazini na sheria nyengine zozote zinazohusika.

(2) Kampuni, mkandarasi na mwendeshaji:

(a) ataanzisha, kutekeleza, kufuatilia na kuendeleza mfumo bora wa kiutawala uliosanifiwa kwa ajili ya kuhakikisha utaratibu na uendelezaji unafuatwa kwa matakwa yote yanayotumika katika afya, usalama na mazingira ya kazi kama ilivyoelezwa na Kanuni;

(b) ataainisha majanga na kutathmini hali hatarishi zinazotokana na kazi yoyote iliyofanywa wakati wa shughuli za kazi za mafuta na gesi asilia iliyofanywa kwa mujibu wa leseni, kazi ambazo zinahatarisha afya za watu walioajiriwa kwa ajili ya kazi hiyo na hatua zinazopaswa kuchukuliwa ili kutii masharti ya Sheria hii;

(c) ataendeleza na kuwasilisha mpango unaoonesha njia ya kujikinga, ushughulikiaji na upunguzaji wa virusi/ukimwi na maradhi mengine ya kuambukiza katika eneo lililotolewa leseni ya shughuli za mafuta na gesi asilia;

(d) atahakikisha usalama wa mtu yeyote alieajiriwa au vyenginevyo aliepo karibu na mitambo unafanywa kwa mujibu wa sheria za afya, usalama wa kazini au sheria nyengine yoyote husika; na

(e) atalinda mazingira na mali asili ikiwa na pamoja na kuchukua hatua za tahadhari kuzuia uchafuzi na uharibifu wa mazingira.

Mahitaji ya jumla kwa ajili ya maandalizi ya dharura.

**119.** Kampuni, mkandarasi au mtu mwengine yeyote anaeshiriki katika shughuli za mafuta na gesi asilia, wakati wote atadumisha maandalizi ya kuchukua hatua za dharura kwa lengo la kukabiliana na ajali na dharura ambazo zinaweza kusababisha upotevu wa maisha, majaraha, uchafuzi wa mazingira au madhara makubwa kwa mali.

Maandalizi ya dharura dhidi ya mashambulizi ya makusudi.

**120.-(1)** Kampuni, mkandarasi na mtu mwengine yeyote ataanzisha na kudumisha hatua za kiusalama kuepuka mashambulizi dhidi ya miundombinu na wakati wote atakuwa na mipango ya dharura kushughulikia mashambulizi hayo.

(2) Kampuni, mkandarasi na mtu mwengine yeyote ataweka miundombinu katika mamlaka husika kwa ajili ya hatua za dharura na usalama ikijumuisha na uchimbaji na pale ambapo ni muhimu atashiriki katika uchimbaji huo.

Maeneo ya usalama.

**121.-(1)** Kutakuwa na eneo la usalama lililozunguka kila miundombinu inayotumika kwa ajili ya shughuli za mafuta na gesi asilia isipokuwa kama itaamuliwa vyenginevyo na Mamlala.

(2) Mamlaka inaweza, endapo zitatokea ajali na dharura, kuanzisha au kuzidisha maeneo ya usalama chini ya kifungu kidogo cha (1).

(3) Kiwango cha maeneo ya usalama yaliyoainishwa katika kifungu kidogo cha (1) na cha (2) yataamuliwa na Mamlaka.

(4) Endapo maeneo ya usalama yatazidishwa nje ya maeneo ya nchi nyengine, Mamlaka itamshauri Waziri kabla ya kutumia uwezo ulioelezwa chini ya kifungu kidogo cha (2).

(5) Mamlaka inaweza kuelekeza kwamba:

(a) eneo linalohusiana na eneo la usalama litaanzishwa ndani ya muda muafaka kabla ya kuweka miundombinu iliyoelezwa katika kifungu kidogo cha (1); au

(b) kutakuwa na eneo la usalama karibu na mbele lililotelekezwa au miundombinu iliyotupwa au sehemu ya miundombinu hiyo.

(6) Shughuli haitofanyika katika maeneo ya usalama bila ya kupata ruhusa ya Mamlaka.

Usitishaji wa shughuli za mafuta na gesi asilia.

**122.-(1)** Endapo kutatokezea ajali au dharura, Kampuni, mkandarasi au mtu mwengine yeyote anaehusika na shughuli za uendeshaji na matumizi ya miundombinu atasitisha shughuli za mafuta na gesi asilia.

(2) Endapo mazingira maalum yatajitokeza, Waziri anaweza kutoa amri kwamba shughuli za mafuta na gesi asilia zisitishwe au anaweza kuweka masharti ya kuruhusu kuendelea kwa shughuli hizo.

(3) Endapo Waziri ataweka amri chini ya kifungu kidogo cha (2) kulingana na mazingira ambayo hayakusababishwa na Kampuni, anaweza, baada ya maombi, kuongeza muda ambao leseni itaendelea kutumika na kupunguza majukumu ya Kampuni.

Tume ya uchunguzi.

**123.** Endapo ajali itatokezea inayohusiana na shughuli za mafuta na gesi asilia na Waziri akaona ajali kuwa ni kubwa, anaweza kuteuwa Tume ya kufanya uchunguzi katika ajali hiyo.

Kufuata misingi ya mazingira.

**124.-(1)** Kampuni, mkandarasi na mtu mwengine yeyote anaefanyakazi, mwenye wajibu au mwenye uwezo chini ya Sheria hii unaohusiana na shughuli za mafuta na gesi asilia, atafuata misingi ya mazingira na usalama iliyoelezwa katika sheria ya Usimamizi wa Mazingira Zanzibar na sheria nyengine husika.

(2) Kampuni, mkandarasi na mwendeshaji mwengine yeyote atahakikisha kwamba usimamizi wa uzalishaji, usafirishaji, uhifadhi, usarifu na uondoshaji wa taka zinazotokana na shughuli za mafuta na gesi asilia unafanywa kwa kuzingatia misingi ya mazingira na usalama ulioelezwa katika sheria ya Usimamizi wa Mazingira na sheria nyengine husika.

(3) Kampuni na mkandarasi wanaweza kuingia katika makubaliano na vyombo vyenye uwezo kwa ajili ya kusimamia usafirishaji, uhifadhi, usarifu na uondoshaji wa taka zinazotokana na shughuli za mafuta na gesi asilia.

(4) Kampuni na mkandarasi wataomba kibali kwa Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira Zanzibar kwa ajili ya usimamizi, usafirishaji, uhifadhi, usarifu na uondoshaji wa taka zinazotokana na shughuli za mafuta na gesi asilia.

(5) Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira Zanzibar ikishauriana na Mamlaka inaweza kutoa kibali kwa ajili ya usimamizi, kwa chombo kilichoingia katika makubaliano usafirishaji, uhifadhi, usarifu na uondoshaji wa taka zinazotokana na shughuli za mafuta na gesi asilia na Kampuni na mkandarasi chini ya kifungu kidogo cha (3) kwa masharti yaliyoelezwa katika kibali.

(6) Mtu ambaye anaeshughulikia usimamizi wa uzalishaji, usafirishaji, uhifadhi, usarifu na uondoshaji wa taka zinazotokana na shughuli za mafuta na gesi asilia bila ya kibali au ameshindwa kufuata masharti yaliyoelezwa katika kibali atakuwa ametenda kosa na atalazimika kulipa faini isiyopungua Dola za Kimarekani Milioni Moja au kifungo cha miaka kumi au vyote kwa pamoja.

Athari za uchafuzi na uharibifu wa mazingira.

**125.-(1)** Katika utekelezaji wa shughuli zao za mafuta na gesi asilia, Kampuni, mkandarasi au mtu mwengine yeyote atachukua hadhari zote muhimu kuhifadhi mazingira ili kulinda afya, maumbile, bioanuwai, miti, wanyama, mifumo ya kimazingira, ardhi, hali ya hewa, utamaduni, akiolojia na urithi wa sanaa.

(2) Kwa madhumuni ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Kampuni na mkandarasi watawasilisha katika Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira na Mamlaka ya udhibiti wa mafuta na gesi asilia, mipango yote muhimu inayohitajika kwa mujibu wa sheria ya Usimamizi ya Mazingira Zanzibar.

(3) Kampuni na mkandarasi watalipa fidia kwa Mamlaka kwa athari yoyote ya mazingira au mtu, mara inapogundulika katika shughuli za uendeshaji wa mafuta na gesi asilia na njia mbadala za kulipa fidia zitafuata.

(4) Shughuli za mafuta na gesi asilia zitafanyika kwa mujibu wa sheria zinazotumika, kanuni na uzoefu wa ujumla wa sekta ya mafuta na gesi asilia unaokubalika wa kimazingira, usalama, usafi na afya.

Dhima kwa Uchafuzi na Uharibifu wa Mazingira.

**126.-(1)** Kampuni, mkandarasi na mtu mwengine yeyote atawajibika kwa uchafuzi wa mazingira bila ya kujali kushindwa kwake.

(2) Pale inapojitokeza kwamba tukio lisiloepukika la maumbile, vita, utendaji wa mamlaka husika au tukio la janga la maumbile limechangia kwa kiasi kikubwa madhara au kwa ukubwa wake, wa mazingira ambao upo nje ya udhibiti wa Kampuni au mkandarasi, dhima inaweza kupunguzwa kwa kiasi kinachofaa, kwa kuzingatia:

(a) ukubwa wa shughuli;

(b) mazingira ya upande uliopata madhara; na

(c) fursa ya kuchukua bima.

Dhima ya kuharibu uchafuzi wa mazingira bila ya leseni au kibali.

**127.-(1)** Endapo uharibifu, uchafuzi au madhara yatatokezea wakati wa shuhuli za mafuta na gesi asilia na shughuli hiyo imefanyika bila ya leseni au kibali, upande uliofanya shughuli hiyo utawajibika kwa madhara bila ya kujali kushindwa kwake.

(2) Dhima itatumika kwa mtu mwengine yeyote ambae ameshiriki katika shughuli hiyo na ambae anajua au alipaswa kujua kuwa shughuli hiyo ilifanyika bila ya kibali.

Madai ya fidia.

**128.-(1)** Dhima ya Kampuni na mkandarasi kwa ajili ya hasara ya uchafuzi au uharibifu wa mazingira itadaiwa kwa mujibu wa Sheria hii na sheria nyengine yoyote zinazotumika.

(2) Dhima kwa uchafuzi au uharibifu wa mazingira haitodaiwa dhidi ya:

(a) mtu yeyote isipokuwa Kampuni na mkandarasi ambae wanachukua hatua za kuzuia, kupunguza kiwango cha uchafuzi wa mazingira, kuokoa maisha au kuokoa mali ambazo zimehatarishwa kutokana na shughuli za mafuta na gesi asilia, isipokuwa hatua itakayochukukuliwa inapingana na makatazo yaliyowekwa na mamlaka husika au mtu aisiyekuwa mamlaka husika bila ya kuzingatia makatazo yaliyotolewa na mwendeshaji au mmiliki wa mali iliyohatarishwa; au

(b) mtu yeyote alieajiriwa na Kampuni au mtu alielezwa katika aya (a).

(3) Endapo Kampuni na mkandarasi wametakiwa na Mahkama kulipa fidia kwa uchafuzi wa mazingira, lakini wameshindwa kulipa ndani ya muda uliotolewa katika hukumu, upande ambao umepata hasara unaweza kuchukua hatua dhidi ya upande uliosababisha hasara hiyo kwa namna ambavyo kama Kampuni na mkandarasi wanaweza kuchukua hatua kwa kitendo hicho dhidi ya upande uliosababisha hasara.

(4) Kampuni na mkandarasi wanaweza kudai fidia kwa upande ambao umesababisha uchafuzi wa mazingira kwa Kampuni na mkandarasi kwa namna ambavyo kama Kampuni na mkandarasi wanaweza kuchukua hatua kwa kitendo hicho dhidi ya upande uliosababisha hasara.

Madai ya fidia kwa uchafuzi wa mazingira.

**129.-(1)** Kampuni na mkandarasi hawataweza kudai fidia kwa hasara iliyosababishwa na uchafuzi wa mazingira kwa mtu yeyote aliyesameheka na dhima, isipokuwa iwapo mtu huyo amefanya kwa masukudi au kwa uzembe uliopitiliza.

(2) Dhima ya kusababisha uchafuzi inaweza kupunguzwa kwa kiasi ambacho kinakubalika katika muonekano unaotizamika, uwezo wa kiuchumi na hali ya kimazingira kwa ujumla.

(3) Makubaliano yoyote ya usababishaji wa uchafuzi wa mazingira kuhusiana na madai dhidi ya mtu ambae dhima iliyowekwa inapingana na kifungu kidogo cha (1) haitokubalika na haitadaiwa fidia.

Mamlaka.

**130.** Hatua za kisheria zinazohusiana na fidia kwa uchafuzi wa mazingira zitawasilishwa mbele ya mahakama yenye mamlaka katika eneo ambalo athari au shughuli za mafuta na gesi asilia zinafanyika au sehemu ambapo hasara imetokezea.

Usimamizi wa mazingira.

**131.-(1)** Huduma zote za kimiuondombinu zilizoanzishwa na kuendeshwa kuhusiana na mfumo wa mafuta na gesi asilia itaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Zanzibar.

(2) Endapo tathmini ya athari ya kimazingira itahitajika au masharti yanahitaji kutimizwa kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Zanzibar na sheria nyengine husika, muombaji leseni au idhini atatimiza masharti au matakwa hayo.

(3) Masharti yatawekwa ili kuyarejesha mazingira katika hali yake ya maumbile na mpango wa ukomo wa miundombinu ya mafuta na gesi asilia kabla ya usitishwaji wa matumizi, na kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Zanzibar na Sheria nyengine husika.

Uvujaji wa mafuta na gesi asilia.

**132.-(1)** Kampuni na mkandarasi watawasilisha tathimini kamili ya athari za uharibifu wa mazingira kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Zanzibar kwa mpango wa uhifadhi na uwajibikaji dhidi ya uvujaji wa mafuta na gesi asilia.

(2) Endapo kutakuwa na uvujaji wa mafuta na gesi asilia unaosababisha au kuleta madhara makubwa kwa afya na usalama wa jamii, Kampuni na mkandarasi watawasilisha kwa haraka iwezekanavyo kuchukua hatua muhimu kwa ajili ya kusitisha uvujaji au kupunguza madhara ya uvujaji huo.

(3) Bila kuathiri kifungu kidogo cha (1), Kampuni au mkandarasi ndani ya masaa ishirini na nne ya ugunduzi wa uvujaji wa mafuta na gesi asilia, watatoa taarifa ya tukio hilo kwa Mamlaka.

Umwagikaji wa Mafuta na gesi asilia na vinavyotokana navyo.

**133.-(1)** Endapo kutakuwa na umwagikaji mkubwa wa mafuta na gesi asilia au kemikali zinazohusiana nazo, msimamizi atatoa taarifa ya tukio hilo kwa Mamlaka ndani ya masaa ishirini na nne mara tu baada ya umwagikaji huo wa mafuta na gesi asilia.

(2) Kampuni, mkandarasi au mmiliki wa kemikali za mafuta na gesi asilia kwa haraka atachukua hatua stahiki kusafisha umwagikaji huo wa kemikali hizo na atalipa gharama kwa mujibu wa Sheria zinazohusika.

(3) Endapo Kampuni, mkandarasi au mtu aliyeelezwa chini ya kifungu kidogo cha (2) ameshindwa kutimiza matakwa ya Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira Zanzibar ndani ya muda ulioelezwa katika notisi au kwa kipindi kingine zaidi ya kile kipindi kilichoelezwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira Zanzibar, inaweza kuruhusu kwa maandishi, au kusababisha kuchukuliwa hatua kama itakavyoona inafaa, kusafisha umwagikaji huo na kurejesha gharama zilizoingiwa kwa mujibu wa sheria zinazohusika.

(4) Kifungu hiki kitatumika kwa tukio ambalo:

(a) linajumuisha au linatokana, kwa ujumla au sehemu, na umwagikaji wa mafuta na gesi asilia au kujumuisha athari za kemikali za mafuta na gesi asilia au kemikali zinazohusiana na shughuli hizo; au

(b) limetokana na usafishaji au urejeshaji katika hali ya asili ya sehemu husika.

(5) Endapo taasisi ya Serikali au Mamlaka za Mitaa zimeingia gharama kwa sababu ya kutokezea kwa tukio ambalo kifungu hiki kitatumika, gharama hizo zilizoingiwa na Mamlaka husika zitarejeshwa na kuwa deni la Serikali kwa mujibu wa sheria husika.

(6) Gharama zitarejeshwa:

(a) iwapo gharama zimeingiwa na Mamlaka za Mitaa; na

(b) iwapo gharama zimeingiwa na taasisi husika ya Serikali.

(7) Gharama iliyoingiwa itarejeshwa kutoka:

(a) iwapo tukio lililoelezwa katika aya ya (a) ya kifungu kidogo cha (4):

(i) mtu ambae alikuwa mmiliki wa kemikali za mafuta na gesi asilia au kemikali zinazohusina nazo wakati wa tukio;

(ii) mtu ambae anao udhibiti au umiliki wa kemikali za mafuta na gesi asilia au kemikali zinazohusina nazo wakati wa tukio ; au

(iii) mtu ambae amesababisha tukio;

(b) iwapo tukio liloelezwa katika aya (b) ya kifungu kidogo cha (4):

(i) leseni husika au mwenye kupata idhini;

(ii) mmiliki wa maeneo husika, majengo, miundombinu au mtambo ambapo uvujishaji umeanzia;

(iii) mtu aliyesababisha tukio.

(8) Bila ya kuathiri sharti la kifungu hiki kidogo, gharama hazitalipwa kwa mtu yeyote atakaethibitisha kwamba:

(a) tukio limetokana na sababu zilizo nje ya uwezo wa mtu huyo au kwa kufanya au kuacha kufanya tendo kwa mtu mwengine;

(b) mtu huyo asingeweza kuzuwia tukio hilo hata kwa kufanya bidii inayostahiki; au

(c) tukio halikuchangiwa na mtu kwa kufanya au kuacha kufanya ambae ni mwajiriwa au wakala wa mtu huyo wakati wa kutokea tukio hilo.

(9) Kwa madhumuni ya kifungu hiki, "umwagikaji mkubwa wa mafuta na gesi asilia au kemikali zinazohusiana na shughuli za mafuta na gesi asilia" maana yake ni umwagikaji wa mafuta na gesi asilia au kemikali zinazotokana nazo ambazo zitasababisha upatikanaji wake kuwa ni zaidi ya kiwango kilichoruhusiwa na Sheria za Usimamizi wa Mazingira.

## SEHEMU YA SABA
## THAMANI YA WADAU WA NDANI, JUKUMU LA USHIRIKISHAJI JAMII NA KIAPO CHA UADILIFU

Maendeleo ya jamii na masharti ya bidhaa na huduma.

**134.-(1)** Kampuni na wakandarasi watachangia katika jamii kwa:

(a) kusaidia taasisi za kijamii za elimu ya juu na vituo vya elimu ya amali ili kuwawezesha kushiriki katika shughuli za mafuta na gesi asilia kupitia mafunzo na ajira; na

(b) kuchukuwa hatua za udhamini, kuendeleza na kuwashajihisha wawekezaji wazalendo kuwekeza katika shughuli za mafuta na gesi asilia.

(2) Kampuni na wakandarasi watatoa kipaumbele kwa bidhaa na huduma zilizopo katika soko la ndani linasimamiwa na wazanzibari au kampuni zilizopo Zanzibar.

(3) Endapo bidhaa na huduma zinazohitajika katika shughuli za mafuta na gesi asilia hazipatikani ndani ya Zanzibar, bidhaa na huduma hizo zitatolewa na kampuni zilizoingia ubia na kampuni zilizopo Zanzibar.

(4) Kampuni zilizopo Zanzibar zilizotajwa katika kifungu kidogo cha (3), ni lazima ziwe na hisa isiyopunguwa asilimia kumi na tano (15%) katika ubia.

(5) Kwa madhumuni ya kifungu kidogo cha (1) na (2), Kampuni, mkandarasi na mkandarasi mdogo watatayarisha na kuwasilisha kwa Mamlaka mpango wa manunuzi wa angalau miaka mitatu unaoonesha pamoja na mambo mengine, matumizi ya huduma za ndani ya Zanzibar katika bima, fedha, sheria, akaunti za benki na huduma za kiafya, na bidhaa zinazozalishwa au zinazopatikana Zanzibar.

(6) Kampuni, wakandarasi na mtu mwingine yeyote atahakikisha kuwa, taasisi zilizotajwa katika kifungu kidogo cha kwanza zitaijulisha Mamlaka kuhusiana na:

(a) kiwango, afya, usalama na viwango vya mazingira zinavyohitajika na Kampuni au mkandarasi;

(b) mikataba inayotarajiwa kwa haraka kama iwezekanavyo; na

(c) kuendana na mipango ya huduma za jamii iliyoidhinishwa.

(7) Taasisi zilizotajwa katika kifungu kidogo cha (1):

(a) zitakuwa na uwezo wa kuongeza thamani ili kukidhi viwango vya afya, usalama na mazingira ya shughuli za mafuta na gesi asilia zilizofanywa na Kampuni na mkandarasi; na

(b) zitaidhinishwa kwa mujibu wa vigezo vilivyoelezwa na Kanuni.

(8) Ndani ya siku sitini baada ya kumalizika mwisho wa kila mwaka wa fedha, Kampuni itawasilisha kwa Mamlaka ripoti ya ufanisi wake, ufanisi wa wakandarasi na wakandarasi wadogo katika matumizi ya bidhaa na huduma za Wazanzibar katika mwaka huo wa fedha.

(9) Mkandarasi atawasilisha kwa Mamlaka:

(a) ripoti ya utekelezaji wa programu chini ya kifungu hiki kama ilivyoelezwa na Kanuni; na

(b) programu kamili ya maendeleo ya mtowaji wa huduma wa ndani kwa mujibu wa mpango wa huduma za jamii ulioidhinishwa.

(10) Kwa madhumuni ya Sheria hii "kampuni za ndani" maana yake ni kampuni au kampuni tanzu iliyosajiliwa chini ya Sheria ya Makampuni, ambayo nyingi ya hisa zake zinamilikiwa na Wazanzibari.

Mafunzo na ajira.

**135.-(1)** Kampuni na mkandarasi, ndani ya miezi kumi na mbili baada ya kupata kila leseni, na kila baada ya kukamilisha mwaka mmoja wa kupewa leseni hiyo, itawasilishwa kwa Mamlaka kwa ajili ya kuidhinishwa, programu kamili ya ajira na mafunzo kwa Wazanzibari kwa mujibu wa mpango wa huduma za jamii ulioidhinishwa.

(2) Programu itatoa mafunzo na ajira kwa Wazanzibari katika awamu zote za shughuli za uendeshaji za mafuta na gesi asilia na kuzingatia jinsia, usawa na watu wenye mahitaji maalum, jamii iliyozunguka na mpango wa mafanikio kwa mujibu wa Sheria ya Ajira na Sheria ya Uhusiano Kazini.

(3) Endapo programu au udhamini wa masomo uliopendekezwa kutolewa chini ya kifungu hiki umeidhinishwa na Mamlaka, hautobadilishwa bila ya ruhusa ya Mamlaka.

(4) Kampuni na mkandarasi watawasilisha kila mwaka kwa Mamlaka, ripoti inayohusiana na utekelezaji wa programu chini ya kifungu hiki.

(5) Katika kifungu hiki "jamii zilizozunguka" maana yake ni wakaazi wa eneo ambalo shughuli za mafuta na gesi asilia zinafanyika.

Mafunzo na uhaulishaji taaluma.

**136.-(1)** Ripoti iliyotajwa chini ya kifungu cha 135(4) itajumuisha:

(a) programu ya mafunzo iliyoelezwa kwa uwazi kwa ajili ya wafanyakazi wa Kizanzibari wa Kampuni na mkandarasi, ambayo yanaweza kufanyika ndani au nje ya Zanzibar na inaweza kujumuisha udhamini wa masomo na misaada mengine ya fedha iliyolenga katika elimu;

(b) kujikubalisha kwa Kampuni na mkandarasi kwa ajili ya kuongeza uhaulishaji wa taaluma katika kiwango cha hali ya juu kwa Wazanzibari na kuazisha uwezo wa kiuongozi na kiufundi na mambo mengine yoyote yanayofaa kwa kazi za kiufundi zikijumuisha ufafanuzi wa taarifa.

(2) Mamlaka inaweza kutayarisha Kanuni ndogo ndogo na miongozo zitakazoelezea matakwa kwa Kampuni na mkandarasi kwa ajili ya kutoa uhaulishaji wa teknolojia na utaalamu unaohusiana na sekta ya mafuta na gesi asilia kwa Wazanzibari ambao wameajiriwa katika sekta hiyo.

(3) Uhaulishaji wa teknolojia ulioainishwa chini ya kifungu kodogo cha (1) utakuwa ni wajibu wa pamoja baina ya Serikali, Kampuni na mkandarasi.

(4) Kampuni na mkandarasi watatakiwa kuandaa ripoti kuhusiana na maendeleo yaliyofanywa kwa Wazanzibari juu ya mpango wa mafunzo na hatua zilizochukuliwa na mkandarasi kuziba mwanya kwa mafunzo yaliyoainishwa.

Jukumu la ushirikishaji wa jamii.

**137.-(1)** Kampuni na mkandarasi kwa kila mwaka, wataandaa kwa pamoja Mpango wa Ushirikishaji Jamii utakaokubalika na mamlaka ya Serikali ya mtaa husika kwa kuzingatia Mpango Mkakati wa Ushirikishaji Jamii Zanzibar.

(2) Mpango ulioandaliwa chini ya kifungu kidogo cha (1) utazingatia shughuli za kimazingira, kijamii, kiuchumi na kiutamaduni kuhusiana na vipaumbele vya Serikali ya mtaa ya jamii inayozunguka.

(3) Mpango wa Ushirikishaji Jamii Zanzibar uliotajwa chini ya kifungu kidogo cha (1) utawasilishwa na Kampuni kwa mamlaka ya Serikali ya mtaa kwa kuzingatiwa na kuidhinishwa.

(4) Kwa mujibu wa masharti ya kifungu hiki, kila mamlaka ya Serikali ya mtaa:

(a) itasimamia utekelezaji wa hatua za Mpango wa Ushirikishaji Jamii Zanzibar; na

(b) kutoa muamko kwa jamii katika maeneo ambayo mradi wa mafuta na gesi asilia unafanyika.

Kiapo cha uadilifu.

**138.-(1)** Kampuni na mkandarasi ambao wanaojishughulisha katika shughuli za mafuta na gesi asilia chini ya Sheria hii watalazimika kufuata kiapo cha uadilifu.

(2) Kiapo cha uadilifu kilichotajwa chini ya kifungu kidogo cha (1) kitajumuisha matakwa yafuatayo:

(a) usimamizi wa shughuli zilizowekwa kwa uadilifu wa hali ya juu;

(b) kuacha kujishirikisha katika mpangilio wowote ambao utadhoofisha au kwa namna yoyote unahatarisha mfumo wa usimamizi wa kifedha nchini;

(c) kuacha kujishirikisha katika jambo lolote ambalo utadhoofisha au kwa namna yoyote unahatarisha mfumo wa kodi;

(d) kuacha kujishirikisha katika jambo lolote ambalo linapingana na malengo ya kiuchumi, sera na mikakati ya kiuchumi ya nchi;

(e) kuacha kujishirikisha katika jambo lolote ambalo linadhoofisha au vyenginevyo linapingana na usalama wa taifa; na

(f) kuendeleza kuwakatia bima dhidi ya hasara, madhara au uharibifu wa mazingira, jamii, mtu mmoja mmoja na mali, ambayo inaweza kusababisha utekelezaji wa shughuli za mafuta na gesi asilia.

(3) Mtu yeyote ambae atashindwa kutii kiapo cha uadilifu atakuwa amevunja masharti ya leseni au kibali kujihusisha na shughuli za mafuta na gesi asilia na leseni ya kibali hicho kitachukuliwa kuwa kimebatilishwa au kufutwa na Serikali itakuwa na haki ya kuchukua miundombinu iliyoelezwa kwa mujibu wa Sheria hii.

## SEHEMU YA NANE
## MAKOSA NA ADHABU

Kumzuia Afisa aliyeidhinishwa.

**139. Mtu ambae:**

(a) bila ya sababu za msingi, atamzuia au atamshambulia Afisa aliyeidhinishwa katika kutekeleza majukumu yake chini ya Sheria hii; au

(b) kwa kujua au kwa uzembe atatoa maelezo au kutoa waraka ambao wa uongo au unaopotosha ukweli kwa afisa aliyidhinishwa kutekeleza majukumu na kazi zake chini ya Sheria hii,

atakuwa ametenda kosa na atalazimika kulipa faini ya fedha za kitanzania zenye thamani isiyopungua Dola za Kimarekani Laki Moja au kifungo kisichopungua miaka mitano au vyote kwa pamoja.

Kuzuia Kampuni na mkandarasi.

**140.** Mtu ambae bila ya sababu ya msingi, ataizuia au kuishambulia Kampuni au mkandarasi kabla au baada ya utekelezaji wa shughuli yoyote ambayo leseni imetolewa kufanya hivyo chini ya Sheria hii au leseni yake, atakuwa ametenda kosa na atalazimika kulipa faini ya fedha za kitanzania zenye thamani isiyopungua Dola za Kimarekani Laki Tano au kifungo kisichopungua miaka mitano au vyote kwa pamoja.

Makosa yaliyofanywa na taasisi au mtu binafsi.

**141.-(1)** Endapo kosa limefanywa na taasisi na likathibitika kuwa lilifanywa na taasisi kwa ridhaa au kwa kushiriki, au limefanywa kwa uzembe chini ya uwezo wa mkurugenzi, meneja, katibu au afisa mwengine yeyote anaefanana nao wa taasisi hiyo au mtu yeyote ambae aliedhamiria kutenda kosa kwa uwezo wowote aliokuwa nao kama taasisi atakuwa ametenda kosa na atalazimika kulipa faini ya fedha za Kitanzania zinazolingana na Dola za Kimarekani zisizopungua Elfu Hamsini.

(2) Mtu mwengine yeyote ambae ametenda kosa chini ya kifungu kidogo cha (1), atalazimika kulipa faini ya fedha za Kitanzania zinazolingana na Dola za Kimarekani zisizopungua Elfu kumi au kifungo kisichopungua miaka mitano au vyote kwa pamoja.

Amri ya kutaifisha.

**142.(1)** Endapo mtu ametiwa hatiani kwa kosa chini ya Sheria hii, mahakama inaweza, pamoja na adhabu yoyote iliyotolewa kutoa:

(a) amri ya kutaifisha fedha taslim, hundi, nyaraka, huduma, vyombo vya usafiri wa ardhini, angani na majini au amri ya kuchukua vifaa vilivyotumika wakati wa kutenda kosa; na

(b) amri ya:

(i) kutaifisha mafuta na gesi asilia yaliyopatikana wakati wa kutenda kosa;

(ii) mtu kuilipa Serikali kiwango cha fedha kilichosawa na kile kilichopatikana wakati wa mauzo wa mafuta na gesi asilia; au

(iii) mtu kuilipa Serikali thamani ya mafuta na gesi asilia iliyopimwa, kutathminiwa na mahakama kuendana na kiwango kilichopatikana au kwa ajili ya malipo ya fedha ya sehemu ya kiwango hicho kwa mazingira yoyote mahakama inaona inafaa.

(2) Endapo mahakama imeridhika kwamba amri iliyotolewa chini ya kifungu kodogo cha (1)(b)(i) kwa sababu yoyote ile haikutekelezwa, mahakama inaweza, kufuatia maombi ya mtu ambae madai yamewasilishwa, kutengua amri na kutoa amri iliyoelezwa chini ya kifungu kidogo cha (1)(b)(ii) au (iii).

(3) Mahakama inaweza, kabla ya kutoa amri yoyote chini ya kifungu hiki, kutaka notisi itolewe na kumsikiliza mtu yeyote ambae mahakama inaona inafaa.

Kwenda kinyume na maamuzi na kutoa amri chini ya Sheria hii.

**143.** Mtu ambae bila ya kuwa na sababu ya msingi atakwenda kinyume na maelekezo yoyote yaliyotolewa chini ya Sheria hii, atakuwa ametenda kosa na atalazimika kulipa faini ya fedha za Kitanzania zinazolingana na:

(a) ikiwa ni mtu binafsi, faini isiyopungua Dola za Kimarekani Elfu Hamsini au kifungo kisichopungua miaka kumi au vyote kwa pamoja; au

(b) ikiwa ni taasisi, faini isiyopungua Dola za Kimarekani Laki Mbili na Elfu Hamsini.

Makosa ya jumla.

**144.** Mtu ambae:

(a) kwa maombi yoyote chini ya Sheria hii, kwa kujua au kwa uzembe atatoa au kuruhusu kutolewa taarifa ambazo ni za uongo au zenye kupotosha juu ya jambo maalum;

(b) kwa ripoti yoyote au kiapo kilichowasilishwa kwa mujibu wa Sheria hii au leseni, kwa kujua au kwa uzembe akajumuisha, au akaruhusu kujumuishwa, taarifa ambazo ni za uongo au zenye kupotosha jambo maalum; au

(c) kwa kuweka au kuhifadhi, au kifaa katika kukiweka au kukihifadhi kwa ajili ya shughuli za mafuta na gesi asilia au kukiweka mahala popote kwa nia ya kumpotosha mtu mwengine kuweza kufikia kwenye hifadhi iliyopo katika sehemu hiyo,

atakuwa ametenda kosa na atalazimika kulipa faini ya fedha za Kitanzania zinazolingana:

(i) ikiwa mtu binafsi, si chini ya Dola za Kimarekani Laki Mbili na Hamsini Elfu au kifungo kisichopungua miaka kumi au vyote kwa pamoja; au

(ii) ikiwa ni taasisi, si chini ya Dola za Kimarekani Laki Tano au kifungo kisichopungua miaka mitano au vyote kwa pamoja.

Makosa na adhabu.

**145.-(1)** Mtu ambae:

(a) bila ya sababu za msingi, atakataa, atachelewa au atashindwa kutoa nyaraka yoyote au taarifa nyengine zinazohusuiana na shughuli za mafuta na gesi asilia na uwekaji wa vifaa ambavyo vinaweza kuhitajika kutolewa chini ya Sheria hii;

(b) kwa makusudi kupotosha au kuidanganya mamlaka yoyote au afisa aliyeidhinishwa anapofanya kazi zake au kuzuia taarifa;

(c) atatangaza au vyenginevyo atatoa taarifa inayopingana na Sheria hii;

(d) bila ya sababu za msingi atapinga au kumzuia mkaguzi au afisa mwengini wa mamlaka au mtu mwengine yeyote anaefanya kwa niaba ya mamlaka, kuingia au kuchunguza sehemu yoyote au kumsimamisha na kupekuwa chombo chochote au vyenginevyo kufanya majukumu yake na haki zake chini ya Sheria hii;

(e) kukataa, kuchelewesha au kushindwa kufuata amri, katazo, maelekezo, matakwa au notisi iliyotolewa kisheria na kutumwa kwake au kuchapishwa au vyenginevyo kutolewa chini ya Sheria hii;

(f) kwenda kinyume na masharti ya Sheria hii, amri au kanuni zilizofanywa chini ya Sheria hii;

(g) kutoa taarifa za siri wakati ambapo bado ni mfanyakazi wa Mamlaka au mtumishi wa umma anaehusika na sekta ya mafuta na gesi asilia au anaposita kuwa mtumishi wa Umma au Mjumbe wa Bodi ya Mamlaka au taasisi ambayo amepata taarifa hizo wakati wa ajira yake,

atakuwa ametenda kosa na atalazimika kulipa faini ya fedha za Kitanzania zinazolingana na Dola za Kimarekani zisizopungua Elfu Ishirini au kifungo kisichozidi miaka mitano au vyote kwa pamoja.

(2) Mtu ambae atajaribu au atasaidia kubadilisha, kuondosha au kuunganisha bomba lolote au miundombinu ya mafuta na gesi asilia bila ya kupata ridhaa ya Kampuni na mkandarasi atakuwa ametenda kosa na atalazimika kulipa faini ya fedha za Kitanzania zinazolingana na Dola za Kimarekani zisizopungua Elfu Kumi au kifungo kisichopungua miaka mitano au vyote kwa pamoja.

(3) Mtu ambae ataendelea kufanya kosa atakuwa ametenda kosa na atalazimika kulipa faini ya fedha za Kitanzania zinazolingana na Dola za Kimarekani Mia Tano kwa kila siku ambayo ameendelea kutenda kosa.

(4) Mtu ambae:

(a) atahujumu uendeshaji wa miundombinu ya mafuta na gesi asilia;

(b) ataharibu kazi za mfumo wa mafuta na gesi asilia;

(c) atafanya jambo lolote ambalo litahatarisha kazi za mfumo wa mafuta na gesi asilia; au

(d) ataacha kufanya, au vyenginevyo kuacha kufanya jambo ambalo analazimika kufanya kwa mujibu wa sheria au mkataba au amri halali, ambayo itasababisha uhujumu, uharibifu au kuhatarisha kazi za mfumo wa mafuta na gesi asilia,

atakuwa ametenda kosa na atalazimika kulipa faini ya fedha za Kitanzania zinazolingana na Dola za Kimarekani zisizopungua Elfu Kumi au kifungo kisichozidi miaka mitano au vyote kwa pamoja.

Muunganisho wa Makosa kwa Mamlaka.

**146.-(1)** Kufuatia maombi yaliyofanywa na mtu yeyote ambae ametenda kosa zaidi ya kosa lililoelezwa chini ya kifungu 145(4), Mamlaka inaweza kuunganisha makosa yaliyofanywa na mtu yeyote chini ya Sheria hii au Kanuni zake kwa kumtaka mtu huyo kulipa faini kwa ajili ya kosa hilo, ikizingatiwa kwamba mtu huyo:

(a) amekubali kwa maandishi kwamba ametenda kosa na atachukua hadhari ya kutokurejea tena; na

(b) atalipa madeni yake au malipo mengine yoyote yanayostahiki kulipwa chini ya Sheria hii au Kanuni.

(2) Ikiwa kosa la jinai limefunguliwa dhidi ya mtu, uwezo ulioelezwa chini ya kifungu hiki hakitatumika bila ya kupata ridhaa ya maandishi kutoka kwa Mkurugenzi wa Mashtaka Zanzibar.

(3) Mtu ambae amekubali kulipa faini chini ya kifungu kidogo cha (1), atapatiwa na Mamlaka hati itakayoelezea asili ya kosa, tarehe au muda uliotokezea, faini iliyolipwa na masharti mengine yaliyomo katika makubaliano.

(4) Ikiwa faini imetolewa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki haikulipwa pale ilipohitajika, Mamlaka inaweza kufungua kesi mahakamani au kuchukua hatua stahiki kwa ajili ya kurejesha faini kwa namna nyengine yoyote inayoruhusiwa na Sheria hii kwa ajili ya kurejesha deni ambalo halijalipwa.

(5) Faini iliyowekwa chini ya kifungu kigogo cha (1) cha kifungu hiki haitochukuliwa kama ni adhabu kwa kosa lililofanywa, na ikizingatiwa kwamba deni limelipwa kwa ukamilifu, hakuna hatua zitakazochukuliwa kwa kosa linalodaiwa kufunguliwa au kuendelezwa.

(6) Endapo mtu yeyote atakubali kuunganishwa katika kosa, hati ya kuunganishwa huko haitakatiwa rufaa na inaweza kutekelezwa kwa namna sawa kama ambavyo hukumu au amri imetolewa na Mahakama Kuu.

## SEHEMU TISA
## UTATUZI WA MIGOGORO

Mamlaka inaweza kutatua migogoro.

**147.-(1)** Mamlaka inaweza kuhoji na kutatua migogoro yote baina ya mtu anaejishughulisha na shughuli za utafutaji au uendelezaji wa mafuta na gesi asilia, ama miongoni mwao au wanaohusiana nao na pande nyengine zisizokuwa Serikali zinazojishughulisha na shughuli za mafuta na gesi asilia, inayohusiana na:

(a) mipaka ya eneo lolote la utafutaji na uendelezaji wa mafuta na gesi asilia;

(b) kitendo chochote kilichofanywa au kuachwa kufanywa, au kudaiwa kufanywa au kuachwa kufanywa, wakati wa shughuli au kabla ya shughuli za utafutaji au uendelezaji wa mafuta na gesi asilia;

(c) tathmini na malipo ya fidia kwa mujibu wa Sheria hii; au

(d) mambo mengine yoyote yanayohusiana na shughuli za utafutaji wa matufa na gesi asilia.

(2) Mamlaka inaweza kutoa hukumu au amri ambayo inaona inafaa kwa madhumuni ya utekelezaji wa maamuzi yake katika madai yaliyopo chini ya sehemu hii, na inaweza kutoa amri ya malipo, kwa upande wowote ule wenye mgogoro kuhusu fidia kama itakavyoona inafaa kwa upande wowote mwengine wenye mgogoro.

(3) Mamlaka inaweza, kukataa kutatua mgogoro wowote ulioelezwa katika sehemu hii, na ikifanya hivyo itatoa taarifa kwa maandishi kwa pande zenye mgogoro.

Utekelezaji wa hukumu na amri za Mamlaka.

**148.-(1)** Mamlaka inaweza, kutuma nakala zilizothibitishwa za hukumu au amri zilizotolewa na mamlaka kwa mahakama yoyote iliyopo ndani ya mamlaka ya eneo husika kwa ajili ya rufaa, mahakama ya madai itatekeleza hukumu na amri ya mamlaka kwa namna iliyo sawa ambayo inatekeleza maamuzi na amri zake.

(2) Ada zinazolipwa kufuatia utekelezaji wa hukumu au amri ni zile ambazo zinalipwa kufuatia utekelezaji wa hukumu au amri iliyotolewa na mahakama husika.

Kutenganishwa kwa uwezo wa Mahakama.

**149.** Mtu hatafungua madai yake katika mahakama inayohusiana na mgogoro wa aina yoyote ulioainishwa katika kfiungu cha 147 isipokuwa mamlaka ilikataa kufuatia kifungu kidogo cha (3) cha kifungu hiki kuamua mgogoro huo.

Taratibu zinazohusiana na madai.

**150.** Mamlaka inaweza, kuweka taratibu zinazohusiana na uanzishaji na usimamizi wa madai chini ya kifungu cha 147 na kuweka kumbukumbu na taarifa za ushahidi unaohusiana na madai hayo.

## SEHEMU YA KUMI
## MASHARTI YA MPITO

Mikataba iliyoingiwa awali.

**151.-(1)** Serikali haitokuwa na wajibu au dhamana yoyote au inayohusiana na mikataba iliyoingiwa awali inayohusiana na shughuli za mafuta na gesi asilia, na haitokuwa mrithi wa mikataba hiyo.

(2) Bila ya kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (1), Serikali inaweza ikiona kuna haja ya kufanya hivyo, kupitia upya Mikataba iliyoingiwa awali na kuweka masharti mapya ya utekelezaji kwa kuzingatia masharti ya Sheria hii.

(3) Serikali haitokuwa na wajibu wa deni lolote au wajibu wa madeni mengine yaliyoingiwa kabla ya kutumika kwa Sheria hii.

(4) Waziri anaweza kugawa upya vitalu ambavyo kwamba vinaingiliana na mipaka ndani ya Jamhuri ya Muungano kulingana na maeneo yaliyomo katika eneo la Zanzibar na Tanzania Bara na masharti ya makubaliano mapya ya mafuta na gesi asilia yataakisi ugawaji mpya wa vitalu hivyo.

## SEHEMU YA KUMI NA MOJA
## MASHARTI YA JUMLA

Kutumika leseni kama dhamana

**152.-(1)** Waziri anaweza baada ya kushauriwa na Mamlaka kuidhinisha kutumiwa leseni ya uendelezaji wa mafuta na gesi asilia kwa Kampuni na mkandarasi chini ya Sheria hii kama ni dhamana ya hisa ya leseni yake ikiwa ni sehemu ya kugharamia shughuli zinazohusika na leseni ya uzalishaji wa matufa na gesi asilia kwa namna ambavyo ilivyoelezwa katika Kanuni.

(2) Dhamana iliyotajwa katika kifungu kidogo cha (1) itakuwa ni hisa ya Kampuni au stahiki ya mapato ya baadae iliyopatikana kutokana na uzalishaji wa mafuta na gesi asilia kama ilivyoainishwa katika mikataba.

Mgogoro wa maslahi.

**153.-(1)** Afisa katika Utumishi wa Umma ambae anahusika na utekelezaji wa Sheria hii, kwa uwezo wake binafsi, kwa kujua moja kwa moja au vyenginevyo, hatopata, hatojaribu kupata au kuchukua:

(a) maslahi katika leseni ya shughuli ya mafuta na gesi asilia;

(b) moja kwa moja au vyenginevyo maslahi ya kiuchumi, maslahi ya ushiriki au hisa ya chombo ambacho kimeidhinishwa chini ya Sheria hii kutekeleza shughuli za mafuta na gesi asilia; au

(c) moja kwa moja au vyenginevyo maslahi ya kiuchumi, maslahi ya ushiriki au hisa katika taasisi ambayo inazalisha bidhaa au inatoa huduma kwa Kampuni na mkandarasi chini ya Sheria hii.

(2) Mtu ambae anapingana na kifungu kidogo cha (1) atakuwa ametenda kosa na atalazimika kulipa faini ya fedha za Kitanzania zinazolingana na Dola za Kimarekani zisizopungua Elfu Ishirini na Tano au kifungo kisichozidi miaka mitano au vyote kwa pamoja.

(3) Katika uendeshaji wa madai ya kosa chini ya kifungu hiki ya kupata au kuendeleza maslahi ya aina yoyote yaliyotajwa chini ya kifungu kidogo cha (1), yatatosha kuwa ni utetezi ikiwa mtu aliyeshtakiwa anathibitisha kwamba maslahi yamepatikana kwa mujibu wa Sheria.

Mfuko wa mapato ya mafuta na gesi asilia.

**154.** Kwa madhumuni ya kuhakikisha kwamba:

(a) uwazi na uwajibikaji katika ukusanyaji, mgao, matumizi na usimamizi wa mapato ya mafuta na gesi asilia;

(b) mapato ya mafuta na gesi asilia yanatumika kwa maendeleo endelevu ya sekta ya mafuta na gesi asilia na faida ya kizazi kilichopo na kinachokuja,

Baraza la Wawakilishi litatunga sheria inayoanzisha Mfuko wa Mapato ya Mafuta na Gesi Asilia ambao kutawekwa mapato yaliyotokana na shughuli za mafuta na gesi asilia.

Kanuni.

**155.-(1)** Waziri anaweza kutunga Kanuni zitakazoainisha mambo yaliyomo katika Sheria hii ambayo yatahitajika au kuruhusika kuelezewa kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa Sheria hii.

(2) Bila ya kuathiri kifungu kidogo cha (1), Waziri atalazimika kutunga Kanuni zinazoelezea:

(a) utafutaji wa mafuta na gesi asilia na kufanya shughuli na kutekeleza kazi kwa ajili hiyo;

(b) uzalishaji wa mafuta na gesi asilia na kufanya shughuli na kutekeleza kazi kwa ajili hiyo;

(c) kulinda na kuhifadhi takataka zinazotokana na mali ghafi, ama za mafuta na gesi asilia au vyenginevyo, kwenye ardhi ambayo Sheria hii inatumika;

(d) ujenzi, upangaji na uendeshaji wa miundombinu katika kutekeleza shughuli na kutekeleza kazi, kwa madhumuni yote yanayohusiana nayo;

(e) udhibiti wa uingiaji na kuzuia upotevu wa mafuta na gesi asilia, maji, gesi zisizokuwa mafuta na gesi asilia au kufufua mambo mengine yenye sumu na athari;

(f) kuzuia upotevu wa maji au maji maji yanayotumika wakati wa uchimbaji au mchanganyiko wa maji au mambo mengine yoyote yanayohusiana nayo;

(g) uondoshaji wa miundombinu, vifaa na mali nyengine zilizoletwa Zanzibar zinazohusiana na utafutaji, uzalishaji au usafirishaji wa mafuta na gesi asilia ambavyo havitumiki au havikusudiwi kutumiwa katika shughuli za utafutaji, uzalishaji au usafirishaji;

(h) kuongeza nguvu za msukumo au kupunguza katika hifadhi ya mafuta na gesi asilia na kusarifu mafuta na gesi asilia;

(i) uzalishaji wa mafuta na gesi asilia kutoka katika hifadhi kwa kutumia njia ya kati na ya juu na mbinu zitazotumika katika uzalishaji huo;

(j) matumizi ya visima na matumizi ya ardhi kwa ajili ya uondoshaji wa mafuta na gesi asilia, maji na vitu vyengine vinavyozalishwa;

(k) kuhusiana na utafutaji au uzalishaji wa mafuta na gesi asilia;

(l) viwango au njia ya kuweka viwango, ambavyo mafuta na gesi asilia na maji yanaweza kuzalishwa kutoka katika kisima chochote au hifadhi ya mafuta na gesi asilia;

(m) njia zitakazotumika kwa kupima mafuta na gesi asilia, maji na mambo mengine yanayotoka katika kisima;

(n) viwango vya usalama vya mafuta na gesi asilia, afya na usalama au watu walioajiriwa katika utafutaji wa uzalishaji au usafirishaji wa mafuta na gesi asilia;

(o) kuchukua, kulinda na kuwasilisha kwa Mamlaka vipande vya miamba, vipande vidogo vidogo vya miamba na sampuli zinazotoka katika visima na sampuli za mafuta na gesi asilia na maji;

(p) kuipatia Mamlaka taarifa, mrejesho wa taarifa na taarifa nyenginezo;

(q) kuchukua taarifa za kisima au mwelekeo wa utafiti au kufanya utafiti mwengine ndani ya visima;

(r) mipaka ya urejeshaji wa gharama inayohusiana na leseni ya utafutaji na uendelezaji wa mafuta na gesi asilia;

(s) utaratibu wa malipo yanayohusiana na mrahaba, ziada, faida, ada au malipo mengine yoyote;

(t) uangalizi na usimamizi wa kumbukumbu na ripoti; au

(u) kanuni nyengine yoyote kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa masharti na madhumuni ya Sheria hii.

## JADWELI LA KWANZA

## MWENENDO WA BODI
**{ Chini ya Kifungu Cha 16 }**

---

Kikao cha Bodi.

**1.(1)** Bodi itakutana kikao cha kawaida angalau mara moja kwa kila baada ya miezi mitatu.

(2) Bodi inaweza kukutana kikao cha dharura wakati wowote inapohitajika kufanya hivyo.

(3) Vikao vya Bodi vitafanyika ndani ya Zanzibar, isipokuwa ikijitokeza haja ya kufanya kikao nje ya Zanzibar baada ya kushauriana na Waziri.

Kuitisha kikao.

**2.-(1)** Mikutano yote ya Bodi itaitishwa na Mwenyekiti au asipokuwepo itaitishwa na Makamo Mwenyekiti.

(2) Mwenyekiti au asipokuwepo, Makamo Mwenyekiti, ataitisha mkutano maalum wa Bodi kufuatia ombi la maandishi lililosainiwa na wajumbe zaidi ya nusu wa Bodi na atawezesha kikao hicho kufanyika ndani ya siku ishirini na moja za kupokea ombi hilo.

(3) Iwapo Mwenyekiti na Makamo Mwenyekiti hawapo, wajumbe waliopo watachagua mjumbe mmoja miongoni mwao kuendesha kikao hicho na mjumbe aliechaguliwa atakuwa na uwezo na kufanya kazi zote za Mwenyekiti.

Makamo Mwenyekiti.

**3.** Bodi itamchagua mmoja miongoni mwao kuwa Makamo Mwenyekiti wa Bodi.

Maisha ya Bodi.

**4.(1)** Mwenyekiti wa Bodi atashikilia nafasi hiyo kwa muda wa miaka mitatu kuazia tarehe ya uteuzi na anaweza kuteuliwa tena kwa vipindi vyengine.

(2) Isipokuwa kwa mjumbe ambae yupo kwa mujibu wa nafasi yake, mjumbe mwengine wa Bodi, isipokuwa kama uteuzi wake umefutwa au kukoma kwa njia nyengine yoyote, atashikilia nafasi hiyo kwa muda wa miaka mitatu na anaweza kuteuliwa tena kwa vipindi vyengine.

Akidi ya Kikao.

**5.** Akidi ya kikao chochote cha Bodi itakuwa zaidi ya nusu ya wajumbe.

Maamuzi ya Bodi.

**6.-(1)** Bodi itafanya maamuzi yake kwa maafikiano na iwapo wamekosa kuwafikiana maamuzi yatafikiwa kwa kupiga kura na iwapo kutakuwa na usawa wowote katika kura Mwenyekiti au Makamo Mwenyekiti au mjumbe anaendesha kikao hicho atakuwa na kura ya turufu.

(2) Bila ya kujali kifungu kidogo cha (1) maamuzi yanaweza kufanywa na Bodi kwa kugawa karatasi kwa wajumbe ambapo kila mjumbe ataeleza maoni yake kwa maandishi isipokuwa kwamba mjumbe yeyote anaweza kutaka uamuzi huo uwasilishwe kwa mjadala katika kikao kamili cha Bodi.

(3) Azimio lililopitishwa kwa maandishi na kusainiwa na wajumbe wote waliopo Zanzibar kwa wakati huo, lakini wasipungue wajumbe watano, utakuwa uamuzi sahihi kama uliofanywa katika kikao, isipokuwa kwamba mjumbe huyo anaweza kutaka kwamba jambo hilo liwasilishwe katika kikao cha Bodi kinachofuata bila kujali sahihi za wajumbe.

Kumbukumbu za kikao cha Bodi.

**7.** Bodi itawezesha kunakiliwa na kutunzwa kumbukumbu zote za vikao vyake na kumbukumbu za kila kikao cha Bodi zitathibitishwa katika kikao kinachofuata na kusainiwa na Mwenyekiti wa kikao na Katibu wa Bodi.

Mualikwa.

**8.** Bodi inaweza kumualika mtu yeyote ambae si mjumbe, kuhudhuria maamuzi ya kikao cha Bodi kama mtaalam lakini mualikwa huyo hatokuwa na haki ya kupiga kura.

Kutangaza maslahi ya mjumbe.

**9.(1)** Mjumbe ambae moja kwa moja au kwa njia nyengine anamaslahi katika mkataba au mkataba unaopendekezwa au jambo lolote linalotaka kujadiliwa na Bodi, atatangaza maslahi yake kwa Bodi na atajizuia kushiriki katika maajadiliano ya jambo hilo.

(2) Mjumbe ambae anamaslahi katika jambo lolote ambalo limejadiliwa na Bodi na mjumbe huyo ameshindwa kutangaza maslahi yake na akashiriki katika majadiliano ya Bodi, atasitishwa kuwa mjumbe wa Bodi.

Kujiuzulu kwa mjumbe.

**10.-(1)** Mwenyekiti au mjumbe yeyote wa Bodi anaweza, wakati wowote kujiuzulu kwa kutoa notisi ya maandishi kwa mamlaka iliyemteua na kuanzia tarehe hiyo iliyoainishwa katika notisi au, iwapo hakuna tarehe iliyoainishwa, kuanzia tarehe iliyopokelewa notisi na mamlaka ya uteuzi, atakoma kuwa mjumbe.

(2) Endapo mtu amekoma kuwa Mwenyekiti au mjumbe wa Bodi kama hali itakavyokuwa, kwa sababu yoyote kabla ya muda wake kumalizika, mamlaka ya uteuzi itamteua mtu mwengine kujaza nafasi yake na mtu atakaeteuliwa atashikilia nafasi hiyo kwa muda uliobakishwa na mtangulizi wake.

(3) Endapo mjumbe yeyote amekosekama katika vikao vitatu mfululizo vya Bodi bila ya sababu ya msingi, Mwenyekiti wa Bodi atatoa taarifa kwa Waziri juu ya jambo hilo na Waziri atatengua uteuzi wa mjumbe huyo na atateua mjumbe mwengine kujaza nafasi yake na mtu atakaeteuliwa atashikilia nafasi hiyo kwa muda uliobakishwa na mtangulizi wake.

(4) Endapo Mwenyekiti amekosekana katika vikao vitatu mfululizo bila ya sababu ya msingi, Makamo Mwenyekiti atatoa taarifa kwa Waziri, ambae nae atawasilisha taarifa hiyo kwa Rais, akiona inafaa atamteua Mwenyekiti mwengine.

Nafasi tupu ya mjumbe.

**11.-(1)** Nafasi ya mjumbe wa Bodi itakuwa wazi:

(a) kwa kufariki;

(b) iwapo bila sababu ya msingi ameshindwa kuhudhuria vikao vitatu mfululizo;

(c) iwapo atajiuzulu au kwa njia yoyote ile atapoteza sifa za kuwa mjumbe wa Bodi; au

(d) iwapo atakuwa hawezi kutekeleza majukumu yake kwa sababu ya ugonjwa au afya ya akili.

(2) Kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii, yanayohusiana na akidi, Bodi inaweza kuendelea na shughuli zake bila ya kujali kuwepo kwa nafasi wazi kwa mjumbe na hakuna jambo wala mwenendo wa Bodi utakaobatilishwa kwa sababu tu ya udhaifu katika uteuzi wa mtu ambae anapaswa kuwa mjumbe.

Kamati za Bodi.

**12.-(1)** Katika kutekeleza kazi zake Bodi inaweza kuanzisha idadi ya kamati kutekeleza kazi maalum kama Bodi itakavyoamua.

(2) Mwenendo, masharti na mambo mengine yanayohusiana na kamati hiyo inayoanzishwa itakuwa kama itakavyoainishwa na Bodi.

Posho kwa wajumbe.

**13.** Mwenyekiti na wajumbe wengine wa Bodi wanapaswa kulipwa posho na ada katika viwango ambavyo Waziri ataamua mara kwa mara

Utaratibu wa vikao.

**14.** Kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii, Bodi itakuwa na uwezo wa kusimamia mienendo yake kuhusiana na vikao na utendaji wa shughuli zake ikijumuisha na kamati za Bodi.

Katibu wa Bodi.

**15.-(1)** Kutakuwa na Katibu wa Bodi ambae atateuliwa na Bodi.

(2) Katibu wa Bodi atakuwa na angalau shahada ya kwanza ya Sheria iliyojikita katika nyanja ya mafuta na gesi asilia na uzoefu usiopungua miaka mitano.

(3) Katibu atawajibika kwa Bodi, na atawajibika kuhakikisha kwamba:

(a) kumbukumbu za vikao vya Bodi vinachukuliwa kwa usahihi;

(b) kumbukumbu sahihi na zinazotosheleza za Bodi zinatunzwa kwa usahihi;

(c) utoaji taarifa uliosahihi wa vikao vya Bodi kwa wajumbe;

(d) anatoa ushauri sahihi kwa Bodi anapohitajika kufanya hivyo; na

(e) jambo jengine lolote ataloelekezwa na Bodi.

## JADWELI LA PILI

*(Limefanywa Chini ya Kifungu cha 101(1))*

## MRAHABA NA MGAO WA FAIDA

**1.** Mmiliki wa leseni kwa niaba yake na kwa niaba ya mkandarasi atatekeleza wajibu wake wa kulipa mrahaba kutokana na uzalishaji wa ujumla chini ya sheria hii kutoka katika eneo la mkataba, kwa kuwasilisha serekalini 12.5% kwa nchi kavu na 7.5% kwa eneo la baharini ya mafuta au gesi yote iliyozalishwa kabla ya kutoa gharama za uzalishaji wa mafuta au gesi asilia kwa kiwango hicho cha mrahaba au kwa namna abavyo Serikali itakavyoelekeza.

**2.** Faida ya serikali inayotokana na mafuta yaliyozalishwa katika eneo la mkataba hayatakuwa chini ya kiwango kilichotajwa katika jadweli hapo chini:

A. Viwango vya faida ya Serikali katika mafuta ghafi:

***i. Kwa eneo la nchi kavu***

| Kiwango cha kila siku cha mafuta mafuta ghafi kwa pipa | Mgao wa Serikali kwa asilimia | Mgao wa mkandarasi kwa asilimia |
|---|---|---|
| 0 - 12,499 | 50% | 50% |
| 12,500 - 24,999 | 55% | 45% |
| 25,000 - 49,999 | 60% | 40% |
| 50,000 - 99,999 | 65% | 35% |
| 100,000 - na zaidi | 70% | 30% |

***ii. Kwa eneo la baharini***

| Kiwango cha kila siku cha mafuta ghafi kwa pipa | Mgao wa serikali kwa asilimia | Mgao wa mkandarasi kwa asilimia |
|---|---|---|
| 0 – 49,999 | 50% | 50% |
| 50,000 - 99,999 | 55% | 45% |
| 100,000 - 149,999 | 60% | 40% |
| 150,000 - 199,999 | 65% | 35% |
| 200,000 - na zaidi | 70% | 30% |

***B. Viwango vya faida ya Serikali katika Gesi Asilia:***

***i. Kwa eneo la nchi kavu***

| Kiwango cha kila siku cha Gesi Asilia katika ujazo wa mita milioni kwa siku | Mgao wa serikali kwa asilimia | Mgao wa mkandarasi kwa asilimia |
|---|---|---|
| 0 - 19.99 | 60% | 40% |
| 20 - 39.99 | 65% | 35% |
| 40 - 59.99 | 70% | 30% |
| 60 - 79.99 | 75% | 25% |
| 80 - na zaidi | 80% | 20% |

ii. Kwa eneo la baharini

| Kiwango cha kila siku cha Gesi Asilia katika ujazo wa mita milioni | Mgao wa serikali kwa asilimia | Mgao wa mkandarasi kwa asilimia |
|---|---|---|
| 0 - 149.999 | 60% | 40% |
| 150 - 299.999 | 65% | 35% |
| 300 - 449.999 | 70% | 30% |
| 450 - 599.999 | 75% | 25% |
| 600 - 749.999 | 80% | 20% |
| 750 - na zaidi | 85% | 15% |

**Umepitishwa** na Baraza la Wawakilishi, tarehe 27 Septemba, 2016.

**{ RAYA ISSA MSELLEM }**
**KATIBU, BARAZA LA WAWAKILISHI**
**ZANZIBAR**